

**BUNGE LA TANZANIA**

---

**MAJADILIANO YA BUNGE**

---

**MKUTANO WA KUMI NA MOJA**

**Kikao cha Hamsini na Tatu – Tarehe 19 Juni, 2018**

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Naibu Spika (Mhe. Dkt. Tulia Ackson) Alisoma Dua*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tukae. Katibu.

**NDG. PAMELA PALLANGYO – KATIBU MEZANI:**

**HATI ZA KUWASILISHA MEZANI**

Hati ifuatayo iliwasilishwa mezani na:-

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU (K.n.y. WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO):**

Taarifa ya mwaka na Hesabu zilizokaguliwa za Bodi ya Mfuko wa Barabara kwa mwaka wa fedha 2014/2015 *(The Annual Report and Audited Accounts of the Roads Fund Board for the Financial Year 2014/2015)*.

**NAIBU SPIKA:** Katibu.

**NDG. PAMELA PALLANGYO – KATIBU MEZANI:**

**MASWALI NA MAJIBU**

Na. 447

**Kupandisha Hadhi Kituo cha Afya Sinza  
Kuwa Hospitali ya Wilaya**

**MHE. JOSEPH R. SELASINI (K.n.y. MHE. SAED A. KUBENEA)** aliuliza:-

Mheshimiwa Rais wa Awamu ya Nne alipotembelea Kituo cha Afya cha Palestina kilichopo Kata ya Sinza alitangaza kukipandisha hadhi kuwa Hospitali ya Wilaya. Hata hivyo, bado Serikali inaendelea kuipatia fedha hospitali hiyo kama Kituo cha Afya.

Je, ni lini Serikali itaitambua hospitali hiyo kama Hospitali ya Wilaya kwa kuipa fedha na vitendea kazi vinavyofanana na hadhi yake?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Saed Ahmed Kubenea, Mbunge wa Ubungo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Kituo cha Afya cha Palestina kimekuwa kinafanya kazi kama Hospitali ya Wilaya kufuatia tamko la Mheshimiwa Rais wa Awamu ya Nne la tarehe 11 Disemba, 2012.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya tamko hilo, ukaguzi ulifanyika na kubaini uhitaji wa kuongezewa eneo kwa ajili ya upanuzi wa huduma. Ifahamike wazi kuwa kituo hiki kilianzishwa ili kitoe huduma kama Kituo cha Afya, hivyo hakiwezi kuwa Hospitali ya Wilaya. Kwa kutambua umuhimu

wa kituo hiki, hatua zifuatazo zimechukuliwa kutatua baadhi ya changamoto:-

(i) Kwa mwaka wa fedha 2017/2018 ruzuku ya ununuzi wa dawa, vifaatiba na vitendanishi kutoka Bohari Kuu ya Dawa (MSD) imeongezeka hadi kufikia shilingi milioni 69 kutoka shilingi milioni 57.4 kwa mwaka wa fedha 2016/2017.

(ii) Madaktari Bingwa watatu wameshapelekwa katika kituo hiki kati ya watano wanaohitajika, kwa maana ya Madaktari Bingwa wa Watoto, wawili na Daktari wa Magonjwa ya Wanawake na Uzazi mmoja.

(iii) Katika mwaka wa fedha 2018/2019, kiasi cha shilingi milioni 160 kimetengwa kwa ajili ya kuendeleza ujenzi wa jengo la ghorofa moja ambalo lina wodi ya wanaume, wanawake na watoto.

(iv) Kwa mwaka wa fedha 2018/2019 kituo kimetengewa asilimia 25 ya fedha za Mfuko wa Pamoja wa Wafadhili (*Health Sector Basket Fund*) ambayo ni sawa na shilingi milioni 357.73 ya mgao wa Manispaa ya Ubungo ambayo ni shilingi bilioni 1.43. Fedha hizi ni kwa ajili ya utawala na ununuzi wa dawa na vifaa tiba.

Mheshimiwa Naibu Spika, kupitia Bunge lako tukufu, napenda kuelekeza Halmashauri ya Ubungo kutenga eneo lisilopungua ekari 25 litakaloweza kuwepo katika eneo moja majengo yote ya msingi ya Hospitali ya Wilaya. Aidha, Serikali itaendelea kupeleka Madaktari Bingwa na kuboresha huduma zaidi katika kituo hiki kadri bajeti itakavyokuwa ikiruhusu.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Joseph Selasini, swali la nyongeza.

**MHE. JOSEPH R. SELASINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Mara nyingi Mawaziri wetu hapa Bungeni wamekuwa wakituambia kwamba ahadi ya Rais ni sheria na lazima itekelezwe. Sasa kupandisha hadhi Kituo cha Afya

cha Palestina kuwa Hospitali ni ahadi na agizo la Mheshimiwa Rais. Sasa ni kwa sababu gani badala ya Serikali kutekeleza ahadi hii, inafanya maboresho?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, Kituo cha Afya cha Tarakea katika Wilaya ya Rombo kinachukua wagonjwa wengi sana kutokana na eneo kubwa na wagonjwa wengine kutoka nchi jirani ya Kenya, lakini hakina *incinerator*, hakina *mortuary*, vilevile kilikuwa hakina uzio lakini Mbunge akajitahidi kwa fedha za Mfuko wa Jimbo kujenga uzio.

Sasa je, Mheshimiwa Waziri yuko tayari kufika Rombo kutembelea kituo kile ili tushauriane naye namna ya kukiboresha kiweze kuhimili idadi kubwa ya wagonjwa ambao wanakwenda kwenye kile kituo?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu kwa maswali hayo.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, kama ambavyo nimejibu katika jibu langu la msingi, Serikali tunakiri juu ya umuhimu wa Kituo cha Afya cha Sinza pale Palestina, lakini ni ukweli usiopingika kwamba ili Kituo cha Afya kiwe Hospitali ya Wilaya kuna suala zima la eneo ambalo katika jibu langu la msingi nimemwambia kwamba tunahitaji ekari 25. Sasa ukienda katika kile Kituo cha Afya cha Palestina, eneo hilo halipo na ndiyo maana katika maboresho ambayo yanaendelea ni pamoja na kutenga shilingi milioni 160 ili kuweza kuwa na hadhi ya kufanana na Kituo cha Afya.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni ukweli usiopingika kwamba tunapata changamoto katika Vituo vya Afya vilivyo Mijini, kitu ambacho kinakosekana ni jina lipi tutumie? Kwa sababu vinakuwa na hadhi zaidi ya Vituo vya Afya, lakini vinakuwa havijafikia kuwa Hospitali za Wilaya. Ndiyo maana nimesema kwamba ni vizuri Manispaa wakatenga eneo kwa ajili ya ujenzi wa Hospitali ya Wilaya. Kwa hiyo, kama Serikali tuko tayari na wala hatupingani na kile ambacho

Mheshimiwa Rais alielekeza kwa wakati ule, lakini changamoto ya ardhi ndiyo inayotusababisha tuseme kwamba ni vizuri likatengwa eneo lingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika swali lake la pili, Mheshimiwa Selasini anataka utayari wangu kwenda kutazama Kituo cha Afya Tarakea. Naomba nimhakikishie, kama ambavyo nimefanya ziara kwenda Kituo cha Afya cha Kiaseri kule, niko tayari kufika hata Tarakea kwa kadri muda unavyokuwa umeruhusu.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, niwasihi kabla sijaanza kuwaita kwa ajili ya maswali ya nyongeza, maswali yawe mafupi. Ukiuliza marefu, unawanyima wenzio fursa ya kuuliza maswali.

Mheshimiwa Flatei Massay, swali la nyongeza.

**MHE. FLATEI G. MASSAY:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, changamoto iliyopo Ubungo inafanana kabisa na changamoto iliyopo Jimbo la Mbulu Vijijini. Tuna kituo kimoja tu cha afya Jimbo zima; je, Serikali ina mpango gani sasa wa kutuongezea angalau kituo kimoja ili katika huduma za afya jimboni, pakawa na hali ya kuwasaidia wananchi?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu kwa swali hilo.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, changamoto iliyopo kwenye Kituo cha Afya katika swali la msingi, ni suala la eneo, lakini kwake yeye eneo siyo tatizo kama ambavyo iko Sinza, Palestina pale.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia naomba kwa dhati kabisa ya moyo wangu nimpongeze Mheshimiwa Flatei

Massay kwa jinsi ambavyo amekuwa akilipigania Jimbo lake, amehakikisha kwamba Halmashauri inajengwa lakini pia ni miongoni mwa maeneo ambayo yanakwenda kujengewa Hospitali za Wilaya. Naomba nimhakikishie kwa dhati hiyo ambayo Serikali imeonesha kuhakikisha kwamba tunajenga Hospitali za Wilaya, ni azma yetu pia kuhakikisha kwamba tunajenga Vituo vya Afya vya kutosha na kwa kadri bajeti itakavyokuwa imeruhusu hakika hatutasahau eneo la kwake. (Makofi)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Qulwi Qambalo, swali la nyongeza.

**MHE. QAMBALO W. QULWI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Katika mwaka wa fedha unaokuja, Serikali imetenga fedha za kujenga Hospitali za Wilaya kwenye maeneo 67, lakini pia ni wazi zipo Wilaya nyingi ambazo bado hazina Hospitali ya Wilaya ikiwemo Wilaya yangu ya Karatu. Ni lini sasa wananchi wa Karatu wategemee kujengewa Hospitali ya Wilaya?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, kama ambavyo nimekuwa nikijibu hapa, kuanza na Hospitali za Wilaya 67 tafsiri yake ni kwamba zikikamilika hizo tutakwenda kujenga nyingine. Ni azma ya Serikali inayoongozwa na CCM kuhakikisha kwamba Wilaya zote ambazo hazina Hospitali za Wilaya baada ya kumaliza hizi 67 tutakwenda hatua nyingine ya kwenda kuzijengea.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Mheshimiwa Mbunge avute subira, bajeti ndiyo imepita, tumwombe Mwenyezi Mungu makusanyo yetu yaende vizuri, tukimaliza 67 tutakwenda hatua ya pili.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Daimu Mpakate, swali la nyongeza.

**MHE. DAIMU I. MPAKATE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante.

Mheshimiwa Rais wa Awamu ya Nne, mwaka 2014 alipotembelea Jimbo la Tunduru Kusini alitembelea katika Kijiji cha Mbesa ambapo kuna Hospitali ya *Mission* pale. Hospitali ile inatoa huduma kubwa kuliko Hospitali ya Wilaya na Mheshimiwa Rais aliahidi kuipandisha daraja hospitali ile kuwa Hospitali Teule. Je, ni lini hospitali ile itapewa hadhi ya kuwa Hospitali Teule ili iweze kuendelea kutoa huduma vizuri?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, samahani, sikusikia vizuri hospitali inaitwaje, naomba arudie nisikie.

**MHE. DAIMU I. MPAKATE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni Hospitali ya *Mission* ya Mbesa.

**NAIBU SPIKA:** Huyu ni Mbunge wa Tunduru, kwa hiyo, itakuwa iko Tunduru hiyo.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, kama ambavyo nimekuwa nikijibu na ambavyo nimejibu leo, ni azma ya Serikali kuhakikisha kwamba maeneo ambayo hakuna Hospitali za Wilaya zinakwenda kujengwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia ni azma ya Serikali kwa kushirikiana na Taasisi za Dini na Mashirika mengine pale ambapo sasa hivi hatuna Hospitali Teule, tunatumia zile ambazo zipo ili zifanye kazi kwa muda tu kama Hospitali Teule. Ni azma ya Serikali kuhakikisha kwamba tunakuwa na hospitali zetu za Serikali na zile za Mashirika ya Dini pale ambapo tutakuwa tumejenga za Serikali wabaki wakiendesha kwao na sisi Serikali tuwe na za kwetu tukifanya kazi kama Serikali. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Tunaendelea. Mheshimiwa Waziri wa Afya, majibu ya nyongeza.

**WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza namshukuru Naibu Waziri kwa majibu mazuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka tu kumshauri Mheshimiwa Mpakate, ili hospitali binafsi au ya Shirika la Dini ifanywe kuwa *DDH* sasa hivi tumeshusha madaraka haya kwenye Halmashauri husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, Halmashauri ndiyo itafanya majadiliano na makubaliano na hospitali ile na tumeelekeza kuwe na mkataba wa muda maalum, kwamba Halmashauri ya Tunduru inaamua kuingia makubaliano na hospitali hii ili iwe Hospitali Teule ya Halmashauri na mkishakubaliana ndiyo mnaleta taarifa hizi TAMISEMI na Wizara ya Afya. Kwa hiyo, tutazitambua rasmi sasa kuwa ni Hospitali Teule ya Halmashauri husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, niseme tunatoka kwenye Hospitali za Wilaya, tunakwenda kwenye Hospitali ya Halmashauri. Kwa hiyo, sasa hivi kila Halmashauri itakuwa na Hospitali badala ya kuwa Hospitali ya Wilaya.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, kama kuna Wilaya zina Halmashauri mbili, zote zinapaswa kuwa na Hospitali ya Halmashauri ambayo ni ngazi ya kwanza ya Hospitali.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Ofisi ya Rais, Muungano na Mazingira, Mheshimiwa Mwantum Dau Haji, Mbunge wa Viti Maalum sasa aulize swali lake.



Na. 448

## **Athari za Mabadiliko ya Tabianchi**

**MHE. MWATUM DAU HAJI** aliuliza:-

Kilimo cha Tanzania hutegemea mvua za msimu ambazo kwa kiasi kikubwa zimeathiriwa na mabadiliko ya tabianchi na hivyo kuathiri shughuli za uzalishaji.

Je, Serikali ina mpango gani wa kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, (MUUNGANO NA MAZINGIRA)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, (Muungano na Mazingira), napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mwatum Dau Haji, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi katika Sekta ya Kilimo, Ofisi ya Makamu wa Rais iliandaa Mpango wa Taifa wa Kuhimili Mabadiliko ya Tabianchi wa mwaka 2007 na Mkakati wa Taifa wa Kukabiliana na Mabadiliko ya Tabianchi wa mwaka 2012 katika sekta mbalimbali ikiwemo na sekta ya kilimo. Mipango hii kwa sekta ya kilimo imejikita katika kuendeleza kilimo cha umwagiliaji ikiwa ni pamoja na kutumia teknolojia zinazopunguza upotevu wa maji ili kuepuka kilimo cha kutegemea mvua.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, mipango hii inaelezea namna ya kubadili vipindi vya upandaji mazao ya misimu ili kuendana na mabadiliko ya misimu ikiwa ni pamoja na kupanda mazao na mbegu zinazohimili ukame, kuboresha mbinu za kudhibiti wadudu waharibifu wa mazao na kuweka mifumo mbadala ya kilimo ili kuongeza uzalishaji. Aidha, Ofisi ya Makamu wa Rais ipo katika mchakato wa kukamilisha kuandaa mpango endelevu wa Kitaifa wa

Kuhimili Mabadiliko ya Tabianchi (*National Adaptation Plans*). Mpango huu utakapokamilika utawezesha nchi kuwa na mipango itakayoweza kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi katika sekta muhimu ikiwemo sekta ya kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ofisi ya Makamu wa Rais imekuwa inashirikiana na Wizara ya Kilimo pamoja na Wizara ya Maji na Umwagiliaji katika kuandaa mipango ya kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi katika Sekta ya Kilimo. Mipango iliyoandaliwa ni pamoja na:-

Moja, Mpango Mahususi wa Sekta ya Kilimo katika Kukabiliana na Mabadiliko ya Tabianchi (*Tanzania Agriculture Climate Resilience Plan*); pili, Mpango wa Kitaifa wa Kilimo Rafiki cha Mabadiliko ya Tabianchi (*National Climate Smart Agriculture*) na programu mbalimbali za uendelezaji wa kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika utekelezaji wa mipango na programu hizi katika sekta ya kilimo, suala la kuhimili mabadiliko ya tabianchi katika kilimo imezingatiwa hasa kwa kusisitiza uwekezaji katika miundombinu ya kilimo (suala la kuongeza kilimo cha umwagiliaji).

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mwantum Dau Haji swali la nyongeza.

**MHE. MWATUM DAU HAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Kwanza namshukuru Mheshimiwa Waziri kwa majibu yake mazuri aliyoyatoa yenye kila aina ya vinjonjo. Napenda kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa programu hizi katika sekta ya kilimo linahusiana na suala la kuhimili mabadiliko ya tabianchi; je, Serikali ina mkakati gani kutoa elimu kwa wakulima ili waende sambamba na mabadiliko ya tabianchi? (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira) majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, (MUUNGANO NA MAZINGIRA):** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa nampongeza Mheshimiwa Mwatum ambaye amekuwa akifuatilia sana masuala ya mazingira na hasa mambo haya ya mabadiliko ya tabianchi. Namhakikishia kwamba pamoja na mipango hii ambayo Serikali tumekuwa tukiifanya, hata kule Unguja na Pemba tunashirikiana na Taasisi za Kimataifa *USAID* pamoja na *FAO* katika miradi ya kilimo ya kuhimili mabadiliko ya tabianchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa kutoa elimu, nimhakikishie Mheshimiwa Mwantum tayari mpaka sasa Serikali ilishatoa mwongozo pamoja na mafunzo kwa watu wapatao 192 wakiwemo Maafisa Kilimo, Maafisa Uvuvi, Maafisa Mifugo pamoja na Maafisa Mipango kutoka kwenye Halmashauri za Wilaya na kuwaelekeza kwamba katika mipango wanayoipanga Wilayani pamoja na bajeti waweze kushirikisha mipango hiyo ya kilimo himilivu cha mabadiliko ya tabianchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, elimu hii tayari tulishaipeleka kwa wananchi na bado tunaendelea katika mpango huu tuliosema endelevu wa kuhimili mabadiliko ya tabianchi, ni *element* ambayo pia inahusishwa. Pamoja na kwamba Mheshimiwa Rais alizindua juzi hapa *ASDP II*, vilevile kuna *element* ya kutoa mafunzo ya kilimo himilivu kutokana na mabadiliko ya tabianchi.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, nawaona mmesimama, lakini niwakumbushe kuuliza maswali yenye uhusiano na swali la msingi. Mnaipa Serikali wakati mgumu mnapouliza maswali yasiyohusiana kabisa na ninyi mnaona na mnataka majibu yaliyokamilika. Mheshimiwa Alex Gashaza swali la yongeza.

**MHE. ALEX R. GASHAZA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi niulize swali.

Mheshimiwa Naibu Spika, mapema mwaka 2017 niliwasilisha andiko la mradi ujulikanao kama *Commitment*

*Bush Fire Management and Livelihood Improvement* kwa lengo la kudhibiti uchomaji moto ovyo. Ni lini Wizara yenye dhamana itaweza kuwezesha mradi huu kwa kutoa fedha ili tuweze kutekeleza kikamilifu kwa kuanzisha zao ambalo ni rafiki na mazingira lakini pia na ufugaji wa nyuki? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira) majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, (MUUNGANO NA MAZINGIRA):** Mheshimiwa Naibu Spika, mapema katika Mkutano uliopita Mheshimiwa Gashaza aliuliza swali la nyongeza kuhusiana na mradi wake huu.

Napenda nimhakikishie kwamba sasa hivi Ofisi ya Makamu wa Rais inaandaa maandiko mbalimbali kwa ajili ya kuomba fedha kwa ajili ya utekelezaji wa miradi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia tunahamasisha Halmashauri za Wilaya waweze kuandika maandiko ambayo watayaleta Ofisi ya Makamu wa Rais ili tuweze kuwatafutia fedha katika kutekeleza miradi hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimhakikishie Mheshimiwa Gashaza, andiko lake tumelipitia ni muhimu sana. Pia aliweza kuwahusisha wananchi wa Jimboni kwake kupitia michezo wakiwa na kauli mbiu ya kwamba mazingira ni uchumi ili waweze kucheza ligi ile na kauli mbiu hiyo waweze kuhakikisha kwamba wanajihusisha na ufugaji wa nyuki pamoja na kilimo ili wasiendelee kuchoma misitu ambayo inaendeleza uharibu wa mazingira.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Gashaza kwamba hata hiyo ligi yake, baada ya kupata fedha mimi mwenyewe nitaenda kumsaidia kuizindua ili iwe kichocheo kwa nchi nzima ili wananchi wengine nao wafanye hivyo. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Yussuf swali la nyongeza.

**MHE. YUSSUF SALIM HUSSEIN:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi. Nasikitika kwamba Mheshimiwa Naibu Waziri hajajibu hili swali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuathirika kwa kilimo ni matokeo ya athari za tabianchi. Tuambie Serikali ina mikakati gani ya kukabiliana na athari hizi? Maziwa yanakauka, mito inakauka, misitu inapotea. Mna mkakati gani mliouchukua au ndiyo mko kwenye mipango tu? Ndiyo jibu tunalolitaka kutoka kwako. Nakushukuru.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Makamu wa Rais, (Muungano na Mazingira), majibu.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, (MUUNGANO NA MAZINGIRA):** Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyojibu kwenye swali la msingi ambalo Mheshimiwa Mwantum Dau Haji alitaka kujua Serikali tuna mipango na mikakati gani; nimeeleza kwamba mkakati wa kwanza tulionao tuliandaa mwaka 2007 ambao unahusu uhimilivu katika mabadiliko ya tabianchi kwenye suala la kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nimejibu hapa kwamba mwaka 2012 tuliandaa mpango mwingine wa mabadiliko ya tabianchi tofauti na ule wa mwanzo. Vilevile nimejibu hapa kwamba mpaka sasa Serikali kupitia Ofisi ya Makamu wa Rais na kupitia wataalam tunaandaa na tunakaribia kumaliza kupata sasa mpango mkakati endelevu wa kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi kwenye suala la kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, siyo kwamba mikakati haipo, nimeeleza hapa. Pia nimeeleza hapa kwamba hata juzi Mheshimiwa Rais amezindua *ASDP* Awamu ya Pili ambamo ndani mwake pia kuna mikakati mingi sana imezungumziwa. Pia mikakati na mwongozo niliousema ambao tumepeleka kwenye Halmashauri ambapo Maafisa Mipango wanatakiwa kuweka kwenye bajeti zao, tumeeleza kuhusu utafiti wa mbegu ambayo inahimili

kwenye ukame pamoja na kilimo cha umwagiliaji na umwagiliaji wa matone.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, mikakati hii ipo, Mheshimiwa Yussuf mtani wangu wa kisiasa, naomba uelewe Serikali ya Mheshimiwa Dkt. Magufuli ni Serikali makini, ni Serikali ambayo inaongoza kwa kuwa na mikakati, tena mikakati ambayo inatekelezeka. Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Sware Semesi, swali fupi.

**MHE. DKT. IMMACULATE S. SEMESI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa nafasi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ofisi ya Makamu wa Rais imekuwa ikipokea fedha mbalimbali kutoka kwa wafadhili ili kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi kila mwaka. Miaka miwili iliyopita walikabidhiwa takribani shilingi bilioni 224 kwa ajili ya shughuli hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Naibu Waziri anaongelea kuhusu mikakati; je, kuna utekelezeji wowote wa mikakati hii ya kuhusisha mabadiliko ya tabianchi na kuboresha kilimo chetu kwa kutumia hizi fedha za wafadhili ambazo zinagusa hususan mabadiliko ya tabianchi? Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Makamu wa Rais, (Muungano na Mazingira) majibu.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, (MUUNGANO NA MAZINGIRA):** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, namshukuru Mheshimiwa Dkt. Sware ni mwanamazingira na ni kweli anafahamu kabisa kwamba Ofisi ya Makamu wa Rais tumekuwa tukipata fedha ambazo zinasaidia miradi mbalimbali ya kuhimili mabadiliko ya tabianchi. Amesema sasa mbali na mikakati, fedha hizi namna gani tunazi-*link*.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nimhakikishie kwamba mojawapo ya miradi ambayo tumeihusianisha na hiki kilimo kutokana na athari za mabadiliko ya tabianchi, ukienda kule Rufiji tayari katika Halmashauri ya Wilaya ya Rufiji tulikuwa tunatekeleza mradi ukiwa ni pamoja na kupanda mikoko na kuwawezesha wananchi wahimili mabadiliko ya tabianchi kwa kilimo cha mboga pamoja na matunda.

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na hilo, ukienda kule Pemba Kisiwa Panza mbali na kujenga ukuta, vilevile tulikuwa tunawasaidia wananchi waweze kuhimili mabadiliko ya tabianchi kwa kilimo cha mboga na matunda.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hayo sasa hivi tuna Mikoa kama Tabora, Singida, Kagera, Morogoro, Tanga ambako tayari tunatekeleza miradi mbalimbali ya kutumia fedha hizi ikiwa ni pamoja na kuwajengea uwezo wakulima wa namna wanavyoweza kuhimili mabadiliko ya tabianchi, ikiwa ni pamoja na kuhakikisha kwamba wanatumia zile fedha katika kilimo cha mboga pamoja na matunda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hiyo ni pamoja pia na Bonde la Kihansi kule Kilombero, vilevile tumeweza kutoa fedha ili wananchi wahimili athari za mabadiliko ya tabianchi kwa kilimo katika lile mbonde.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Sware kwamba siyo mikakati tu ambayo Serikali inaishia, ni pamoja na fedha hizi. Tumetoa fedha nyingine shilingi milioni 200 sasa ambazo zinapeleka maji kule Shinyanga na yale maji yatatumika pia katika kusaidia umwagiliaji kwenye kilimo. Hiyo ni katika kuhimili mabadiliko ya tabianchi. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge tunaendelea na Wizara ya Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Dkt. Jasmine Tisekwa Bunga, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 449

### **Kujenga Hoteli Kubwa za Kitalii - Mikumi**

**MHE. DKT. JASMINE T. BUNGA** aliuliza:-

Mkoa wa Morogoro una vivutio vingi sana vya utalii ambavyo vikitumika vizuri vinaweza kuchangia pato la Taifa na wananchi kwa ujumla; moja kati ya vivutio hivyo ni pamoja na Mbunga za Hifadhi ya Wanyama Mikumi ambayo inaongeza mapato mengi, lakini mbuga hizo hazina hoteli nzuri za kitalii zenye kukidhi viwango vya kimataifa, kutokana na kuungua kwa Hoteli ya Kitalii ya Mikumi.

Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga hoteli kubwa za kitalii ndani ya Mbunga ya Mikumi ili kuvutia watalii wengi?

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maliasili na Utalii naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Jasmine Tisekwa Bunga, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kabisa kuwa Mkoa wa Morogoro una vivutio vingi vya utalii ikiwemo Hifadhi ya Mikumi. Baada ya kuungua kwa *lodge* ya Mikumi, Serikali kupitia *TANAPA* imeendelea na juhudi mbalimbali za kuhamasisha uwekezaji katika hifadhi hiyo, ambao fursa za uwekezaji hususan huduma za malazi zimekuwa zikitangazwa. Aidha, mwekezaji wa kuifufua *lodge* ya Mikumi alishapatikana na kazi ya ukarabati inaendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, watalii wanaotembelea Hifadhi ya Mikumi kwa sasa wanatumia kambi tatu za mahema (*tented camps*) zilizoko ndani ya hifadhi, *lodge* na hoteli kumi zilizopo Mikumi Mjini. Wizara kupitia *TANAPA* imetenga maeneo saba kwa ajili ya uwekezaji wa hoteli na *lodge* ndani ya Hifadhi ya Taifa ya Mikumi zenye hadhi na



viwango vya kimataifa ili kuleta watalii wengi na kuongeza mapato.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuchochea maendeleo ya sekta ya utalii katika Ukanda wa Kusini kwa ujumla, Serikali ilizindua rasmi mradi wa kuendeleza utalii Ukanda wa Kusini wa Tanzania ujulikanao kama *REGROW* tarehe 12 Februari, 2018 Mjini Iringa. Lengo la mradi huu ni kuwezesha maendeleo ya utalii kwa kuboresha miundombinu, kuhifadhi maliasili na mazingira katika hifadhi ya Ukanda wa Kusini ikiwemo Hifadhi ya Taifa ya Mikumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo, napenda kutumia fursa hii kumwomba Mheshimiwa Mbunge, uongozi pamoja na wakazi wa Mikumi kwa ujumla kutenga maeneo ya uwekezaji wa huduma za malazi na utalii ili kunufaika na biashara ya utalii nje ya Hifadhi ya Taifa ya Mikumi. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Jasmine Tisekwa Bunga, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. JASMINE T. BUNGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya swali la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri bado kidogo ayajaniridhisha kwa sababu mimi nilitembelea Mikumi pale 2016 na majibu niliyopewa ni haya haya kwamba mwekezaji amepatikana na ukarabati unaendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa namwomba Mheshimiwa Naibu Waziri anihakikishie hapa huu ukarabati utamalizika lini ili tuweze kupata mapato ya uhakikika? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu la pili ni kwamba mbuga hii ya Mikumi ipo katikati ya barabara ambayo inaenda mikoani na nje ya Tanzania. Kulikuwa na mpango wa kuanzisha *road toll* ili kuweza kupata mapato zaidi katika

mbuga hii ambayo inakumbana na changamoto nyingi, miundombinu na hata magari ya kuzuia ujangili.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka kujua, ni lini Serikali itaanzisha ushuru huu kwa sababu mchakato ulishaanza, sasa kuna kigugumizi gani? Hii itasaidia mbuga hii iweze kupata mapato na kukabiliana na changamoto ili iweze kuboresha na kuongeza mapato zaidi? Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Maliasili na Utalii, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naomba nichukue nafasi hii kumpongeza kwa jinsi ambavyo amekuwa akifuatilia na ni kweli kabisa kwamba mwaka 2016 alifika pale kuangalia ni namna gani hoteli zinaweza kuongezeka katika lile eneo ili kukabiliana na hii changamoto ya uhaba wa vyumba vya watalii kulala pale Mikumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimhakikishie kwamba ni kweli kabisa kwamba yule mwekezaji alipatikana siku nyingi toka mwaka 2016, lakini baada ya kupatikana, kwa mujibu wa taratibu za uwekezaji, lazima kwanza *EIA* ifanyike ili aweze kuendelea na huo mradi. Huo mradi baada ya kufanya hiyo tathimini ya mazingira, imekamilika mwezi Novemba, 2017. Baada ya kukamilika, mwezi Februari, 2018 ndipo mwekezaji amekabidhiwa rasmi lile eneo.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kukabidhiwa lile eneo, sasa hivi ametoa mpango kazi, na mimi mwenyewe nilienda pale nikaona, sasa hoteli yenyewe inategemea kukamilika mwezi Novemba mwaka ujao yaani mwaka 2019. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu suala la kuweka *road toll* kule Mikumi, ni kweli hili suala limekuwepo na tumekuwa tukiliangalia ndani ya Serikali kuona kama kweli linaweza likatusaidia na kama linaweza likafanya kazi. Bado tuko kwenye hatua za majadiliano na kuona namna bora

ya kuweza kulitekeleza hilo ili kusudi tusilete usumbufu kwa wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, wazo la Mheshimiwa Mbunge ni zuri na ninaomba niseme kwamba Serikali bado inaendelea kulifanyia kazi.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mbarouk, swali la nyongeza.

**MHE. MBAROUK SALIM ALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru.

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu nyingi ambazo zina vivutio vya utalii utakuta miundombinu yake ni mibovu sana. Hii ndiyo sababu kubwa ambayo inasababisha wawekezaji warudi nyuma na washindwe kuwekeza katika maeneo ambayo yana vivutio na hivyo kushusha utalii.

Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha kwamba wanaboresha miundombinu katika maeneo hayo ya utalii? Nashukuru. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kabisa kumekuwa na maeneo ya namna hiyo na bado kumekuwa na changamoto ya uwekezaji. Kazi kubwa tunayoifanya kama Serikali ni kuhakikisha kwamba tunaboresha kwanza mazingira ya uwekezaji na kuwahamasisha wawekezaji ili kusudi waweze kuwekeza katika maeneo yote hayo na yaweze kuchangia katika shughuli mbalimbali za utalii.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niseme tu kwamba tutakaa na Mheshimiwa Mbunge ili tuone namna gani tunaweza tukafanya hiyo kazi ili kusudi wananchi wa eneo lile waweze kufaidika na matunda ya hiyo kazi.

**NAIBU SIPKA:** Mheshimiwa Janet Mbene, swali la nyongeza.

**MHE. JANET Z. MBENE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, sekta ya utalii ni sekta ambayo ina fursa nyingi sana na kubwa za kulisaidia Taifa kimapato. Suala la Mikumi kama ambavyo limejibiwa sasa hivi, tunapoteza fursa kubwa sana. Mikumi ilikuwa ni kivutio katika vivutio vya mwanzo kabisa vya utalii nchi hii. Ilikuwa inatoa fursa kubwa sana kwa utalii wa ndani hasa kwa vijana, wanafunzi na taasisi mbalimbali wanaotaka kwenda kuangalia mambo ya utalii. Jinsi ilivyo sasa hivi imekwama kwa muda mrefu na hii sawa na sehemu nyingine nyingi tu.

Je, Serikali sasa hivi iko tayari kuja na mkakati mahususi unaohakikisha kuwa sehemu zote za kitalii zinaendelezwa kwa kutumia sekta binafsi? Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kabisa kwamba Mikumi ilikuwa ni moja ya hifadhi ambayo ilikuwa inatoa mchango mkubwa sana katika pato la Taifa, lakini kumekuwa na changamoto ya hivi karibuni kwamba mchango ule kidogo umeshuka sana kutokana na mambo mbalimbali. Ndiyo maana kwa kutambua hilo, Serikali tumekuwa na mradi mkubwa wa kuboresha utalii Kusini. Katika mradi huo, moja ya maeneo ambayo yamepewa uzito ni pamoja na hifadhi ya Mikumi, kwa sababu ule mradi wa kukuza utalii wa Kusini, tunahudumia Selous upande wa Kaskazini, Udzungwa, Mikumi na Ruaha.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, katika huo mradi tunaboresha miundombinu yote, tutatangaza ipasavyo kuhakikisha kwamba tunawavutia watalii mbalimbali wa ndani na nje ya nchi ili waweze kuingiza mapato na Serikali

iveze kupata mapato ya kutosha na kuweza kuendeleza nchi yetu.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Felister Bura, swali la nyongeza.

**MHE. FELISTER A. BURA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza Swali la nyongeza. Kama ilivyo Morogoro kwamba kuna vivutio kwa watalii ndivyo ilivyo kwa Mkoa wa Dodoma ambako Wilayani Kondoa kuna michoro ambayo haipo Tanzania na michoro ile iko katika mapango ya Kolo na Pahi, lakini vivutio vile havijawahi kutangazwa na Serikali.

Je, Serikali ina mkakati gani? Pamoja na Wabunge wa Kondoa kuhangaika kuleta watalii, lakini bado haitoshelezi kama Serikali haitatia mkazo kutangaza vile vivutio.

Je ni lini sasa au Serikali ina mkakati gani kutangaza michoro ile ya mapango ya Kolo, Pahi na maeneo mengine katika Wilaya ya Kondoa?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maliasili na Utalii, naomba nichukue nafasi hii kwanza nimpongeze sana Mheshimiwa Felister Bura na Wabunge wote wa Mkoa wa Dodoma kwa jinis ambavyo wamekuwa wakilifanyia kazi hili suala. Hivi sasa tunajua kabisa kwamba Dadoma ndiyo Makao Makuu ya nchi na kweli lazima tuziimarisha hizi hifadhi zetu na maeneo maengine ya Utalii ili kuweza kuvutia watu mbalimbali kuja kuwekeza katika Mkoa huu wa Dodoma.

Mheshimiwa Naibu Spika, kitu ambacho tunategemea kukifanya katika kutangaza yale maeneo ya michoro ya Miambani kule Kondoa; yaani Kolo na pale Pahi; jitihada ambazo tunaweka kuanzia tarehe 1 Julai, 2018 tunategemea

kuanzisha *studio* ya kutangaza utalii yaani kutangaza vivutio vyote nchi nzima. Hiyo ni pamoja na hilo eneo, tatalitangaza vizuri sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, tunategemea kuanzisha *channel* maalum kupitia *TBC* ambayo itakuwa inahusiana na masuala ya utalii. Kwa kutumia hilo basi, tunaamini kwamba basi matangazo, wananchi wengi wa ndani na wa nje wataweza kupata fursa ya kuweza kujua vivutio vyote tulivyonavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, la tatu, tunategemea kutumia viongozi mbalimbali mashuhuri pamoja na mambo mengine mengi kutangaza ndani ya nchi na nje ya nchi kwa kutumia mitandao ya *facebook*, *twitter* na mambo mengineyo ili kusudi vivutio vyote vieleweke kwa watazania lakini kwa watu wote walioko nchi za nje waweze kujua Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nitumie nafasi hii niseme kwamba sasa hivi Tanzania tumepata taarifa kwamba sasa imekuwa ni nchi inayoongoza kwa safari Afrika kupitia Serengeti. Kwa kweli huu ni ufahari mkubwa na Dodoma nayo itafaidika sana na haya mambo ambayo tunakwenda kuyafanya.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Ally Keissy, swali la nyongeza.

**MHE. ALLY K. MOHAMED:** Mheshimiwa naibu Spika, ahsante sana. Kuhusu Hoteli ya Kitalii ya Mikumi: Je, Mheshimiwa Naibu Waziri anafahamu kwamba mwekezaji wa kwanza alifanya hujuma makusudi baada ya kuchukua shilingi bilioni nne na mpaka leo akaichoma hoteli ile?

Je, Serikali imechukua hatua gani kwa yule mwekezaji wa kwanza? (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli kama Serikali hatuna taarifa kama kweli ile ilichomwa kama hujuma, lakini tunachojua ni kwamba ilipata janga la moto mwaka 2009 na ikaungua yote. Yule aliyekuwa amekabidhiwa baada ya hapo, alishindwa kuendeleza. Baada ya kuona ameshindwa kuendeleza, ndiyo maana Serikali tukaamua tena kuchukua hatua kuhakikisha kwamba tunamtafuta mwekezaji mwingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwekezaji huyu sasa liyepatikana amekuja na michoro mizuri sana na *design* nzuri sana ambazo ninazo hata baaadaye Mheshimiwa Keissy naweza nikamwonyesha hapa jinsi ilivyo ambapo tunategemea itakapofika mwaka 2019 hoteli yenyewe itakuwaje? Kwa hilo tunalo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hilo la kusema kwamba alifanya hujuma, hizo taarifa hatunazo kama Serikali.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na swali la Mheshimiwa Ester Alexander Mahawe, Mbunge wa Viti Maalum, swali lake litaulizwa kwa niaba na Mheshimiwa Innocent Bashungwa.

Na. 450

**Kuboresha Miundombinu katika  
Hifadhi za Taifa**

**MHE. INNOCENT L. BASHUNGWA (K.n.y. MHE. ESTER A. MAHAWE)** aliuliza:-

Sekta ya utalii inachangia pato kubwa la fedha za kigeni katika nchi yetu.

Je, ni lini Serikali itatengeneza barabara ya Serengeti ambayo ni mbovu kiasi cha kufanya watalii kukataa kupita huko?

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII alijibu:-**

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maliasili na Utalii, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Ester Alexander Mahawe, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa naibu Spika, Hifadhi ya Taifa ya Kilimanjaro na Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro ndiyo zinachangia zaidi katika mapato ya fedha za kigeni zitokanazo na shunguli za utalii hapa nchini. Hifadhi ya Taifa ya Serengeti ina ukubwa wa kilometa za mraba 14,763 na barabara zenye urefu wa kilometa 3,155. Barabara hizo ni pamoja na barabara kuu zinazounganisha Hifadhi na Mikoa ya Arusha, Mara na Simiyu. Barabara nyingine ni zile za mizunguko ya utalii na nyingine ni za utawala na doria. Barabara zote hizo ni za kiwango cha changarawe.

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara zenye matumizi makubwa ni zile kuanzia mpaka unaotenganisha Hifadhi ya Taifa ya Serengeti na Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro hadi Kituo cha Seronera yenye urefu wa kilometa 60 na kilometa 30 kutoka Seronera hadi lango na Ikoma. Barabara hizi wakati wa msimu wa watalii wengi zinatumiwa na magari zaidi ya 300 kwa siku. Kutokana na matumizi makubwa kiasi hicho, barabara hiyo yenye kiwango cha changarawe uchakavu wake huongezeka kwa kasi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuanzia mwezi Agosti, 2016 hifadhi inaendelea kuelekeza nguvu za ziada kuhudumia barabara hizi wakati wote wa msimu wa watalii.

Mheshimiwa Naibu Spika, juhudi zinazoendelea zinahusisha kufanya matengenezo ya barabara hizo kwa kutumia nyenzo mbalimbali ikiwemo mitambo miwili ya barabara yaani *motor graders* pamoja na malori. Ili kupata ufumbuzi wa muda mrefu kukabiliana na changamoto hiyo ya ubovu wa barabara, Shirika la Hifadhi za Taifa linaendelea kutafuta teknolojia mbadala ili kuwa na barabara zitakazodumu bila kuathiri ikolojia ya wanyamapori.



**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Innocent Bashungwa, swali la nyongeza.

**MHE. INNOCENT L. BASHUNGWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri nina maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, changamoto za miundombinu katika hifadhi ya Serengeti zinafanana na changamoto za Hifadhi mpya ya Kimisi na Burigi.

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuweka miundombinu katika hifadhi mpya ya Kimisi na Burigi ili hifadhi hii iweze kuchangia mapato katika Halmashauri zetu za Wilaya zilizopo katika Mkoa wa Kagera pamoja na kuchangia pato la Taifa?

Swali la pili, Mheshimiwa Waziri yupo tayari kuambatana na mimi kwenda kwenye Kata za Bweranyange, Rugu, Nyakasimbi, Nyakabanga na Nyakakika ili kutatua migogoro ya mipaka kati ya vijiji kwenye Kata hizi na Hifadhi? Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nichukue nafasi hii kuwapongeza sana Wabunge wa Mkoa wa Kagera kwa jinsi ambavyo wameshirikiana na Serikali kuhakikisha kwamba maeneo yale yanapandishwa hadhi na sasa Burigi na Kimisi yatakuwa ni mojawapo ya Hifadhi za Taifa. Kwa hiyo, itakuwa ni hadhi ya juu kabisa ya uhifadhi katika nchi yetu. Kwa kweli hongereni sana.

Mheshimiwa Spika, sasa baada ya kupandisha hadhi maeneo hayo, hatua inayofuata sasa ni kuhakikisha kwamba miundombinu ya maeneo yote yale inaimarishwa, barabara zipitike wakati wote ili kusudi watalii waweze kutembelea katika yale maeneo na Serikali iweze kupata fedha nyingi zinazotokana na mapato ya utalii. Kwa hiyo, hilo litafanyika.

Swali la pili, kuhusu kuambatana naye kwenda katika maeneo hayo, naomba nimhakikishie tu kwamba mara baada ya Mkutano huu wa Bunge tutaambatana pamoja, kwa sababu tunataka kwenda kuangalia sasa baada ya kupandisha hadhi mapori yetu yote yale matano, tuone je, nini kinatakiwa kufanyika? Tufanyeje kuhakikisha kwamba utalii sasa unakua katika ile Kanda ya Magharibi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli hilo lote, tutalifanya vizuri kabisa na ninaomba tushirikiane ili tuweze kufanyakazi vizuri zaidi.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Abdallah Bulembo, swali la nyongeza.

**MHE. ABDALLAH M. BULEMBO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana.

Kutokana na swali la msingi la ubovu wa barabara ya Serengeti, Wizara ya Maliasili inaniambiaje; kwa sababu barabara zimekuwa mbovu, Hoteli ya Seronera, Lobo, Ngorongoro na *Lake Manyara* zilikuwa ni hoteli katika nchi hii katika Hifadhi ya Serengeti? Leo hii watalii wakienda, wanabebewa maji kwenye ndoo. Wizara inayajua hayo? Inazirudisha lini hoteli hizi Serikalini? (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kabisa kwamba tulikuwa na hoteli ambazo zilikuwa zinamilikiwa na Serikali katika miaka ya nyuma na hoteli hizi nyingi zilibinafsishwa. Kati ya hoteli 17 ambazo zilikuwa zimebinafsishwa ilionekana karibu hoteli 11 zilikuwa hazifanyi vizuri ikiwemo hizi hoteli chache ambazo Mheshimiwa Mbunge amezitaja.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali tumeliona hilo, tumeanza kufuatilia kupitia mikataba ile ambayo walipewa ili kuhakikisha kwamba kama tumeona kwamba

hawakufanya yale waliyostahili kuyafanya na uwekezaji waliotakiwa kuufanya, Serikali iweze kuzichukua hizo hoteli na kuwapa wawekezaji wengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba baadhi ya hoteli sasa hivi zimechukua hatua, zinaboresha huduma zao. Hili analolisema la maji, kwa kweli sasa litaendelea kupungua hasa baada ya kuanza kutekeleza miradi mbalimbali ya kuhakikisha maji yanakuwepo katika maeneo hayo. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Aida Khenani, swali la nyongeza.

**MHE. AIDA J. KHENANI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Katika Mkoa wetu wa Rukwa tumejaaliwa kuwa na maporomoko ya Kalambo ambayo kama Mkoa sisi tumejipanga.

Sasa napenda kujua katika Wizara ya Maliasili na Utalii mmejipangaje katika kutengeneza mazingira rafiki ili kuweza kuwavutia watalii?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kabisa kwamba katika Mkoa wa Rukwa tunalo eneo lile la maporomoko ya Kalambo ambayo ni maporomoko ya aina yake ambayo tena ni urithi wa dunia. Kwa kweli lile eneo ni zuri sana. Baada ya kuona hivyo, mimi mwenyewe nimefika pale kuangalia mazingira yalivyo, tumechukua hatua ya kuanza kujenga ngazi kubwa ambayo inatoka kule juu kushuka kule chini ambayo ni mita karibu 230. Tunatarajia lile daraja litasaidia sana katika kuboresha na kuvutia watalii kuweza kutembelea yale maporomoko.

Mheshimiwa Naibu Spika, hatua ya pili, tumewaagiza Wakala wa Misitu Tanzania *(TFS)* kuhakikisha kwamba wanawekeza katika lile eneo; wanaweka hoteli ambayo

itakuwa ndiyo kivutio kizuri cha kuwavutia watalii katika lile eneo kusudi waweze kutumia muda mrefu wa kukaa katika lile eneo. Ni tofauti na sasa hivi ambapo unakuta kwamba wenzetu wa Zambia wameweka hoteli upande wao, lakini upande wetu huduma hizi zimekuwa hazipo. Hivyo tumekuwa tukikosa watalii. Nina imani baada ya kuchukua hizi hatua, sasa watalii wataongezeka sana kwa upande wa Tanzania kwa sababu ndiyo sehemu pakee unayoweza ukaiona Kalambo vizuri kuliko maeneo mengine.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Richard Mbogo, swali la nyongeza.

**MHE. RICHARD P. MBOGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa nafasi. Changamoto zilizopo maeneo ya Serengeti na kwingine, zinafanana kabisa na Mbuga yetu ya Katavi ambayo inakosa watalii kutokana na miundombinu mibovu.

Je, Serikali ina mpango gani wa kuboresha miundombinu ndani ya Mbuga ya Katavi ili kuvutia watalii?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kabisa kwamba tunayo hifadhi kubwa ya Katavi ambayo ina wanyama wa kila aina.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi sasa Setikali imechukua hatua mbalimbali za kuhakikisha kwamba kwanza tunaboresha miundombinu iliyopo ndani ya ile hifadhi ili tuweze kuwavutia watalii wengi kutoka maeneo mengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, hatua nyingine ni kwa sababu ule uwanja wa Ndege wa Katavi umekuwa mzuri kabisa na tunaamini katika hizi jitihada ambazo Serikali imechukua za kuongeza ndege, basi safari za ndege zikianza kutumia uwanja ule wa Katavi basi ina maana watalii wataongezeka sana katika lile eneo na hivyo miundombinu

ikiwa inapitika, watalii wengi sana wataweza kuvutiwa na kutembelea katika ile mbuga ya Katavi.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na swali la Mheshimiwa Marwa Ryoba Chacha, Mbunge wa Serengeti.

Na. 451

### **Ukatili Wanaofanyiwa Wananchi Wanaouzunguka Mbuga ya Serengeti**

**MHE. MARWA R. CHACHA** aliuliza:-

Kumekuwepo na tabia ya askari wa *SENAPA* kuwakamata wananchi ndani ya hifadhi na wakati mwingine wasipouawa huwapeleka mbali na Mahakama za Wilaya ya Serengeti.

(a) Je, ni lini vitendo vya mauaji ya watu wanaozunguka Hifadhi ya Serengeti vitakoma?

(b) Je, ni lini askari wa *SENAPA* wataacha kuwapeleka watuhumiwa waliokamatwa ndani ya hifadhi nje ya Mahakama za Wilaya?

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maliasili na Utalii, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Marwa Ryoba Chacha, Mbunge wa Serengeti, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Askari wa Hifadhi ya Taifa ya Serengeti wanafanya kazi kwa mujibu wa sheria, kanuni, taratibu na miongozo mbalimbali iliyopo. Ni kweli kwamba baadhi ya wananchi wamekuwa wakikamatwa na kufanya shughuli au kuingia kwenye hifadhi bila ya kufuata taratibu zilizopo. Wengi wamekuwa wakijihusisha na ujangili ndani ya hifadhi. Kwa msingi huo, Askari wa Hifadhi huwakamata watuhumiwa wote na kuwafikisha katika Jeshi la Polisi na

hatimaye Mahakamani kwa hatua zaidi. Jumla ya kesi 437 zimefunguliwa na zipo katika hatua mbalimbali za usikilizaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, Hifadhi ya Taifa ya Serengeti imepakana na Wilaya nane tofauti. Mtuhumiwa anapokamatwa ndani ya hifadhi, anapelekwa katika Kituo cha Polisi kilicho jirani kwa hatua zaidi. Baadhi ya watuhumiwa wamekuwa na tabia ya kufanya uhalifu kwa kufuata mienendo ya wanyamapori wahamao. Kwa mfano, kati ya mwezi Mei na Juni ya kila mwaka, wanyama wengi wanahamia maeneo ya Kusini na Magharibi mwa Hifadhi ambapo kiutawala yako Wilaya ya Bariadi na Bunda.

Hivyo baadhi ya watuhumiwa kutoka Wilaya ya Serengeti huenda katika Wilaya nyingine kufanya ujangili wa wanyamapori ambapo kwa kipindi hicho hawapatikani kirahisi katika aneo la Wilaya zao. Kutokana na hali hiyo, watuhumiwa wamekuwa wakikamatwa na kushitakiwa katika Mahakama za eneo au Wilaya waliyokamatwa wakifanya uhalifu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni vyema wananchi wakazingatia taratibu zote za Hifadhi na niwaase wananchi hao kuachana na ujangili ili kuepuka adhabu hizo na kuwataka washirikiane na Serikali kulinda hifadhi za Taifa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Marwa Ryoba Chacha, swali la nyongeza.

**MHE. MARWA R. CHACHA:** Mheshimiwa Waziri, wananchi wa vijiji vya Merenga, Machochwe, Nyamakendo, Mbalibali, Tamkeri, Bisarara, Mbilikili, Bonchugu, Miseke na Pakinyigoti wamenituma nimwombe Mheshimiwa Rais Dkt. Magufuli aende akawasikilize matatizo yao, lakini Mheshimiwa Rais, Dkt. Magufuli wa Wizara ya Maliasili na Utalii ni Mheshimiwa Waziri.

Je, uko tayari baada ya Bunge hili kuambatana na mimi kwenda kusikiliza matatizo yao? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili. Wananchi wa vijiji vilivyopo kando kando ya Hifadhi ya Serengeti, mapori ya akiba ya Ikorongo na Gurumeti pamoja na Ikoo na WMA kazi yao kubwa ilikuwa ni uwindaji, ufugaji na kilimo. Uwindaji sasa hivi hawawindi, maana wakienda kuwinda hawarudi; mifugo yao imetafishwa; mazao yao ya kilimo tembo wanakula; ninyi kama Wizara, nini mbadala mnaowasaidia wananchi wa maeneo haya ili waweze kujikimu kiuchumi? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, majibu kwa maswali hayo.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kabisa kwamba kwanza naomba nimhakikishie tu kwamba niko tayari wakati wowote pale ambapo muda utaruhusu tutapanga, lazima twende tukatembelee katika yale maeneo. Hiyo inatokana na kwamba sasa hivi tuna mpango kabambe wa kuhakikisha kwamba maeneo yote yanayopakana na Hifadhi za Taifa, lazima vijiji vyote vile vipimwe vizuri, tuweke mipaka vizuri lakini pia tuimarishe ule ulinzi katika yale maeneo hasa kule ambako kumekuwa na changamoto nyingi ambapo wanyamapori wamekuwa wakiharibu mazao na shughuli za wananchi wanazofanya katika yale maeneo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, pia tutaweka minara, pamoja na kutumia ndege zisizokuwa na Rubani. Kwa hiyo, mambo mengi tutayafanya kuhakikisha kwamba haya yanafanyika. Ili kufanya hayo, lazima tufike na tuone kwamba wananchi wanaondokana na hizi changamoto.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu hatua mbadala; sasa hivi tunatoa elimu ni nini kinaweza kufanyika katika yale maeneo yaliyo jirani na hifadhi? Kwa sababu ukipanda yale mazao ambayo wanyamapori wanayapenda, ni wazi kabisa kwamba yataliwa na wanyamapori. Ukipanda yale mazao ambayo wanyamapori hawayapendi, wanayaogopa, basi kidogo hii itasaidia.

Mheshimiwa Naibu Spika, tutakwenda kukaa pamoja na Mheshimiwa Mbunge na wananchi kwa pamoja, tutashauriana kuona ni aina gani ya mazao ambayo wananchi wa maeneo yale watashauriwa kwamba wayapande ili kuondokana na hii migogoro ambayo imekuwa ikijitokeza katika hayo maeneo. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Zacharia Issaay swali la nyongeza.

**MHE. ZACHARIA P. ISSAAY:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Kwanza naishukuru Serikali kwa kutoa kifuta machozi takribani milioni nane kwa ajili ya wananchi waliopoteza maisha yao na wale walioathiriwa na wanyama wakali.

Mheshimiwa Naibu Spika, mnamo mwaka 2016 Serikali iliahidi kufanya ziara katika Tarafa ya Daudi na Tarafa ya Ndekoti kwa ajili ya wananchi ambao mali zao na mazao yameharibiwa na wanyama wakali, lakini hadi sasa Serikali haijatumia ahadi yake hiyo kwa kuwa wale waliokuwa kwenye Wizara walibadilishwa.

Je, ni lini Serikali itafanya ziara katika Tarafa ya Daudi na Tarafa ya Ndekoti kwa ajili ya wananchi ambao mali zao zimeathiriwa na wanyama ikiwemo mazao na hawajapata kufidiwa hadi sasa? Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kabisa kwamba inawezekana kulikuwa na ahadi ya kwamba viongozi wa Kitaifa wataenda kutembelea katika lile eneo.

Naomba tu nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba hata kama viongozi wa kitaifa hawajafika, bado wapo Watendaji wetu ambao lazima wafike katika yale maeneo na wahakikishe kwamba wanahakiki mali



zilizopotea, wanahakiki uharibifu uliofanyika kusudi wale wananchi wanaostahili kupewa kile kifuta jasho au kifuta machozi, waweze kulipwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, kwa nafasi hii, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba leo hii nitawaagiza watendaji wafike katika lile eneo ili wakutane na hao wananchi, wafanye tathmini na tuone ni kiasi gani wananchi wale wanastahili kulipwa kwa mujibu wa kanuni zetu tulizonazo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu utayari, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tutakuwa tayari, tutakuja pia kuhakikisha kwamba haya yote yanatekelezeka na wananchi waweze kuona kwamba Serikali yao inawajali vizuri. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Pudenciana Kikwembe, swali la nyongeza.

**MHE. PUDENCIANA W. KIKWEMBE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipatia nafasi na mimi niweze kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa matatizo yaliyopo katika Jimbo la Serengeti yanafanana kabisa na matatizo yaliyopo katika Jimbo la Kavuu hasa katika Kata za Chamalendi, Mwamapuli, Majimoto na vitongoji vyake; kumekuwa na matatizo ambayo wananchi hasa wafugaji wamekuwa wakisukumizwa na askari wa wanyamapori ndani ya Mbuga ya Katavi na wamekuwa wakipotea na mara nyingi wakiwa wakitafutwa na ndugu zao ni nguo tu zinapatikana:-

Je, Serikali inasema nini sasa kwa ujumla kuhusu askari wote wa wanyamapori wanaofanya kazi katika mbuga zote za *National Park* katika kuhakikisha usalama wa wale wanaowaita majangili wakati sio majangili? Kwa sababu tu wanakuwa wameingia kwenye mbuga, kwa hiyo, wataitwa majangili.

Je, Serikali inasema nini kuhusu Askari hao ambao wamekuwa wakiwateka wananchi na kuwapora ng'ombe zao na mali...

**NAIBU SPIKA:** Ameshakuelewa Mheshimiwa. Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa swali hilo.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naomba niseme tu kwamba sina taarifa kamili kwamba askari wetu wamekuwa wakiwakamata watu na kuwaingiza kwenye hifadhi halafu wanapotea moja kwa moja. Hizo taarifa hatunazo kama Serikali na kama Mheshimiwa Mbunge anazo na anao ushahidi wa namna hiyo, basi nitaomba nikae naye ili aweze kunipa hayo majina ya watu ambao wamepotea kusudi Serikali iweze kuchukua hatua zinazostahili.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu namna ya kuboresha yale maeneo, naomba nitumie nafasi hii kuwaomba wananchi wote wanaopakana na hifadhi zetu kuhakikisha kwamba wanazingatia taratibu, sheria, kanuni na miongozo iliyopo. Hawaruhusiwi kuingia bila kibali kwenye hifadhi. Kwa kawaida ukiingia kwenye hifadhi bila kibali, ni vigumu sana kujua yupi ni jangili, yupi sio jangili. Kwa hiyo, ili kuweza kuondokana na hilo, ni kuwaomba wananchi kutoingia katika maeneo ya hifadhi ili kusudi tuondokane na hilo tatizo.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea na Wizara ya Nishati. Mheshimiwa Alfredina Apolinary Kahigi, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake. (*Makofi*)

Na. 452

### **Hitaji la Umeme kwa Wananchi wa Kagera**

**MHE. ALFREDINA A. KAHIGI** aliuliza:-

Wananchi wa Kagera wana tatizo la umeme na umeme wa *REA* // umeingia katika *center* za vijiji tu.

Je, ni lini wananchi hao watapatiwa umeme ili waondokane na adha ya kutumia vibatari?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Alfredina Aporinary Kahigi, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, awamu ya pili ya utekelezaji wa miradi ya kusambaza umeme vijijini lililenga pamoja na mambo mengine kufikisha umeme katika maeneo ya njia kuu, baadhi ya maeneo muhimu katika vijiji na katika taasisi za umma. Utekelezaji wa miradi ya *REA* Awamu ya Pili ulikamilika mwezi Desemba, 2016.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia Wakala wa Nishati Vijijini (*REA*) ilianza kutekeleza Mradi wa *REA* Awamu ya Tatu mzunguko wa kwanza tangu mwezi Julai, 2017. Katika Mkoa wa Kagera vijiji vipatavyo 141 vinatarajia kupatiwa umeme kupitia mradi huu. Mradi huu utakamilika mwezi Juni, 2019. Kazi ya kupeleka umeme katika vijiji hivi inahusisha ujenzi wa njia ya umeme wa msongo wa kilovoti 33 yenye urefu wa kilometa 299, njia ya umeme wa msongo wa kilovoti 0.4 yenye urefu wa kilometa 574, ufungaji wa transfoma 287 za KVA 50 na 100 pamoja na kuunganishia umeme wateja wa awali 9,136. Gharama za mradi ni shilingi bilioni 38.

Mheshimiwa Naibu Spika, hadi kufikia mwezi Aprili, 2018 mkandarasi Kampuni ya *Nakuroi Investment Ltd.* aliyepewa kazi ya ujenzi wa miundombinu ya kusambaza umeme katika Wilaya zote za Mkoa wa Kagera alikuwa ameshakamilisha kazi ya upimaji wa maeneo yatakayopelekewa umeme. Kazi zinazofanyika sasa ni kusambaza nguzo katika maeneo ya mradi na kujenga miundombinu, pamoja na kusambaza umeme.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kahigi swali la nyongeza.

**MHE. ALFREDINA A. KAHIGI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi nyingine. Nina maswali mawili ya nyongeza, naomba kuyauliza.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la kwanza, katika Wilaya yetu ya Bukoba Vijijini kuna baadhi ya kata nitazisema japokuwa ni nyingi. Katika Kata ya Rubafu -Kijiji cha Bwendangabo, Kata ya Buma - Kijiji cha Bushasha, Kata ya Bwendangabo - Kijiji cha Kashozi, Kata ya Nyakato - Kijiji cha Ibosa; hizo ni baadhi ya Kata ambazo nimezitaja, lakini ni kata nyingi sana katika Wilaya yetu ya Buboka Vijijini au niseme Mkoa mzima wa Kagera tuna shida ya umeme.

Je, Serikali inaona umuhimu wa kuwapa kipaumbele cha kuweza kuwawekea umeme haraka iwezekanavyo? Hilo ni swali la kwanza.

Mheshimiwa Spika, swali la pili, wananchi wa kata hizo hizo nilizozitaja wamenunua *solar*. *Solar* hizo tayari zimesharibika. Je, Serikali ina mkakati gani wa kuhakiki hizo *solar* kabla hazijaingia sokoni? Ahsante. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati majibu kwa maswali hayo.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, swali lake la kwanza, amezitaja kata mbalimbali katika Wilaya yake ya Bukoba Vijijini na amewakilisha Mkoa mzima na ameeleza ni namna gani Serikali itaweka kipaumbele. Nataka nimthibitishie Mheshimiwa Mbunge kuwa Serikali ya Awamu ya Tano chini ya Rais wetu, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli katika Mkoa huo wa Kagera kwa awamu hii ya tatu inayoendelea jumla ya vijiji 141 vitapatiwa umeme. Katika Wilaya yake ya Bukoba Vijijini, Kijiji cha Burugo kimeshasambaziwa nguzo na kazi zinaendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nimthibitishie Mheshimiwa Mbunge kuwa Kata zile alizozitaja na vijiji alivyovitaja, kwa awamu hii ya kwanza vijiji kwa Bukoba vijijini ni 22, lakini kwa awamu ambayo itaendelea mzunguko

wa pili unaoanza Julai vijiji vyote vilivyosalia vitapatiwa umeme.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali lake la pili, ameuliza masuala ya sola ambazo zimewekwa katika maeneo hayo ya Bukoba Vijijini na maeneo mengine ya Mkoa wake kwamba nyingi zimeharibika. Serikali ina utaratibu ndani ya Serikali na kwa Taasisi mbalimbali. Kwa mfano, kuna masuala ya *TBS* yanavyoangalia viwango na taasisi nyingine za kiserikali za kuangalia bidhaa zinazolingia ndani ya nchi zisiwe bidhaa ambazo kwa kweli ni *fake*.

Mheshimwia Naibu Spika, kwa hiyo, naomba nimthibitishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali yetu itaendelea kuziimarisha zile taasisi zinazohusika na kuzuia bidhaa feki ndani ya nchi ili kujiridhisha na vifaa hususani vya masuala ya nishati viingie vifaa bora na wananchi wapate huduma bora. (*Makofi*)

Mheshimwia Naibu Spika, nakushuruku Mheshimiwa. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Hongoli, swali fupi.

**MHE. JORAM A. HONGOLI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo la umeme lililopo Wilaya ya Kagera linafanana kabisa na tatizo la umeme mradi ule wa Makambako - Songea. Ule mradi umepita katika Kata tatu; Kata ya Kichiwa, Kata ya Igongoro na Kata ya Ikuna. Kwenye maeneo hayo kuna baadhi ya maeneo yana huduma muhimu kama shule, zahanati na vituo vya afya umeme haujapelekwa huko. Nini kauli ya Serikali kwa mkandarasi aliyesambaza umeme kwenye maeneo haya, kuhakikisha kwamba umeme unaenda kwenye maeneo yenye huduma muhimu? Ahsante sana. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Katika mradi unaoendelea Makambako - Songea kwa kweli tunarajia mwezi Septemba mradi ule utakamilika na kuzinduliwa rasmi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kazi inayoendelea ya kusambaza umeme katika maeneo ambayo yameainisha, nataka nimthibitishie Mheshimiwa Mbunge kwamba kwa kuwa miradi hii ya kupeleka umeme vijiji ipo ya aina mbalimbali, kuna mradi wa Makambako - Songea ambao unalenga vijiji 121, lakini sambamba na hilo kuna mradi ambao unaendelea wa *densification* kwa maeneo ya Mkoa wa Njombe na Mkoa wa Iringa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mradi huu, *densification* ya awamu ya kwanza ina vijiji kama 305 na mradi umekamilika umefikia asilimia 98.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, maeneo ambayo hajasalia kama ambavyo tunafahamu mradi wa *REA* Awamu ya Tatu unaendelea na maeneo yale na maelekezo yetu kama Serikali, tumesema taasisi za umma iwe shule, iwe zahanati, iwe miradi ya maji na taasisi zote kwamba kipaumbele kwa wakandarasi waelekeze kwenye maeneo hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, kama Serikali tunaendelea kusesitiza hayo maelekezo na yaendeleo kutekelezwa na Wakandarasi wote. Nimthibitishie Mheshimiwa Mbunge, kwa kweli kwa awamu inayoendelea, changamoto hizi hazitakuwepo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa, tunaendelea na Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji, Mheshimiwa Hassan Elias Masala, Mbunge wa Nachingwea, sasa aulize swali lake. (*Kicheko*)

Na. 453

## **Viwanda vya Kukamua Mafuta Nachingwea**

**MHE. HASSAN E. MASALA** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani juu ya wawekezaji walioshindwa kuendeleza Viwanda vya Kukamua Mafuta vya Ilulu na Kiwanda cha Mamlaka ya Korosho Wilayani Nachingwea?

**NAIBU WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Viwanda, Biashara na Uwekezaji naomba kujibu swali la Mheshimiwa Hassan Elias Masala, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza napenda kulitaarifu Bunge lako tukufu kwamba Serikali inafuatilia kwa karibu ili kuhakikisha kuwa waliobinafsishiwa viwanda wanatimiza wajibu wao ipasavyo na kwamba viwanda hivyo vinafanya kazi kama ilivyokusudiwa kwa mujibu wa mkataba wao na Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa Kiwanda cha Mafuta Ilulu, kiwanda hicho kiliuzwa kwa njia ya ufilisi. Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Msajili wa Hazina imekuwa ikimfuatilia mwekezaji ili kiwanda kilichonunuliwa kichangie katika uchumi wa Taifa letu. Kutokana na ufuatiliaji huo, tarehe 6 Juni, 2018, mmiliki wa Kiwanda cha Mafuta cha Ilulu, alitoa taarifa rasmi kurejesha kiwanda hicho cha Serikalini kwa kuwa ameshindwa kukiendeleza. Taratibu za kisheria zinafuatwa ili kukamilisha makabidhiano hayo rasmi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ofisi ya Msajili itaendelea kuona matumizi bora zaidi ya kiwanda au eneo hilo. Aidha, kwa upande wa Kiwanda cha Korosho Nachingwea, kilibinafsishwa kwa kuuza hisa asilimia 100. Hivyo, uendeshaji wote wa kiwanda upo chini ya mwekezaji binafsi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kiwanda kinaendelea na zoezi la kufunga mitambo ya kubangua korosho na sehemu ya maghala inatumika kuuzia na kuhifadhia korosho za wakulima na wanunuzi. Mpango wa Serikali ni kuhakikisha kuwa kiwanda hicho kinakamilisha ufungaji mitambo na kuanza uzalishaji haraka ifikapo msimu ujao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama ambavyo nilikuwa nimeahidi hapo awali, narudia kusema tena mara baada ya Bunge hili nitatembelea viwanda vyote vilivyobinafsishwa Mkoani Lindi na Mtwara pamoja na maeneo mengine kwa ajili ya ufuatiliaji na tathmini ya viwanda hivyo.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Hassan Elias Masala, swali la nyongeza.

**MHE. HASSAN E. MASALA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa majibu ya Mheshimiwa Waziri, lakini pamoja na majibu hayo naomba niulize maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la kwanza, nilitaka nijue Serikali imejipanga vipi au imejiandaa vipi? Kwa sababu wakati Kiwanda hiki cha Mafuta Ilulu kinabinafsishwa, kilikuwa na majengo pamoja na mitambo yake, lakini ukaguzi niliufanya kwa awamu ya mwisho mpaka sasa hivi huyu mwekezaji anatangaza kukirudisha, kiwanda kile hakina mashine hata moja na amesema kwamba anakirudisha. Nini kauli ya Serikali juu ya mashine ambazo zilifungwa katika Kiwanda kile cha Mafuta cha Ilulu?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu la pili, nilikuwa nataka nijue; kwa sababu Serikali imetoa hisa asilimia 100 kwa wawekezaji kwa ajili ya Kiwanda cha Korosho, ambapo wawekezaji waliopewa ni *Sunshine* na mashine walizozifunga pale hazioneshi kama zinaweza zikafanya kazi ambayo tunaikusudia. Kwa nini Serikali isichukue angalau asilimia 51 ya hisa zile ili Serikali iweze kupata gawio lake la moja kwa moja badala ya kutegemea mwekezaji? Ahsante.



**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Viwanda, Biashara na Uwekezaji, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, kwa upande wa Kiwanda cha Mafuta cha Ilulu ambacho anadai kwamba mashine zake zimeshaondolewa na kiko katika hali mbaya na kinarejeshwa, ndiyo maana tumesema kwamba tutakipokea kufuatana na taratibu za kisheria. Kwa hiyo, tutaangalia masuala yote ya kisheria pale tutakapona kwamba mwekezaji huyu anabanwa na masharti hayo, basi hatua za kisheria zitachukuliwa dhidi yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa kiwanda cha korosho, niseme tu kwamba Serikali ilikuwa imeshajitoa katika kufanya shughuli za uwekezaji na hiyo ndiyo sera yetu. Tunachofanya zaidi ni kuwahamasisha wawekezaji, wao ndio wawekeze na mitaji mingi zaidi iweze kufika na kuwekeza katika nchi. Ila tu katika maeneo yale ambayo tunaamini kwamba pengine kwa mwekezaji binafsi ataona hakuna tija, lakini wakati huo kwa upande wa Serikali tunaona kwamba suala hilo lina manufaa makubwa kwa Watanzania au jamii kwa ujumla, ndipo Serikali inapoingilia na kuweza kuona umuhimu wa kuwekeza.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Wizara ya Kilimo. Mheshimiwa Abdallah Dadi Chikota, Mbunge wa Nanyamba, sasa aulize swali lake.

Na. 454

### **Kuporomoka kwa Bei ya Mbaazi Nchini**

**MHE. ABDALLAH D. CHIKOTA** aliuliza:-

Wakulima wa mbaazi Mikoa ya Mtwara na Lindi wameshuhudia kuporomoka kwa bei katika msimu wa mwaka huu pamoja na kwamba walihamasika kulima kwa wingi.

(a) Je, ni nini kilisababisha kuporomoka kwa bei ya mbaazi?

(b) Je, Serikali inachukua hatua gani ili kuhakikisha hali hiyo haijitokezi msimu ujao?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Abdallah Dadi Chikota, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli bei ya mbaazi iliporomoka kutoka wastani wa bei ya shilingi 2,750 kwa kilo mwaka 2014/2015 hadi shilingi 700 kwa msimu wa mwaka 2016/2017 na kufikia wastani huo na katika mikoa mbalimbali hapa nchini. Hali hii imesababishwa na ongezeko la uzalishaji wa mbaazi katika nchi za India, China, Brazil, Myanmar, Canada, Msumbiji, Sudan na Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na ongezeko hilo la uzalishaji, mwezi Agosti, 2017 nchi ya India ambayo ndio wanunuzi wakuu wa mbaazi zetu ilizuia uingizaji wa mbaazi kutoka nje ya nchi hiyo kwa kuwa walikuwa na uzalishaji mkubwa wa kukidhi mahitaji yao na hivyo kusababisha ukosefu wa soko la uhakika kwa mbaazi zilizozalishwa nchini msimu wa 2016/2017.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuhakikisha wakulima wanapata masoko ya uhakika, Serikali imeandaa mikakati mbalimbali ya muda mfupi na muda mrefu kuimarisha upatikanaji wa masoko ya mazao hususan mbaazi. Mikakati ya muda mfupi ni pamoja na Wizara kupitia Bodi ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko kwamba itaongeza idadi ya mazao yatakayonunuliwa ambayo ni pamoja na mazao ya jamii ya mikunde (mbaazi, choroko na dengi), mbegu za mafuta (ufuta, alizeti na karanga) na nafaka kwa (mtama, ulezi na uwele) katika mwaka 2018/2019. Kwa sasa bodi hiyo imepata soko la tani 100,000 za soya, tani 20,000 za ufuta na tani 3,500 za mbaazi ambazo zitauzwa kwa wadau ndani

ya nje ya nchi. Pia itanunua tani 6,000 za alizeti kwa ajili ya kukamua mafuta katika kiwanda chake kilichopo Kizota, Jijini Dodoma.

Mheshimiwa Naibu Spika, mkakati mwingine wa muda mfupi ni kuuza zao la mbaazi katika soko la bidhaa kwa maana ya *commodity exchange* na kuhamasisha utumiaji wa mbaazi hapa nchini katika maeneo mbalimbali hususan katika mashule na majeshi yetu (Magereza na JKT). Aidha, Serikali kupitia Maafisa Lishe waliopo katika Halmashauri zote nchini, watatoa mafunzo ya namna bora ya kuandaa vyakula vinavyotokana na mbaazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mikakati ya muda mrefu ni pamoja na kampuni kutoka India kujenga Kiwanda cha kiiwacho *Mahashree Agro Processing Ltd* kitakachosindika aina zote za mazao jamii ya mikunde, korosho na ufuta katika Kijiji cha Mtego wa Simba, Kata ya Mkambarani, Wilayani Morogoro kitakachokuwa na uwezo wa kusindika tani 200 za aina mbalimbali ya mikunde kwa siku na kuuza katika soko la ndani na nje. Kiwanda hicho kitasaidia wakulima kupata bei nzuri na soko la uhakika mara kitakapoanza uzalishaji mwaka 2019.

**SPIKA:** Mheshimiwa Abdallah Dadi Chikota, swali la nyongeza.

**MHE. ABDALLAH D. CHIKOTA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, naomba kuulizwa maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa tulitegemea kwamba baada ya kuanzisha Bodi ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko ingekuwa Mkombozi wa mazao mengine ambayo hayana bodi, lakini kuna changamoto ya fedha kwenye bodi hii.

Je, Serikali ina mpango gani wa kutenga fedha nyingi za kutosha ili Bodi ya Nafaka na Mazao iweze kununua mazao mengine pamoja na mbaazi? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; kwa kuwa soko la India limeonesha kulegalega na kwenye zao la korosho tulipoachana na soko la India tumeona kuna mafanikio baada ya kuja Waturuki na Wavietinam; Serikali ina mpango gani wa kuingia kwenye masoko mengine ili kuacha utegemezi wa soko la India?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kumjibu Mheshimiwa Mbunge RAS Mstaafu na kaka yangu Mheshimiwa Chikota maswali yake madogo mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, la kwanza, kama Serikali ni kwamba tumeielekeza na kusioniwa Bodi yetu ya Mazao Mchanganyiko kwamba kuanzia sasa wajikite zaidi katika kufanya biashara ile ya kilimo cha ushindani. Tayari tumeshanza kufanya mazungumzo na *NSSF* na mazungumzo hayo yamefanikiwa na tayari tumeshapata shilingi bilioni 3.6 kwa ajili ya kununua mashine zile kwa ajili ya viwanda vya mahindi na alizeti kwa maana ya mashine mbili na tayari zimeshafika bandarini.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika swali lake la pili la nyongeza, ni kwamba ni vyema sisi kama Serikali; naomba niwaase Halmashauri zote nchini kwamba tutoe elimu kwa wakulima wetu kuweza kufanya kilimo cha kibiashara (*commercial farming*) kwa sababu unapokuwa kwenye *commercial farming*, utaweza kujua ulime kilimo cha aina gani? Mazao gani? Kwa bei gani? Utauzi wapi? Kwa maana hiyo, hakutakuwa na hasara yoyote.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile naomba niwaeleze Waheshimiwa Wabunge kwamba mbaazi ni chakula kama vyakula vingine, tena ina protini zaidi kuliko maharage na inaongeza damu mwilini kuliko maharage. Vilevile nawaomba hata wale wanaofanya vyakula vya mifugo, ni

kwamba hizi mbaazi zetu pia zinatumika vizuri sana katika vyakula vya mifugo kama ilivyokuwa soya. Ahsante. (Makofi)

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea, Mheshimiwa Mohamed Omary Mchengerwa Mbunge wa Rufiji, sasa aulize swali lake.

Na. 455

### **Mradi wa Kilimo katika Bonde la Mto Rufiji**

**MHE. MOHAMED O. MCHENGERWA** aliuliza:-

Mradi wa Kilimo wa *RUBADA* - Rufiji, umekuwa mradi wa kitapeli ambao watu wachache wanajinufaisha na rasilimali za Rufiji bila ya Wana-Rufiji kupata maendeleo yoyote.

Je, ni lini Serikali itafikiria kuleta mradi wa kilimo katika Bonde la Mto Rufiji ambalo kwa miaka mingi liko tupu bila shughuli yoyote ya kilimo hasa ikizingatiwa kuwa bonde hilo lina kila kitu?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Mohamed Omary Mchengerwa, Mbunge wa Rufiji, lenye sehemu mbili, naomba nianze kutoa maelezo ya utangulizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, *Rubada* siyo mradi, bali ilikuwa ni Mamlaka ya Uendelezaji wa Bonde la Rufiji kwa maana ya *Rufiji Basin Development Authority*.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo haya, sasa naomba nianze kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni vema nikiri tu kwamba kulikuwepo upungufu wa kiutendaji ndani ya *RUBADA*.

Kutokana na hali hiyo, Wizara ilifanya uchunguzi mwezi ule wa Oktoba, 2014 na tarehe 8 Aprili, 2015 Wakurugenzi watatu wa *RUBADA* walisimamishwa kazi na hatimaye tarehe 21 Januari, 2016 Bodi ya *RUBADA* iliwaifukuza kazi rasmi Wakurugenzi wawili.

Aidha, kutokana na mabadiliko ya kisera, kisheria na kimfumo, imeonekana kuwa *RUBADA* imekosa uhalali wa kuendelea kuwepo. Hivyo Serikali mnamo mwezi Septemba, 2017 ilileta Muswada wa Sheria Bungeni ukipendekeza kuifuta *RUBADA*. Bunge liliridhia kuifuta *RUBADA* na shughuli zake kuhamishiwa taasisi nyingine za kiserikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inaelewa fursa zilizopo katika Bonde la Rufiji. Hatua kadhaa zimechukuliwa kutumia vizuri fursa hizi. Mathalani, Serikali inatekeleza mradi mkubwa wa Bwawa *Stiegler's Gorge* kwa ajili ya umeme wa megawati 2,100. Bwawa hili pia litawezesha kuhifadhi maji kwa ajili ya umwagiliaji, mifugo na uvuvi. Pia upo mradi wa Bwawa la Maji la Kidunda ambalo pamoja na kutoa uhakika wa maji ya kunywa kwa Jiji la Dar es Salaam litatumika pia kwa umwagiliaji, mifugo na uvuvi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya kilimo kwa kushirikiana na Wizara ya sekta ya kilimo imeandaa programu ya kuendeleza Sekta ya Kilimo Awamu ya Pili kwa maana ya (*ASDP II*) ambapo ina maeneo ya kipaumbele 23 na jumla ya miradi ya uwekezaji kwa maana ya *Investment Projects 56* ya kipaumbele ambayo inajumuisha miradi iliyopo katika Bonde la Mto Rufiji ambayo ilikuwa ikiratibiwa na *RUBADA* chini ya uliokuwa Mpango wa Matokeo Makubwa Sasa (*BRN*). Miradi hiyo ni kama vile iliyopo maeneo ya Muhoro, Tawi, Bumba na Msoro. *ASDP II* inalenga kuendeleza miradi hiyo iliyopo Bonde la Mto Rufiji kama kuweka miundombinu ya umwagiliaji ambapo wananchi wengi watanufaika kupitia programu hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, kaka yangu kuwa miradi hii ikikamilika itaifanya Bonde la Mto Rufiji kuwa lulu ya maendeleo. Kwa

maana hiyo, namwomba kaka yangu Mheshimiwa Mchengerwa avute subira kidogo kuona mabadiliko haya tarajiwa na yenye matokeo chanya.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mohamed Mchengerwa, swali la nyongeza.

**MHE. MOHAMED O. MCHENGERWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, napongeza majibu mazuri ya dada yangu Mheshimiwa Dkt. Mary Mwanjelwa, mchapa kazi na ninaona kabisa anakwenda kuchukua Jimbo la mtu huko Mbeya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nina maswali mawili ya nyongeza; kwanza kabisa Rufiji tunatambua jitihada anazofanya Mheshimiwa Rais za ujenzi wa bwawa la *Stiegler's Gorge* kama ambavyo amelisema Mheshimiwa Naibu Waziri na kwamba tunatambua Serikali inapelekea zaidi ya shilingi trilioni mbili kwenye mradi huu na kuifanya Rufiji kuwa moto moto kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mradi huu wa *Stiegler's Gorge* una zaidi ya ekari 150,000 ambazo zimetengwa kwa ajili ya kilimo. Swali langu kwa Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo: Je, Serikali inawaandaa je Warufiji sasa ili kuweza kupokea fursa hizi za eneo hili la kilimo zaidi ya ekari 150,000 katika kuweka miradi mbalimbali ikiwemo na ule mradi wa kiwanda kikubwa cha sukari kule Rufiji? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu la pili, Watanzania wa Rufiji kwa asilimia 90 wanategemea kilimo na *RUBADA* ilikuwa katika Kata ya Mkongo pale Rufiji; na hii ndiyo kata iliyoathirika sana kwa wafugaji kuingiza mifugo yao eneo la wakulima; je, Serikali inajipangaje kuwasaidia wakulima hususan katika vijiji vya Mbunju, Ruwe pamoja na Mkongo Kusini ambao wameathirika sana kwa mazao yao kuliwa na wafugaji? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, kwanza kipekee kabisa naomba nimpongeze sana Mheshimiwa Mchengerwa, Mbunge wa Rufiji kwa dhati kabisa kwa maana yeye alikuwa ni sehemu mojawapo ya watu ambao walishatueleza na wakatuambia kabisa kwamba mradi huu wa *RUBADA* ni *non-starter* na yeye alikuwa ni sehemu kama Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Sheria, kuleta na kupendekeza kwamba mradi huu wa *RUBADA* haufanyi kazi vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya utangulizi huo, sasa naomba naiende moja kwa moja kumjibu maswali yake madogo sana ya nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kabisa kwamba sisi kama Serikali katika Bonde hili la Rufiji ni hekta 1,350 kwa ajili ya mradi wa *Stiegler's Gorge*. Naomba niseme kwamba eneo la hekta 300,000 limetengwa kwa ajili ya kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba hizo hekta 300,000 zilizotengwa kwa ajili ya kilimo, ni kwa ajili ya *irrigation scheme*. Kwa maana hiyo, naomba nimhakikishie kwamba wananchi wa Rufiji na maeneo mengine yote watanufaika kwenye kilimo kupitia mradi huu ambao unaitwa *irrigation scheme*.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine lile la (b) ni kuhusu suala zima la migogoro aliyozungumzia kuhusu ardhi. Ni kwamba Serikali tumejipanga na mpaka sasa hivi sheria inaandaliwa; tunaangalia suala zima la migogoro hii ya ardhi na maandalizi tayari yameshafanyika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Mbunge avute subira, Serikali inaandaa suala zima la ardhi kwa sababu tumegundua kwamba kuna migogoro mingi sana kati ya wakulima na wafugaji. Nakushukuru. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunamalizia swali la mwisho Wizara ya Maji na Umwagiliaji. Mheshimiwa



Josephine Johnson Genzabuke, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 456

### **Chujio la Maji Katika Mji wa Kasulu**

**MHE. JOSEPHINE J. GENZABUKE** aliuliza:-

Upatikanaji wa maji safi na salama katika Mji wa Kasulu bado ni changamoto kubwa sana, kwani maji yanayotoka kwenye mabomba ni machafu.

Je, ni lini Serikali itatoa pesa kwa ajili ya kununua chujio la maji ili wananchi waweze kupata maji safi na salama?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji na umwagiliaji naomba kujibu swali la Mheshimiwa Josephine Johnson Genzabuke, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatambua tatizo la maji katika Halmashauri ya Mji wa Kasulu ikiwa ni pamoja na miradi ya maji kutokuwa na miundombinu ya kutibu maji katika bajeti ya mwaka 2017/2018. Kupitia Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji, Halmashauri ya Mji wa Kasulu imetengewa shilingi bilioni 3.35 kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu ya maji ikiwemo ujenzi wa miundombinu ya kusafisha na kutibu maji. Hadi sasa usanifu wa miradi minne ya Muganza, Marumba, Muhunga na Kimobwa katika Halmashauri ya Mji wa Kasulu umekamilika na taratibu za kuwapata Wakandarasi watakaotekeleza ujenzi wa miradi hiyo zinaendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, ujenzi wa miundombinu ya kutibu maji ni sehemu ya mradi wa maji wa Kimobwa ambao utaambaatana na uchimbaji wa visima virefu vitano, usambazaji wa bomba la kilometa 14, ujenzi wa tenki lenye

ukubwa wa mita za ujazo 225 na ukarabati wa vyanzo vitatu vya maji kwa ajili ya eneo la mji wa Kasulu.

Mheshimiwa Naibu Spika, miundombinu ya kutibu na kusafisha maji itasaidia kuondoa kero ya ubora duni wa maji yanayotumika hivi sasa hususan maji yanayotoka katika vyanzo vya maji vya Miseno, Nyanka, Nyankatoke na Mto Chai. Hivyo ubora wa maji, uzalishaji na usambaji wa maji kwa pamoja utaongezeka. Lengo ni kuhakikisha maji yanayosambazwa kwa wananchi ni safi, salama na yanayokidhi mahitaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, zabuni kwa ajili ya kazi hiyo imetangazwa tarehe 24 Machi, 2018 na utekelezaji wake utaanza mara tu baada ya mikataba ya ujenzi kusainiwa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Josephine Genzabuke, swali la nyongeza.

**MHE. JOSEPHINE J. GENZABUKE:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la kwanza; katika Kata ya Mwilamvya ndipo yalipo machinjio ya ng'ombe, mbuzi na kondoo. Eneo hilo hupata maji mara mbili kwa wiki au mara tatu, lakini hivi sasa ninavyoongea eneo hilo halina maji na ni muda wa mwezi mzima maji hayapatikani katika eneo hilo.

Je, Serikali iko tayari kutoa pesa kwa mpango wa dharura ili eneo hilo la machinjio liweze kupatiwa maji? *(Makofi)*

Swali langu la pili, katika Halmashauri ya Wilaya ya *Kasulu DC* ipo miradi ya maji ambayo haijakamilika, imefikia asilimia 85 mpaka 95 lakini imekwama kwa ajili ya ukosefu wa pesa; je, ni lini sasa Serikali itamalizia miradi hiyo kwa kupeleka pesa ili miradi hiyo iweze kukamilika na wanawake waweze kuondolewa adha ya upatikanaji wa maji? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji na Umwagiliaji, majibu kwa maswali hayo. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Awali ya yote nampongeza sana Mheshimiwa Mbunge, ni mama shupavu, jasiri, mfuatiliaji na mhangaijaji wa matatizo ya wananchi wa Kigoma hasa katika suala zima la maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi kama Wizara ya Maji hatutakuwa kikwazo kwa wananchi wako wa Mwilamvyi hususan katika eneo hilo la Machinjio katika kuhakikisha wanapata maji safi ili waendeleo na usafi, wakati mwingine usafi ni uhai wa mwanadamu.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali lake la pili kuhusu suala zima la miradi ambayo haijakamilika, nitumie nafasi hii kulishukuru Bunge lako tukufu na wewe mwenyewe kwa Wizara yetu ya Maji kuidhinishiwa fedha na katika Mji huo wa Kasulu umetengewa kiasi cha shilingi 1,466,000,000.

Mheshimiwa Naibu Spika, namwomba Mheshimiwa Mbunge kwa kushirikiana na sisi Wizara na viongozi katika kuhakikisha tunasimamia fedha zile ili ziende zikamilishe miradi ambayo haijakamilika ili wananchi wake waweze kupata maji, salama na yenye kuwatosheleza.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaishia hapo kwa kipindi cha maswali na majibu. Nilete matangazo tuliyonayo hapa mezani. Kwanza, ni matangazo ya wageni. Tutaanza na wageni walioko Jukwaa la Mheshimiwa Spika.

Tutaanza na wageni tisa ambao ni Waheshimiwa Wabunge sita, Wajumbe wa Kamati ya Usalama ya Jamii *(Committee on Community Safety)* na Maafisa watatu kutoka Bunge la Jimbo la Gauteng la nchini Afrika ya Kusini. Nao ni hawa wafuatao; Mheshimiwa Sochayile Khanyile ambaye ni Mwenyekiti *(Committee Chairperson)* please stand up and wave to the house. Thank you very much. Honorable Mike Madladla *(Committee Member)*, Honorable Godfrey Tsotetsi

*(Committee Member), Honorable Mafika Mgcina (Committee Member), Honorable Kate Lorimer (Committee Member), Honorable Michele Clarke (Committee Member), Mr. Sizwe Mayoli (First Secretary Political South African High Commission), Ms. Thabile Malumane (Committee Coordinator) and Ms. Nthabiseng Mofokeng (Committee Administrator), you are all welcome to the House. (Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, pia tunao wageni watatu wa Mheshimiwa Dkt. Harrison Geoge Mwakyembe ambaye ni Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo kutoka Kanisa la *Kingdom Embassy* ambaye ni Nabii Clear Malisa ambaye ameambatana na mke wake Bi. Lisa Malisa. Karibuni sana Nabii Malisa na mke wako. Nabii Clear Malisa, maana Malisa wako wengi. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunao pia wageni wa Waheshimiwa Wabunge mbalimbali tutaanza na wageni 45 wa Mheshimiwa Anna Lupembe ambao ni Wanamaombi kutoka Jijini Dar es Salaam. Karibuni sana wageni wetu. Tunao pia wageni watatu wa Mheshimiwa Marwa Ryoba Chacha, Mbunge wa Serengeti ambao ni watoto wake, Ndugu Esther Chacha, Ndugu Victory Chacha na Ndugu Stephen Mwasanga kutoka Serengeti, Mkoani Mara, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunaye pia mgeni wa Mheshimiwa Halima Bulembo ambaye ni mwanafunzi wa Chuo Kikuu cha Dodoma, Ndugu Badru Shuza, karibu sana. Tunaye pia mgeni wa Mheshimiwa Alex Gashaza ambaye ni rafiki yake kutoka Bukoba Vijijini, Mkoani Kagera na huyu ni Ndugu Khalifa Mutabuzi, karibu sana. Pia nawatambua wageni 42 wa Mheshimiwa Lolesia Bukwimba ambao ni Wanakwaya wa *AICT* Vijana Kanisa la *DVC* kutoka Ipagala Mkoani Dodoma wakiongozwa na Mchungaji Daudi Samweli, karibuni sana. *(Makofi)*

Vilevile tunao pia wageni wanne wa Mheshimiwa Antony Komu ambao ni familia yake kutoka Moshi Mkoani Kilimanjaro akiongozwa na ndugu Jacqueline Antony Komu, karibuni sana.

Tunao pia wageni watatu wa Mheshimiwa Augustino Manyanda Masele ambao ni rafiki zake kutoka Wilaya ya Mbogwe, Mkoa wa Geita, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao pia wageni watatu wa Mheshimiwa James Ole Millya, ambao ni viongozi kutoka Jimboni kwake Simanjiro Mkoani Arusha, karibuni sana. Tunao vilevile wageni nane wa Mheshimiwa Mahmoud Mgimwa ambao ni familia yake na wapiga kura wake kutoka Wilaya ya Mufindi Mkoani Iringa, karibuni sana. *(Makofi)*

Wengine ni wageni nane wa Mheshimiwa Selemani Moshi Kakoso ambao ni viongozi wa Kampuni ya Maxmalipo kutoka Jijini Dar es Salaam wakiongozwa na mwanzilishi wa kampuni hiyo Ndugu Juma Rajabu, karibuni sana. Pia wapo wageni watano wa Mheshimiwa Constantine Kanyasu ambao ni familia yake kutoka Mkoani Geita wakiongozwa na mke wake Ndugu Christina Bunini, karibuni sana. *(Makofi)*

Naona Waheshimiwa Wabunge wanamkaribisha wifii yao hapa na wengine ni shemeji. *(Makofi)*

Wageni Saba wa Mheshimiwa Mendrad L. Kigola ambao ni Wajumbe kutoka *Peace Cop Tanzania* ya Mufindi Mkoa wa Iringa, karibuni sana *and you are welcome*. Tunao pia Wageni Watatu wa Mheshimiwa Joram Hongoli ambao ni wapiga Kura wake kutoka Lupembe Mkoani Njombe wakiongozwa na Katibu wa CCM Kata ya Kichiwa Ndugu Barton Makweta, karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunao pia wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo na hawa ni Wanafunzi 66 kutoka Chuo Kikuu cha Kilimo Sokoine *(SUA)* kilichopo Mkoani Morogoro. Naona hawapo pengine wataingia baadae kidogo. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, ninayo matangazo mengine, tangazo lingine linatoka kwa Katibu wa Bunge anawatangazia Waheshimiwa Wabunge kwamba mwezi Februari, 2018 Ofisi ya Rais Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi

wa Umma iliwaandikia barua baadhi ya Wabunge kuwataka wawasilishe vielelezo vinavyothibitisha umiliki halali wa mali walizoziainisha kwenye fomu ya Tamko la Viongozi wa Umma kwa ajili ya uhakiki. Waheshimiwa Wabunge ningewasihi msikilize kwa makini hili tangazo ni muhimu.

Kwa kuwa Wabunge wengi hawakutekeleza rai hiyo, sasa Sekretarieti ya Viongozi wa Umma inawakumbusha kufanya hivyo kabla ya siku ya Jumatatu tarehe 25 Juni, 2018. Taarifa zinazotakiwa kuwasilishwa kwa ajili ya uhakiki huo ni nyaraka zinazohusu fedha zilizoko benki au taasisi nyingine za fedha, hisa, gawio, nyumba, majengo, mashamba, mifugo, madini, mashine, viwanda na mitambo, magari na aina nyingine za usafiri, rasilimali au maslahi mengine ya kibiashara, madeni na mikopo kwa mali zote zilizopo ndani na nje ya Tanzania. Mwakilishi wa Kamishna wa Sekretarieti ya maadili atafika ofisini kwa Katibu wa Bunge kuchukua taarifa hizo. Aidha, kwa Waheshimiwa Wabunge ambao hawakuwahi kupokea wito huo wanatakiwa kuwasilisha vielelezo vya taarifa kama hizo kwenye ofisi za Sekretarieti za Kanda kama ifuatavyo:

Kanda ya Dar es Salaam Ofisi ya Kanda ya Dar es Salam Mikoa inayohudumiwa ni Dar es Salaam na Zanzibar, Kanda ya Mashariki Ofisi ya Mkuu wa Mkoa Pwani- Kibaha inahudumia Mikoa ya Pwani, Morogoro na Tanga. Kanda ya Kaskazini *Arusha AICC* itahudumia Arusha, Kilimanjaro na Manyara. Kanda ya Kati Dodoma Kilimani itahudumia Dodoma na Singida. Kanda ya Magharibi Tabora itahudumia Tabora, Kigoma na Simiyu. Kanda ya Ziwa Mwanza, itahudumia Mwanza, Geita, Kagera, Shinyanga na Mara. Kanda ya Kusini Mtwara itahudumia, Mtwara, Lindi na Ruvuma. Kanda ya Nyanda za Juu Kusini *Mbeya NBC House* itahudumia Mbeya, Iringa, Njombe, Katavi, Songwe na Rukwa.

Waheshimiwa Wabunge waliokuwa wamepata wito huo wapeleke hizo taarifa na hata ambao hawakupata wito huo wanaombwa kuwasilisha vielelezo vya mali walizonazo na madeni waliyonayo. Ndiyo maana niliwaambia

Waheshimiwa Wabunge tusikilize kwa makini na tarehe ya mwisho ni tarehe 25 Juni, 2018.

Waheshimiwa Wabunge ninalo tangazo lingine kutoka kwa Katibu wa Bunge, anawatangazia Waheshimiwa Wabunge kwamba kesho siku ya Jumaatano tarehe 20 Juni, 2018 kutakuwa na kongamano kuhusiana na masuala ya VVU (UKIMWI), hususani wajibu wa viongozi katika kufikia malengo ya 909090 ifikapo mwaka 2020. Kongamano hilo litafanyika katika Ukumbi wa Msekwa kuanzia saa 7:00 mchana hadi saa 10:00 alasiri ambapo mgeni rasmi atakuwa Mheshimiwa Spika.

Waheshimiwa Wabunge, naomba tusikilizane kidogo wengi mnaongea sana na mimi nimesimama na ninyi mnaifahamu Kanuni zinasemaje, naomba tusikilizane kidogo Waheshimiwa Wabunge tafadhali. Aidha, kuanzia saa 3:00 usiku kutakuwa na majadiliano (*round table discussion*) kuhusu maudhui hayo ambayo yatahudhuliwa na Mheshimiwa Spika, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge, Kazi, Vijana, Ajira na Watu Wenye Ulemavu, Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, mwakilishi wa wadau wa maendeleo na mwakilishi wa AZAKI.

Vilevile siku ya Alhamis tarehe 21 Juni, 2018 kutakuwa na maonesho ya shughuli zinazofanywa na AZAKI mbalimbali katika kufikia malengo ya 909090, maonesho hayo yatafanyika nyuma ya Ukumbi wa Msekwa sambamba na zoezi la upimaji wa virusi vya UKIMWI kwa hiari. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge ninalo pia tangazo kutoka kwa Mheshimiwa Anna Lupembe ambaye ni Mwenyekiti wa Ibada, *Chapel* ya Bunge, anawatangazia Waheshimiwa Wabunge wote wa imani ya kikristo kwamba leo kutakuwa na ibada katika eneo la wazi la *basement* mara baada ya kuahirisha shughuli za Bunge saa 7:00 mchana. Katika ibada hiyo kutakuwa na Mtumishi wa Mungu *Prophet Clear Malisa* wa Kanisa la Ubungo Kibangu, Dar es Salaam na kwaya ya

A/CT Vijana kutoka Dodoma itahudumu. Waheshimiwa Wabunge wote mnakaribishwa kwenye ibada hii muhimu.

Waheshimiwa Wabunge, mtakumbuka Mheshimiwa Spika jana alitangaza kwamba Uwanja wa Jamhuri leo kutakuwa na pamoja na mambo mengine kutakuwa na upimaji wa Waheshimiwa Wabunge wa hiari wa Virusi vya UKIMWI na Waheshimiwa Wabunge wengine walioenda kwenye mazoezi walishaanza kuonesha mfano, na mfano huu wa leo umeonyeshwa na Mheshimiwa Ali Keissy na Mheshimiwa Daimu Mpakate wao wameshapima. Tutawauliza baadae kama wamechukua na majibu maana kupima ni suala moja, kuchukua majibu ni la pili, kwa hiyo tutawauliza baadae. *(Makofi/Kicheko)*

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo tutaendelea.

## MWONGOZO WA SPIKA

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Abdallah Bulembo na Mheshimiwa Goodluck Mlinga. Wote mliosimama ni miongozo? Waheshimiwa Wabunge nawakumbusha siku zote tukae anapoanza mwenzio kuzungumza Mwongozo isome vizuri ile Kanuni, ili usije ukajisikia vibaya nitakapokujibu hapa namna unavyoleta Mwongozo wako. Mheshimiwa Abdallah Bulembo.

**MHE. ABDALLAH M. BULEMBO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Ninaomba Mwongozo wangu ni Kanuni ya 68 (7) tukio la leo ni kwenye swali namba 454 linalohusiana na mazao lililoulizwa na Mheshimiwa Abdallah Chikota.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Mwongozo wako kwa sababu ya wakulima wa pamba wa Mkoa wa Mara na Wilaya zake wamekumbwa na tatizo ambalo Wizara ya Kilimo walishajibu hapa kwamba siyo lazima mkulima wa Pamba aende kufungua akaunti ndiyo aweze kuuza pamba yake. Mikoa ya Shinyanga, Geita, Simiyu wao wanaendelea, lakini Mkoa wa Mara Wakuu wa Wilaya wamekataa,



kwamba lazima wale wakulima wakafungue akaunti ndio waweze kuuza pamba yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Mwongozo wa Serikali wakulima wa Mkoa wa Mara dhambi yao ni ipi? Kwa nini wanatofautishwa na wakulima wa Mikoa mingine? Naomba Serikali itolee tamko na iweze kutoa agizo ili wakulima hawa waache kuteseka na pamba yao.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Goodluck Mlinga.

**MHE. GOODLUCK A. MLINGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Naomba Mwongozo kupitia Kanuni ya 68(7) ambao unatokana na tangazo lako ulilotangaza sasa hivi.

Kwanza naomba niipongeze Serikali yetu kwa uhakiki wa mali za Wabunge na kutaka nyaraka ili kutaka kuthibitisha kuwa mali walizonazo ni kweli za kwao. Pia niipongeze Serikali kwa kuhakiki watumishi hewa na watumishi ambao hawana sifa kulingana na kazi zao.

Naomba Mwongozo wako huu uhakiki usiishie tu kwenye mali, kwa sababu sifa za Mbunge mojawapo ni kujua kusoma na kuandika. Tumeshuhudia katika Bunge lako hili tangu Bunge la Bajeti lianze Wabunge wa Kambi Rasmi ya Upinzani wameshindwa kuwasilisha hotuba zao kwa sababu hawana mtu wa kuwaandika.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Mwongozo wako, kwa sababu wamelithibitisha hili wao wenyewe jana kuwa wamepata mtu wa kuwaandikia, ndiyo maana wameleta hotuba yao. Nilikuwa naomba Mheshimiwa Spika atengue teuzi zao Wabunge wote wa Kambi Rasmi ya Upinzani kwa sababu hawajui kuandika ili uchaguzi ufanyike tena. Pia nilikuwa naomba uhakiki sasa uanze kwa Wabunge na mimi nimewasaidia nilikuwa ninamhakiki Mheshimiwa Musukuma asubuhi na ameweza kuniandikia majina matatu ya Spika kuwa nimethibitisha kuwa anaweza kusoma na kuandika.  
*(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba mwongozo wako.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Frank Mwakajoka.

**MHE. FRANK G. MWAKAJOKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba mwongozo wako kwa Kanuni ya 68(7) ninataka mwongozo wako kwa watu ambao wanafanya mzaha, Wabunge ambao wanatumia nafasi hiyo kufanya mzaha ndani ya Bunge wakati hiki ni chombo muhimu sana na ni mkutano wa wananchi na wananchi wengi wanataka kusikiliza nini kinachozungumzwa kuhusiana na masuala muhimu ya kitaifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wapo Wabunge humu ndani ya Bunge wanafanya mzaha wanatumia Bunge hili kufanya mzaha kama michezo, michezo ambayo wanafanya huko nje na wanalipwa na Bunge na hizi fedha ni fedha za wananchi. Lakini kilichozungumzwa leo na Mheshimiwa Goodluck Mlinga kwamba Wapinzani wameshindwa kuandika hotuba yao, nataka nimkumbushe pia kwamba ujue kabisa kwamba hata Mawaziri wote hawa hawajawahi kuandika hata siku moja hotuba zaowanaandikiwa, pia wapo masekretari wanaandika. Kwa hiyo, hicho alichokuwa anakizungumza Mheshimiwa Goodluck Mlinga ni kitu ambacho hakifahamu.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunataka tumkumbushe kwamba Sekretarieti ya Katibu wa Bunge wanafanyakazi kubwa ya kuhakikisha kwamba wanaandaa hotuba zote za Mawaziri.

**MBUNGE FULANI:** Sekretarieti ya Wizara.

**MHE. FRANK G. MWAKAJOKA:** Mheshimiwa Spika, Sekretarieti za Wizara wanafanyakazi kubwa kuhakikisha wanaandaa hotuba, pia zote zilizowasilisha hapa...

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Frank Mwakajoka unaniomba Mwongozo mimi ukianza kumjibu yule maana yake wewe unachukua nguvu zangu mimi. Wewe omba

mwongozo wa hilo jambo unalotaka kulisema hoja yako na nadhani umekwisha kueleweka. Unataka mwongozo juu ya alichokisema hapa ndani kwamba watu wanafanya mzaha si ndiyo? Nadhani hiyo ndiyo hoja yako, kwa hivyo kaa umeshaeleweka.

**MHE. FRANK G. MWAKAJOKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni mzaha kwa kweli mzaha umezidi ndani ya Bunge.

**NAIBU SPIKA:** Sawa umeshaeleweka. Mheshimiwa Kitwanga.

**MHE. CHARLES M. KITWANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, natumia Kanuni ya 68(7) Mwongozo wangu unahusu maelezo uliyoyotoa kuhusiana na uhakiki wa mali zetu. Kwa wale ambao tulikuwa hatujapata barua, vithibitisho/vihakiki vyetu viko katika maeneo yetu kule nyumbani. Tarehe 25 Juni ni karibu sana ukizingatia kwamba tarehe 26 Juni tunatakiwa kuwepo Bungeni kupitisha bajeti ya Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Mwongozo wako je, haiwezi kutolewa nafasi zaidi ili tuweze kupeleka hivi viambatanisho baadae? (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, nimeombwa miongozo minne. Kwanza ni Mwongozo niliombwa na Mheshimiwa Abdallah Bulembo, amehusianisha Mwongozo wake na swali namba 454, amezungumzia wakulima wa pamba kwamba wapo wakulima ambao wanalazimishwa kufungua akaunti benki wakati maeneo mengine wanaruhusiwa kuendelea kuuza pamba yao.

Sasa ametaja Mkoa wa Mara kwamba wanalazimishwa kufungua akaunti wakati sehemu nyingine wanaruhusiwa kuuza pamba. Kwa sababu namna hata yeye alivyolizungumza ni kwamba Serikali ilishatoa maelekezo kwamba hiyo siyo moja wapo ya mambo ambayo wakulima wanatakiwa kulazimishwa, kwa sababu benki kuna maeneo ya vijijini ambapo hayajafika. Mwongozo wangu kwenye jambo hili ni kwamba watendaji walioko huko Mara ambao

wanalazimisha hawa watu kufungua akaunti waache, maana Serikali ilishasema jambo hilo. (Makofi)

Waheshimiwa Wabunge, pia nimeombwa Mwongozo na Mheshimiwa Goodluck Mlinga, akisema kwamba tangazo lililotoka kuhusu uhakiki wa mali tuendelee na hilo zoezi lisiishie kwenye kuhakiki mali, pia tuendelee na kuhakiki Waheshimiwa Wabunge kujua kusoma na kuandika. Ameeleza habari ambayo imetokea jana hapa na amelikusisha na hili tangazo la kuhakiki mali.

Waheshimiwa Wabunge, tangazo hili linahusu uhakiki wa mali haliwezi kuhusishwa na uhakiki wa sifa za Waheshimiwa Wabunge kujua kusoma na kuandika. Kwa sababu uhakiki huo huwa unafanywa kabla ya huyo Mbunge kuwa na sifa za kugombea. Kwa hiyo, wakati akija hapa maana yake lazima atakuwa anazo hizo sifa ambazo zimeainishwa Kikatiba na Kisheria.

Waheshimiwa Wabunge, nimeombwa Mwongozo na Mheshimiwa Frank Mwakajoka naye anatoa hoja yake kwamba anataka kujua mzaha ambao hutokea mara nyingi humu ndani na kwamba Waheshimiwa Wabunge mara nyingine tunatumia muda huo kufanya mzaha badala ya kufanya mambo ya msingi.

Waheshimiwa Wabunge, wakati akitoa maelezo yake ameelekeza mzaha huo kwa Mheshimiwa Goodluck Mlinga, ni wazi kwamba Mwongozo aliokuwa anauomba alikuwa amesimama hata kabla Mheshimiwa Mlinga hajapewa fursa ya kuzungumza. Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge kwenye jambo hili la mzaha anaodhaniwa kwamba amefanya Mheshimiwa Mlinga kwa kutumia muda hapa ndani ni namna ile ile ambayo Mbunge mwingine anakuwa amesimama na kuzungumza mambo ambayo hayana uhusiano na jambo ambalo linakuwa lipo mbele yetu.

Waheshimiwa Wabunge, hivyo mnakumbushwa Waheshimiwa Wabunge kuzingatia kanuni zetu zinachosema ili tusifanye mzaha na hasa pale ambapo wanakuwepo wageni, hii haimaanishi kwamba Mheshimiwa Mlinga alichokifanya ndiyo mzaha.

Waheshimiwa Wabunge, nimeombwa Mwongozo na Mheshimiwa Charles Kitwanga akielezea kuhusu tangazo lililolitoa lililotoka kwa Katibu wa Bunge kuhusu tarehe ya mwisho ambayo Waheshimiwa Wabunge mnatakiwa kuwasilisha taarifa zinazohusu uthibitisho wa mali zenu ama vielelezo vya mali na madeni yaliyoko nje na ndani ya nchi, ili Tume yetu iweze kufanyakazi yake kwa ukamilifu na Mheshimiwa Kitwanga ameeleza kwamba kwa muda uliotolewa kwa wale ambao hawakupewa taarifa na Tume, inaweza ikawa ngumu kuwasilisha vielelezo hivyo maana mtakuwa bado mpo Dodoma na hamjapata nafasi ya kwenda kuvifuatilia.

Waheshimiwa Wabunge, yako makundi mawili hapa, kundi ambalo walishaambiwa wawasilishe hivyo vyeti, wawasilishe vielelezo vya mali zao basi wao wafanye hivyo. Kwa hili kundi la pili ambalo halikuwa na hizi taarifa tutaangalia namna ya kuwasiliana nao ili pengine vielelezo hivyo viweze kuwasilishwa katika muda ambao Waheshimiwa Wabunge mtakuwa mmesharudi Majimboni kwenu na kuweza kuvikusanya na kuvipeleka.

Kwa hiyo, hoja hii ya hili kundi la pili ambalo halikupata hizo taarifa basi tunalifanyia kazi na nadhani mtapata tangazo kwamba sasa mnatakiwa kupeleka lini kwenye hiyo Tume. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, baada ya hayo tunaendelea, Katibu.

**NDG. PAMELA PALLANGYO - KATIBU MEZANI:**

**HOJA ZA SERIKALI**

**Hali ya Uchumi wa Taifa kwa mwaka 2017 na Mpango wa  
Maendeleo wa Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019**

**Na**

**Mapendekezo ya Serikali kuhusu Makadirio  
ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa  
Fedha 2018/2019**

*(Majadiliano yanaendelea)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, majadiliano ambayo tulianza jana yanaendelea leo. Kwa hiyo, ninayo orodha ya majina hapa ya wachangiaji kutoka kwenye vyama vyetu. Tutaanza na Mheshimiwa Mussa Mbarouk, atafuatiwa na Mheshimiwa Zuberi Kuchauka na Mheshimiwa Richard Mganga Ndassa ajiandae.

**MHE. MUSSA B. MBAROUK:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijaalia afya njema na kuweza kuchangia katika hotuba hii ya Wizara ya Fedha. Pili, ninawashukuru wapiga kura wangu wa Jimbo la Tanga kwa ushirikiano ambao wananipa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitaanza kuchangia kwenye Mpango. Katika kitabu cha mpango, ukurasa wa tisa, limeelezwa kwamba pato halisi la Serikali limefikia trilioni 50 vilevile pia ni ongezeko la karibu trilioni 3.35 ukilinganisha na mwaka 2016.

Sasa hapa naona kuna marekebisho kidogo kwa sababu ukipiga hesabu vizuri, mgawanyo wa pato la Taifa kwa kipato cha kila Mtanzania kupata shilingi 2,275,601,000

kutoka shilingi 2,086,168,000 za mwaka 2016 naona panahitaji marekebisho kidogo. Namuomba Waziri alifanyie marekebisho hili ili kusudi hesabu hizi zikae sawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikija kwenye suala la mfumuko wa bei. Katika Mpango ukurasa wa 12 kwenye kitabu kimeeleza kwamba mwenendo wa mfumuko wa bei ulikuwa tulivu. Sasa ukisema kwamba mfumuko wa bei ulikuwa tulivu wakati tuna mifano hai katika mwezi Mtukufu tu wa Ramadhani uliopita juzi ambapo leo ni siku nne tangu umemalizika, naona sio sawasawa. Kwa nini nasema hivyo? Kwa sababu ukiangalia bei ya kio moja ya tambi kutoka shilingi 1,800 ilipanda mpaka shilingi 2,500 vilevile pia sukari kutoka kilo moja shilingi 2,000 ilipanda mpaka shilingi 2,500, ngano kutoka 1,200 ilipanda mpaka shilingi 1,800, vilevile pia mafuta ya kula kutoka shilingi 2,200 kwa lita yalipanda mpaka shilingi 3,000. Sasa tukisema kwamba eti mfumuko wa bei ulikuwa tulivu naona hilo haliko sawa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo nataka kulizungumza katika kitabu chetu hiki cha Mpango ni katika ukurasa wa 55 kuna ubia kati ya Sekta ya umma na sekta binafsi. Nimeona kwamba wamezungumzia zaidi katika masuala ya viwanda kwamba sekta ya umma ishirikiane au iwe na ubia na Serikali lakini kuna vyanzo vingine ambavyo vingeweza kuisaidia Serikali kimapato. Kwa mfano, kama Serikali ingeweza kuingia ubia na sekta binafsi na kuweza kujenga viwanja vya michezo kama vile michezo ya *football*, *basketball*, *golf* na *tennis*, angalau pia tungekuwa hapo tumeweka mazingira mazuri kati ya Serikali na sekta binafsi na ingeweza kutupatia kipato kwa sababu katika mipango hiyo sikuiona katika kitabu, sasa nashauri mipango hiyo nayo iingizwe katika Mpango wa Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ni uandaaji wa wachezaji wetu. Nchi za wenzetu nyingi zimekuwa zinanufaika baada ya wachezaji wao kuwa wanacheza katika nchi za Ulaya. Kwa mfano, nchi kama Nigeria, Senegal, Mali, Tunisia, Algeria na nyinginezo, wameweza kukusanya mapato, hata Brazil Serikali inakusanya kodi kutoka kwa

wachezaji kwa sababu kunakuwa na maandalizi maalum, lakini katika kitabu hiki sijaona kama kuna mpango wa kuiendeleza sekta ya michezo kupitia hivyo viwanja hata kwa wachezaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ambalo nataka kulizungumzia sasa niende moja kwa moja kwenye bajeti yetu. Katika bajeti kuna kitu ambacho ninakiona hakiko sawa, kwa mfano, katika bajeti ya Wizara ya Kilimo tumeona hapa kuna upungufu wa karibu asilimia 23 ambayo ni sawasawa na karibu kwa mfano katika fedha za korosho kuna pesa ambazo zilikuwa ni shilingi bilioni 211 za Mikoa ya Kusini, hizi zimeleta mkanganyiko, hazijapelekwa na hazijulikani ziko wapi.

Sasa atakapokuja Waziri hapa atueleze pia kwanini ninagusa kwenye zao la korosho kwa sababu na sisi Tanga katika baadhi ya maeneo korosho zinalimwa. Sasa ikiwa imeguswa Mikoa ya Kusini maana yake na Tanga pia imeguswa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ni katika kupunguza kodi kwa taulo za kike. Mimi naipongeza Serikali kwamba imepunguza kodi, lakini katika siku za karibuni mimi nilichangia nikatoa mfano wa nchi ya Kenya. Rais Uhuru Kenyatta alitia saina sheria ambayo Kenya watazitoa taulo bure badala ya kusema wanapunguza kodi. Kwa nini ninalisema hili? Kenya wameondoa kodi lakini wakaamua pia zitolewe bure, hapa katika viwanda ambavyo vinazalisha hizo taulo za kike, baadhi ya viwanda vimepunguziwa tu kodi, lakini baadhi ya kodi zipo. Kwa hiyo, tufikirie wale watoto wa kike ambao wako maeneo ya vijijini, hiyo taulo ya kike iliyokuwa inauzwa shilingi 3,500 hata ikiuzwa shilingi 1,500 bado kwao itakuwa ni tatizo kwa sababu hawana njia za kipato ambazo zitawawezesha kulipia taulo hizo za kike. Kwa hiyo, naishauri Serikali badala ya kuondoa kodi, zitolewe bure kwa watoto wa kike. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ambalo napenda kulichangia ni kuhusu wastaafu. Serikali yetu kwanza



katika kipindi cha miaka miwili hii tumeshindwa kuongeza mishahara ya wafanyakazi. Sasa bado pamoja na kushindwa kuongeza mishahara, kuna tatizo la wastaafu, wale waliokuwa watumishi wa Serikali waliongezewa kutoka shilingi 50,000 mpaka shilingi 100,000 tena wanalipwa kila mwezi, lakini wale waliokuwa watumishi wa mashirika ya umma bado wako pale pale katika kiwango cha shilingi 50,000 na wanaendelea kulipwa shilingi 50,000 tena kwa malimbikizo baada ya kila miezi mitatu.

Kwa hiyo, naishauri Serikali kwanza hawa wastaafu waliokuwa katika Mashirika ya Umma nao waongezewe wafikie shilingi 100,000 lakini walipwe kila mwezi na isiwe wanalipwa kila baada ya miezi mitatu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ninalopenda kulizungumza ni deni la ndani tumeambiwa ni himilivu, lakini bado kuna wazabuni ambao wana-*supply* vyakula katika magereza, katika shule na taasisi nyingine ambazo zinahitaji vyakula kama vile hospitali. Wazabuni hawa wengine wanapelekwa mahakamani, wanadaiwa kwa muda mrefu na kila mwaka imekuwa inatolewa ahadi tu kwamba wataanza kulipwa.

Kwa hiyo, nashauri Serikali ituambie hapa/Waziri atakapokuja atuambie ni lini wataanza kuwalipa wazabuni ambao wanadai Serikali. Kwa mfano, katika Jiji letu la Tanga wapo wazabuni wengi tu ambao wanadai ambao wame-*supply* vyakula magerezani, hospitalini na shuleni, lakini nimeshuhudia wengine wanataka kufilisiwa, walichukua mikopo kwenye benki, wanashindwa kulipa mikopo ile lakini Serikali inaendelea kuwapa ahadi. Naitaka Serikali ijibu kwamba ni lini wazabuni wale watalipwa fedha zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ni katika miradi. Miradi bado inapelekwa fedha kwa kuchelewa na fedha hizi zinakuwa hazitoshi na bahati mbaya mara nyingi zinapelekwa katika robo ya mwisho ya mwaka wa fedha wa Serikali matokeo yake sasa miradi baada ya kuwa fedha zimeshafika Wakurugenzi, wataalam na wanaohusika

wengine inapelekwa haraka haraka matokeo yake inakuwa chini ya viwango. Kwa hiyo, naishauri Serikali iendelee kupeleka fedha mapema lakini pia namtaka Waziri wa Fedha Tanga katika Halmashauri yetu tumetenga shilingi milioni 300 kwa jengo la Hospitali ya Wilaya na tulikwishaanza kipindikilichopita (mwaka jana) tukajenga *administration block* kwa takriban shilingi milioni 400 lakini sasa hatujapata fedha kwa ajili ya kuweka hii *OPD*, kwa hiyo naiomba Serikali ituongeze fedha ili tuweze kujenga jengo la *OPD*.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo jingine ni kuhusu wastaafu wanaotarajiwa kustaafu, kama Serikali imeshindwa kuwalipa wafanyakazi au kuwaongezea mishahara katika miaka miwili hii, je hawa watakaostaafu mwaka huu, Serikali ina fedha za kuwalipa? Naomba atuthibitishie Mheshimiwa Waziri wa Fedha kwamba hata watakaostaafu waweze kulipwa fedha zao. Kwa nini nalisema hili? Naogopa kwamba Watanzania wataendelea kuwa maskini na mtu baada ya kustaafu anakuwa hana umri mrefu, anapoteza maisha kwa sababu anakuwa hana kipato. Kwa hiyo, ninamtaka Waziri atakapokuja hapa aje atuambie kwamba wamejiandaa vipi kuwalipa wastaafu wanaotarajiwa kwa sababu watumishi wengi wa Serikali ni wastaafu watarajiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la mwisho...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa muda wako umekwisha.

**MHE. MUSSA B. MBAROUK:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Zuberi Kuchauka, atafuatiwa na Mheshimiwa Richard Mganga Ndassa, Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu ajiandae.

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante na mimi kunipa nafasi nitoe mchango wangu kwenye hii bajeti iliyoko mbele yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza niombe tu kusema kwamba hii bajeti tatizo kubwa haiakisi maisha ya wananchi wetu wa kawaida na ndiyo maana kuna baadhi ya watu wengine wanasema hii bajeti ni bajeti hewa, kwa sababu ukiangalia kwenye vipaumbele vilivyoandikwa hapa haijaakisi kabisa maisha ya wananchi wetu wa chini. Kwa mfano, kwenye miradi hii ya kipaumbele, ukiangalia hata kwenye bajeti wamesema kwamba haitetwi fedha za kutosha, hakuna fedha ambazo zimeenda huko fedha za kutosha. Kwa mfano, wamesema kwamba miradi ya kipaumbele kama vile Rufiji. Rufiji mwaka jana ilitengewa shilingi bilioni 220 hivi lakini wakaipeleka shilingi bilioni tatu, sasa unashindwa kuoanisha tatizo liko wapi?

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo kubwa ambalo naliona bajeti hii inaanza kuharibika tangu kwenye mipango. Mipango tunayopanga na tunapokwenda kutekeleza tunatengeneza vitu tofauti. Niwatolee mfano, kwenye mipango utakuta kuna miradi ya *LNG*, Mkuza, kuna huo mradi wa Rufiji, kuna *Special Economic Zone*, kuna makaa ya mawe, kuna *General Tyre*, mambo ya barabara na kufungamanisha kwamba uchumi na maisha ya wananchi. Lakini tunapokwenda kutekeleza, tunatekeleza vitu vingine ambavyo havimo kwenye mpango.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano kwenye bajeti iliyopita hapa nimesikia kuna majengo ya Chuo Kikuu ambayo hayakuwemo kwenye mpango, lakini yamejengwa, kuna ujenzi ule wa *Magomeni Quarter* umeanza kujengwa lakini kwenye mpango haukuwemo, kwenye ukuta pamoja na kwamba ni jambo zuri kwenye huo ukuta wa Tanzanite, haukuwemo kwenye mpango lakini umejengwa. Kwa hiyo, utakuta kuna miradi ambayo inakamilika ujenzi wake, haimo kwenye mpango, lakini ile miradi ambayo imo kwenye mpango haitetwi fedha. Kwa hiyo, kufeli kwa bajeti hii kunaanzia tangu kwenye mipango yetu kwa sababu

tunachokipanga sicho tunachokitekeleza. Tunapanga kama Taasisi, kama mpango, Wachumi wanakaa wanapanga lakini inapokuja kwenye utekelezaji mtu anatoa matamko mengine yanafanyika mambo mengine, matokeo yake zile fedha ambazo zilitakiwa ziende huku, zinaenda huku. Kwa hiyo kwa msingi huu, nasema kabisa kwamba bajeti hii haiwezei kukidhi matakwa ya wananchi wetu. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hivi tunaingia kwenye nchi ya viwanda na uchumi wa kati, hivi kweli kama tunakisahau kilimo, hatutaki kuwekeza kwenye kilimo tuna dhamira kweli ya kwenda kwenye viwanda? Haiwezekani kwenye bajeti ukapanga asilimia 0.4 ziende kwenye kilimo, kilimo ambacho kinaajiri zaidi ya asilimia 65 ya Watanzania halafu mkasema kweli tuna nia thabiti, mimi siwezi kuunga mkono jambo hili. Kwa mfano, unaona kwamba mifugo imepangiwa 0.1, uvuvi ndiyo kabisa, mmeua mmepangia 0.06 maana yake tuendeleo kula wale samaki wa China ambao wanakuja miaka mitatu iliyopita. Sasa tunaposema kwamba hii haiakisi maisha ya wananchi tunamaanisha hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano mimi natoka Liwale, wananchi wangu kule ni wakulima siyo wafugaji, wale ni wakulima lakini sasa naomba nimuulize Mheshimiwa Waziri, wakulima wale mimi nikawaambie nini kwenye bajeti hii? Sisi zao letu la uchumi kule ni zao la korosho, mmeshalihujumu, zile *export levy* zimeshapotea, mpaka leo hii hatujui mbolea, pembejeo tunapataje! Hivi mimi watakaponiuliza kwamba bwana eeh! umekaa Dodoma miezi mitatu unachangia bajeti, hivi kama wananchi wa Liwale tumeletewa nini wakulima? Sasa hivi hawana uhakika wa ufuta, yaani bei za ufuta hazijulikani, masoko hayajulikani.

Mheshimiwa Naibu Spika, juzi hapa mmetangaza kwamba zao la ufuta litanunuliwa kwa stakabadhi ghalani, mmewapa Bodi ya Maghala ndiyo washughulikie hilo, lakini mpaka leo hawajaandaa chochote na ufuta sasa hivi ndiyo uko sokoni, kwa hiyo, mipango hii tuanyopanga haiakisi maisha ya wananchi wetu. Tunaposema hii bajeti siyo rafiki

kwa watu wetu tunamaanisha hiyo kwa sababu wengine mipango hii hatunufaiki nayo. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano nakuja kwenye hoja ya kufungamanisha, mnasema kwamba mnaenda kuandaa akaunti moja (*collection account*) kwamba mapato yote ya nchi hii yakusanywe kwenye akaunti moja halafu Serikali au Hazina ndiyo wagawe. Jambo hili siyo sahihi sana pamoja na kwamba nia yenu ilikuwa ni nzuri. Kwa mwenendo wa upelekaji wa fedha za mafungu haya kwenye Halmashauri zetu au kwenye Taasisi husika na hii sasa mnakwenda kuua. Mmeshaiua Halmashauri, tumejua vyanzo vyote vya Halmashauri mmevichukua mkavipeleka Hazina na hamrudishi, sasa hivi mnaenda kuua mifuko, hii mifuko ambayo ilitengewa fedha maalum.

Mheshimiwa Naibu Spika, ndiyo sababu juzi nilikuwa nachangia, Waziri wa Fedha nilikuwa nachangia kwamba Serikali hii ya Awamu ya Tano hatuoni fedha zile ambazo zilikuwa za mafungu maalum zamani kiingereza wanaita, kuna fedha ambazo zilikuwa *ring fenced*, sasa hivi kwenye Awamu ya Tano hizo fedha hazipo tena na sasa hivi ndiyo maana mnaleta hii sera kwamba mnataka kuweka akaunti moja ili muendeleo kuua hiyo mifuko na mnapoua hiyo mifuko maana yake, kwanza mlitakiwa mjiulize kwa nini hii mifuko iliundwa, je, yale mahitaji ya hii mifuko imeondoka? Na kama mahitaji ya hiyo mifuko bado ipo kwa nini sasa mnaiondoa? Kuiondoa hii mifuko maana yake sasa mnakwenda kuua malengo yaliyopangwa kwenye hiyo mifuko. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa kodi ndiyo maana bajeti zetu zinashindwa kutekelezeka, kwa mfano kwenye miradi ya maendeleo hatujawahi kufika asilimia 50 ya utekelezaji wa bajeti yetu. Pamoja na kwamba mmeongeza, walipa kodi wameongezeka mkumbuke kwamba walipakodi wameongezeka lakini kiwango cha kodi kinachokusanywa kinazidi kupungua. Kwa mfano, kwenye *page* ya tano ya kitabu cha Mwenyekiti amesema; tatizo la kupungua kwa shughuli za uwekezaji nchini ndiyo sababu inayosababisha uchumi wetu kudorora wameeleza

kabisa kwamba shughuli za uwekezaji zimepungua. Sababu nyingine wamesema mitaji inahamishwa na hapa tulishawahi kuwaambia kwamba wafanyabiashara kwa mazingira haya mliyowawekea sasa hivi wafanyabiashara wanahamisha mitaji. Wafanyabiashara wanahama, tukiwaambia mnakataa, matokeo yake ndiyo haya kwamba watu mitaji wanahamisha na mazingira ya uwekezaji bado siyo mazuri, kodi zimekuwa nyingi hazielewekina usumbufu vilevile. Kwa hiyo, haya mambo yote haya tunashindwa kuelewa, mipango yetu hii inatupeleka wapi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano kama mnazo hizo mnazoita *Economic Zones*, pesa hampeleki! Halafu *Economic Zone* zingine ambazo tayari watu wamelipwa ili kuacha uwekezaji pale uendelee halafu uwekezaji hakuna, maana yake pale kwanza wamepoteza fedha za kulipa watu fidia halafu hatuna mipango. Hatuna mpango ambao tunaweza kwenda kuutekeleza.

Sasa hii mimi nashindwa kuelewa, hasa mmeshindwaje ninyi kama Serikali kufungamanisha kilimo na viwanda? Msitegemee hizi nyanya ambazo mnazikuta hapo Morogoro, hizi nyanya watu wachache wanaweka pale barabarani ndizo ambazo mnataka kuvijengea viwanda. Hebu fungueni milango watu wawekeze kwenye kilimo, watu wakija kuwekeza kwenye kilimo ndipo mtaweza sasa kuendeleza hivyo viwanda.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nitolee mfano mmoja, jana Spika alisema hapa anashangaa kwa nini bajeti ya Kenya iko juu kuliko ya kwetu, sababu wenzetu wa Kenya wamejiwekeza kwenye kilimo, sisi tumekataa kuwekeza kwenye kilimo. Asilimia 60 ya nafaka inayosindikwa Kenya ni ya kwao wenyewe lakini sisi asilimia 98 ya nafaka inayosindikwa Tanzania ni kutoka nje. Mfano mzuri mimi nilikuwa msindikaji wa nafaka wa aina ya ngano, asilimia 90 ya ngano inayosindikwa Tanzania ni ya kutoka nje, kwa nini? Ardhi tunayo, tena ardhi nzuri lakini hakuna uwekezaji na wala hamfikirii kutafuta wawekezaji kwenye kilimo cha kisasa, kilimo cha kibiashara. (*Makofi*)

*(Hapa kengele ililia kuashiria kumalizika kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa, kengele ya pili ilishagonga. Nilikuwa nasubiri umalizie sentensi, naona unaendelea na kwa mfano mwingine. Ahsante sana.

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Richard Mganga Ndassa, atafuatiwa na Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu, Mheshimiwa David Silinde ajiandae.

**MHE. RICHARD M. NDASSA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa nafasi hii nami niweze kuchangia mapendekezo ya Serikali kuhusu makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka 2018/2019.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kusema kwamba naunga mkono mapendekezo haya ya Serikali kwa asilimia mia moja, lakini nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri pamoja na wafanyakazi wake kwa maandalizi mazuri kwa kweli ya hotuba hii. Nina ushauri ambao ningependa kuutoa, lakini kwa sababu tukienda kwa wenzetu hawa wa *TRA* kwa sababu yote tunayozungumza humu ndani lazima pesa zipatikane, wala siyo vinginevyo, wala sio maneno. Sasa ni namna gani ofisi yako Mheshimiwa Waziri wa Fedha inaweza ikapata hizi shilingi trilion 18 ambazo tumeipa jukumu la kuzitafuta *TRA*. Sasa ni lazima kwanza ile mianya ya upotevu lazima tuijibe. Lakini wafanyakazi wenyewe wa *TRA* ambao wanafanya kazi nzuri sana, sina mashaka na *TRA* wanafanya kazi nzuri sana na ndiyo maana mapato kila mwaka kila mwezi yanaongezeka.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa ni wajibu wetu sasa, Mheshimiwa Waziri hakikisha hakuna shilingi hata moja inayolala nje, pesa ya Serikali hata senti moja inayolala nje,

hakikisha kwamba kila shilingi inayokusanywa lazima iingie ndani.

Mheshimiwa Naibu Spika, tukija kwenye nidhamu ya matumizi ya fedha, yapo matumizi mengine kwa kweli hayafanani, hayafai. Ili tuwe na pesa nyingi za kutosha ni lazima tunapozipokea, tunapozikusanya, lazima tuwe na nidhamu ya kuzitunza na kuzitumia. Ipo miradi mikubwa, naomba kwa sababu tunacho Kitengo chetu cha *TISS* kwenye ile miradi mikubwa ili kwenda kui-*verify* kama kweli hiyo pesa imetumika kama inavyotakiwa. Nashauri Mheshimiwa Waziri wa Fedha watu hawa kwa sababu wapo na kazi yao ni moja ni kuangalia upande wa pili, je, pesa hii imetumika vizuri?

Mheshimiwa Naibu Spika, nimuombe Mheshimiwa Waziri wa Fedha, moja ya eneo ambalo mapato ya Serikali huwezi kuyapima, kuyaona vizuri na eneo hilo kila mwaka tumekuwa tukilalamika na ukiuliza watu wanatupiana mpira ni pale bandarini.

Mheshimiwa Naibu Spika, *floor meter* watakwambia imepona, lakini ukienda kwenye uhalisia Mheshimiwa Waziri wa Fedha eneo lile ni eneo muhimu kweli kweli kama litasimamiwa, kwa sababu mimi nia yangu ni kupata mapato mengi siyo vinginevyo, tupate mapato mengi ili kusudi pesa hizo ziweze kwenda kusaidia mambo mengine huko.

Sasa pale kwenye *floor meter* Mheshimiwa Waziri wa Fedha hebu pelekoni timu pale, *TISS* waingilie kati liko tatizo. Watakwambia wamechelewesha kushusha sijui, kuna *linkage* sijui, kuna *temperature* sijui, maneno matupu yale, liko tatizo kubwa sana pesa nyingi zinapotea pale. Ni lazima tufanye utaratibu Mheshimiwa Waziri wa Fedha, pesa hizi ziweze kukusanywa kama inavyotakiwa. Lakini ili tukusanye kama inavyotakiwa lazima pale watu wa *TISS* waende wakaangalie upya.

Mheshimiwa Naibu Spika, jamb la pili nikushukuru sana Mheshimiwa Waziri wa Fedha, mwaka jana tulileta mapendekezo kwako kuhusu hii michezo ya kubahatisha.



Mwanzo nafikiri hukuwa unanielewa vizuri, kama nilivyosema mimi nia yangu kwa kweli ni kutafuta namna ya kukusaidia wewe kutafuta vyanzo vingine vya mapato. Hata ukipata shilingi mbili, shilingi tatu, shilingi nne, ukiziongezea kwenye zingine ukakusanya huku na huku chungu chako kitajaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru sana Mheshimiwa Waziri wa Fedha mwaka jana ulikubali, na nimeambiwa kwamba kutoka kwenye bilioni 27 ambayo zilikuwa zimekadiriwa mpaka juzi hapa mmeweza kupata shilingi bilioni 64. Sasa kama tukisimamia vizuri na yale mapendekezo niliyokuletea kwa nia njema kabisa wala siyo vinginevyo, nia ni kukusanya lile eneo likisimamiwa vizuri eneo lile utatoka kwenye shilingi bilioni 64, shilingi bilioni 70 utakwenda mpaka kwenye shilingi bilioni 100 au zaidi. Lakini ni lazima hayo mapendekezo uyapitie vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo hili ni *technical* kidogo na mtu anaweza akafikiri kwamba hivi hii *Gaming Board* ni nini, hivi nayo ina hela? Lakini ukienda Marekani, Las Vegas pale wanaishi lile Jimbo ni kwa sababu ya *casino* tu. Kwa hiyo, eneo hili Mheshimiwa Waziri wa Fedha nikuombe sana yale mapendekezo ambayo tumekuletea, uyaainishe vizuri ili yaje kwenye *Finance Bill*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nikuombe tena hapo, michezo hii ili wote tupate kwa maana ya mchezaji, Serikali na Mwekezaji lazima zile asilimia uziweke vizuri. Kwa sababu utakuta kwa mfano, *BIKO*, TatuMzuka na mwingine *Bet* hawako kwenye *Gross Gaming* kwenye *GGR*, sasa kwa nini unawatenganisha wakati wao wote wanafanya mchezo mmoja. Kwa hiyo, nikuombe sana Mheshimiwa Waziri ili tupate pesa nyingi za kutosha na ziende zikafanye kazi kwenye maeneo yetu hili eneo nalo nafikiri ungelitazama vizuri zaidi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nije kwenye suala la mwisho kabla kengele haijalia. Naunga mkono mapendekezo ya Kamati ya Bajeti, lakini mimi hasa kwenye hii *skipper* hii siyo mbaya sana kwa sababu itatupeleka kuzuri. Lakini liko tatizo

hebu litazameni vizuri tusije tukafika pahala Mheshimiwa Waziri wa Fedha tukaanza kuulizana maswali kwa sababu *tender* yake ilitangazwa mwaka 2016, ikagota pahali ikapelekwa kwa AG ndiyo sasa imekuja tena sina tatizo nao, lakini kwa nini ilipelekwa kwa AG, AG alishauri nini lakini uwekezaji wao nani anaujua kweli kama ni shilingi bilioni 44 nani anaujua. Maana yake mtu anaweza akasema mimi niwekeza shilingi bilioni 44 na hapa nikikaa nitakusanya 66 nani anajua kwamba ni kweli uwekezaji wake ni shilingi bilioni 44. Ni jambo jema lakini ni vizuri Mheshimiwa Waziri wa Fedha ukajiridhisha zaidi ili kusudi yasije yakajitokeza kama yale ya *EFDs*.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana Mheshimiwa Waziri wa Fedha, naunga mkono. Huo ndiyo ulikuwa ushauri wangu. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu, atafuatiwa na Mheshimiwa David Ernest Silinde, Mheshimiwa Ibrahim Hassanali Raza ajiandae.

**MHE. MUSSA A. ZUNGU:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote nikushukuru kwa kunipa nafasi, nimshukuru Mheshimiwa Waziri na Naibu wake na wataalam wote wa Wizara kwa kazi nzuri wanayoifanya kwa maslahi ya Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nipongeze mwongozo wa Mheshimiwa Rais kwa kuongoza nchi iwe na mwelekeo wa viwanda, iwe na mwelekeo wa kizalendo kwa watu wote. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ina-*introduce Electronic Tax Stamp (ETS)* ni jambo ambalo zuri sana na ukitizama tumechelewa, lakini uhakika wa *source ya revenue* ya Serikali utapatikana kwa utaratibu wa mfumo huu wa *Electronic Tax System (ETS)*. Lakini nilitaka kujiridhisha tu au Serikali imejiridhisha vipi na huyu aliyepewa kazi hii, *due diligence* ilifanywa na nani? Kwenye semina tumeambiwa

wamefanya Mabalazi, lakini ukitizama taarifa mbalimbali, hii kampuni ina matatizo makubwa. Hii kampuni ina kesi Morocco, wamefanya *price offering* mara kumi zaidi ya nchi zingine walizofanya kazi hii. Kampuni hii inachunguzwa na Bunge la Kenya, kwa *malpractice*. Kampuni hii imeziangusha Serikali zingine kutokana na mfumo wake wa *malpractice* na *corruption*. Sasa Mabalazi hawa waliofanya *due diligence* ya kampuni hii, mimi nitapenda waitwe waje waulizwe taarifa zao walizipata wapi. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, tulifanya semina; TRA na Wabunge na hoja zilizoulizwa na Wabunge kwenye semina Serikali walizi-*defer*, walishindwa kuzijibu. Kutokana na hoja za msingi za kizalendo ambazo Wabunge wameuliza.

Mheshimiwa Naibu Spika, TTCL chombo cha umma, kwa gharama za mradi huu wa bilioni 48, mimi binafsi naomba Serikali i-*revisit* mpango wake wa kuajiri watu wa nje kusimamia makusanyo ya kodi nchini Tanzania. Unaposema *surrender sovereign* ya *tax regime* ya nchi kwa kampuni ambayo tayari ina matatizo makubwa kama haya duniani na *sever* ya kampuni hii ni mali ya *vendor* mwenyewe. Naiomba Serikali tena na nia njema ku-*support* mpango huu wa *ETS*, lakini bado ningeomba shughuli hii ifanywe na TTCL ambacho kina uwezo, chombo cha umma. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, unaposema *information* za *vendor* huyu zitakwenda kwenye *data center*, kuna njia nyingi sana za ku-*under declare traffic* kwenda kwenye *data center* ya Serikali. Kuna *command* nyingi sana za mitandao unaweza uka-*hide information* zingine. Kwa hiyo, mpango huu ni mzuri naunga mkono asilimia 100, lakini naomba Serikali i-*revisit* jambo la ku-*surrender regime* ya *tax* kwa Kampuni ya nje ambayo tayari ina misugvano kwenye nchi nyingi sana. Kwa hiyo, naomba kazihii nzuri, ni muhimu kwa Taifa letu lakini wapewe TTCL.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 2008 tulishauri Serikali kuhusu masuala ya wizi wa *declaration* za *traffic*

kwenye mitandao ya simu. Serikali ikanunua mtambo, walituambia walinunua mwaka 2008 kumbe hawakununua, walimuweka Mwekezaji ambaye kaja na mtambo wake wa gharama za *50 billion* wakaingia mkataba wa miaka 15, *which was very wrong. (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, masuala ya mitandao *server* kama ni mali ya *vendor* utapigwa tu na tumepigwa na tunaendelea kupigwa. Kwa hiyo, hoja yangu tulihoji hata gharama ya mtambo wenyewe na huu mkataba kwenye semina tumeambiwa ni miaka mitano. Miaka mitano mtu anasimamia *sovereign* ya *regime* ya kodi nchini na hakuna popote ambapo tumepewa *comfort* ya *forensic audit* ya mtambo wake atafanya nani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna nchi nyingi wameweka hii *system*, kuna kitu kinaitwa *new generation quickly response*, hoja kubwa ni makusanyo lakini ku-*cub* na kuzuia *elicit goods* katika soko ambalo ni jambo zuri sana. Mitambo hii inayowekwa sasa hivi huu sijui, kwa *new generation* mimi na wewe ukienda dukani unatumia *app* yako ya simu kuweza kuona *stamp* ile na *goods* ambazo ziko mitaani ni *genuine*. Sababu *stamp* za mitaani ambazo siyo *genuine* hazitakosa ku-*have return* ili kuthibitisha unatumia simu yako una-*log* kwenye ile *code* ya *stamp* inakwambia hii ni *genuine* au siyo *genuine*. Sasa tulitaka kujjuliza mtambo huu ambao Serikali wanatuambia walishainigia mkataba unayo *app* kama hii ambayo kujiridhisha mfanyabiashara, *consumer* kuweza kujua hii *stamp* iliyowekwa hapa ni kweli *stamp* ya Serikali na mwananchi wa kawaida anaisaidia Serikali kwa kwenda katika maduka au katika *supermarket* aki-*log in* pale pale na simu yake na yeye anapewa majibu kuwa hii ni *stamp* ya Serikali au ni *stamp* ya mitaani, nilitaka kujua hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, *server* inapokuwa ni mali ya *vendors* rahisi kwa *TRA* au Serikali kujua *under declaration* ya ripoti yoyote ya *vendor*, siyo rahisi. Kwa hiyo, nilikuwa naomba, naunga mkono mpango huu naunga sana *100 percent*. Ombi langu uwekezaji huu ni mdogo sana,

tuiwezeshe *TTCL* ifanye hii kazi siyo chombo kutoka nje.  
(*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, *Bombardier* mpya zinatolewa *Q400 New Generations*, abiria 96 (*96 passengers*) *flies Dar es Salaam - Dodoma* siku zote watu wanakosa nafasi. Huduma nzuri, *performance* nzuri, tukipata *Bombardier Q400 New Generations* ya abiria 96 gharama za uendeshaji zitashuka, tutakuwa na abiria wengi kwenye ndege. Kwa hiyo naomba Waziri wa Fedha hili nalo alitizime, kuweza kununua *New Generation Bombardier Q400* ili tuweze kupunguza gharama za uendeshaji. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nakubaliana na Taarifa ya Kamati ukurasa wa 47 chombo hiki kiendeshwe na mamlaka ya umma ya Tanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Zungu. Mheshimiwa David Ernest Silinde atafuatiwa na Mheshimiwa Ibrahim Hassanali Raza, Mheshimiwa Mendrad Kigola ajiandae.

**MHE. DAVID E. SILINDE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipatia fursa hii na mimi nichangie hotuba ya Waziri wa Fedha na Mipango.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka jana tukiwa ndani ya Bunge lako tukufu kipindi tunapitisha bajeti humu ndani kama hii Bajeti Kuu, nakumbuka makofi yaliyokuwa yanapigwa humu ndani kwamba bajeti hii hajjawahi kutokea yaani haina mfano! Mwaka jana tukajenga hoja tukaonekana sisi kama vile mwaka jana hatueleweki. Sasa mwaka huu siku ya Alhamis wakati Waziri Mpango anawasilisha bajeti yake, nakumbukua maneno ya Spika mwishoni ana-*windup* anasema jamani haya ni mapendekezo ya bajeti, siyo bajeti hajjawahi kutokea ni mapendekezo. Kwa sababu gani, kwa sababu yale yote waliyoyaahidi mwaka

jana *with confidence*, hayajatekelezeka. Kwa kifupi kwa mara ya kwanza ukisoma hotuba yake yaani unaona kabisa ni bajeti ya kukiri kushindwa, bajeti ya kuomba msaada anaomba Simon wa Kirene kwenye bajeti aje ashuke, abebe msalaba wa zege humu ndani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ukisoma ukurasa wa 81 wametajwa viongozi humu ndani, mashuhuri. Alipowataja mimi nilikuwa nawakumbuka ikabidi nirudi tena nisome upya, ili niainishe hawa viongozi waliotajwa kwenye dunia, viongozi mashuhuri na uchumi wetu wa Tanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mtu wa kwanza aliyewekwa Deng Xiaoping, Rais wa Pili wa Jamhuri ya China, wakati anaingia madarakani alisema, *to embrace people to be rich* (kuwafanya wananchi kuwa mtajiri). *To be rich is something to be glorious*, Deng Xiaoping. Haya yapo kwenye hotuba ya Mheshimiwa Mpango haya kayasema, sasa tu-*compare* na kwetu, sisi tunataka watu wetu wawe matajiri? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna kauli tumezisikia wote, tunataka matajiri waishi kama mashetani. Akatajwa Rais wa Pili, Lee Kuan Yew wa Singapore, huyu aliibadilisha Singapore kutoka dunia ya tatu kuwa dunia ya kwanza. Jambo la kwanza baada ya kupata madaraka, alifanya jambo moja, alisema lazima tuhakikishe watu wetu wanapata ajira (*to promote stable employment jobs*) kwa sababu Singapore *unemployment* ilikuwa iko juu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mambo ya msingi ya kujifunza kwa huyu Rais wa Pili wa Korea, moja yeye ali-*promote private sector*, Singapore uchumi wake ni *private sector*. Sisi angalia *private sector* inavyolia leo, inalia siyo kawaida. Nenda kwenye mabenki angalia uchumi wake kule, mabenki yameporomoka, tumekaa na *NBC* wanakwambia imeshuka mpaka faida, *dividend* ya Serikali hakuna. Tumekaa na *NMB*, tumekaa na watu wa *private sector* wanailalamikia Serikali kwamba hatuwekezi kwa *private sector*. Haya aliyasema Rais wa Pili huyu ambaye

amekuwa *compared* hapa, hizi sifa hizi yeye ali-*promote private sector*. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Lee alikuja Tanzania mwaka 1973 pale UDSM, miaka hiyo akina Mheshimiwa Chenge walikuwepo pale, akaja pale na Mwalimu Nyerere akamwambia Mwalimu hii sera yako ya ujamaa na kujitegemea njia hii siyo sawasawa, alizomewa kweli na wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam wakati huo. Alipozomewa akasema mimi nilichokisema ndiyo hiki, hii njia mliyochukua siyo sawasawa. Juzi nikamsikia Katibu Mkuu wako wa chama anasema turudi ujamaa na kujitegemea! Mnakotupeleka siko. Kama unatumia mifano ya watu ambao waliwajali watu wa chini kuinua uchumi halafu *comparison how?* (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, Dkt. Mahathir Mohamed wa Malaysia, unajua kabisa Malaysia imeendelea kwa mfumo wa PPP (*Public Private Partnership*). Haya tueleze sisi *public private*, tunasema reli tutajenga wenyewe, ndege tutanunua wenyewe, *Stieglers' Gorge* tutanunua wenyewe, kwa nini, tutakopa, mwisho wa siku huu mfumo unaotumika sasa uko Tanzania tu. Duniani kote miradi mikubwa Serikali ina *engage* miradi mikubwa ya kiuchumi pamoja na *private sector*, lengo ili gharama zinazobakia, baadhi ya gharama ziende kusaidia wananchi. Sasa mikopo tunayochukua ni ipi, mikopo ya kibiashara na hii mikopo ya kibiashara tunayoichukua unajua *maturity* yake ni ndani ya muda mfupi miezi sita. Nilizungumza wakati wa Wizara ya Fedha kwamba, jambo la reli (*standard gauge*) siyo baya, lakini matokeo yake reli kabla haijaisha tunaanza kulipa mkopo. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, hii nakueleza ukweli, Waziri wa Fedha asipodhibiti Deni la Taifa tunakwisha. Kwa sababu, mwisho wa siku angalia kwenye hotuba yake kwenye ule ukurasa ambao amesainisha ile bajeti yake nafikiri ni kama ukurasa wa 78, soma mapato anayoyapata. Mapato ya Serikali Kuu ya ndani anategemea kupata trilioni 20, lakini kwa miaka yote hawajawahi kuzidi trilioni 14, hapo ni kama

amekusanya asilimia 100. Ukija ukiangalia kwenye matumizi, Deni la Taifa, trilioni 10, mishahara trilioni saba, matumizi mengineyo trilioni tatu, trilioni 20, hayo ni *first and second charge*, jukumu la kwanza na jukumu la pili, wana uhakika wa kukamilisha? Kuna miradi ya maendeleo, hakuna? (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, ndiyo maana ukipitia bajeti nzima mwaka huu trilioni 10 hawajakusanya, miradi ya maendeleo haijafanyika, Halmashauri zina-*suffocate!* Haya tunawaambia kwa nia njema. Sasa unamgusa mtu kama Nelson Mandela amekaa jela miaka 27, mtu wa kwanza, hebu fikiria mtu aliyekufunga ndiyo unamuweka kuwa Makamu wako wa Rais, Frederik Willem de Klerk. Halafu yule aliyekuwa anamtesa Mandela ndiyo alikuwa *bodyguard* wake mpaka anakwenda kabirini, ndiyo alikuwa *Chief bodyguard*, yule gerezani aliyekuwa anamtesa miaka 27, anayemfanyisha Mandela kazi ngumu mpaka akaumwa TB ndio alikuwa *bodyguard* wa Mandela. Niambie wa kwetu angefungwa hata miezi sita ingekuwaje? (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati fulani mnakimbia vitu. Hebu kwa mfano unataka umuige Mandela, tumekuletea hotuba ya kurasa 521 unakimbia hotuba, mtaweza tabia za Mandela? (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, unajua wakati mwingine kama unakimbia maoni halafu unataka kuwa Mandela, hizi ndio tunaita nadharia. Utekelezaji ni tofauti na nadharia. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mwalimu Nyerere huyu sifa zake hazielezeki, ana sifa kweli na mimi ninakiri kwamba Mwalimu Nyerere anapaswa kuwa Mwenye Heri kama Kanisa Katoliki wanavyotaka, kwa sababu gani, aliunganisha Taifa. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, akina Mtei wale wa Kaskazini walikuwa Magavana wake. Watu wale wa Usalama wa Taifa, Mkuu wa Usalama walikuwa ndiyo watu wake



waliokuwa wanamsaidia, akina Ndugu Kombe wale na akina nani, leo huwezi kusema Taifa moja la upande huu, sijui Kaskazini wasubiri, hawa hivi, haiwezekani! (*Makofi*)

*(Hapa kengele ililia kuashiria  
kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MHE. DAVID E. SILINDE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nilipewa dakika 15 na nimeweka *stop watch* hapa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Silinde, nadhani unayo nakala ya Kanuni zako hapo, Kanuni ya 99(12) uchangiaji kwenye bajeti ni dakika 10 siyo 15. Hata ukipewa zile dakika 10 ndiyo unaweza kugawanya kwa watu wawili, Kanuni iko wazi kabisa. Kwa hiyo, huwezi kuwa na dakika 15, malizia sentensi uliyokuwa unazungumza.

**MHE. DAVID E. SILINDE:** Mheshimiwa Naibu Spika, *it is ok*. Sina shida na suala la *ETS*, mkitaka kushughulika nendeni mpaka kwenye simenti, sigara na mafuta, lakini mfano wake wa mwisho wa Park Chung Hee wa South Korea, yule...

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Silinde.  
(*Makofi*)

Tunaendelea na Mheshimiwa Ibrahim Hassanali Raza, atafuatiwa na Mheshimiwa Mendrad Kigola, Mheshimiwa Mahmoud Mgimwa ajiandae.

**MHE. IBRAHIM HASSANALI MOHAMMEDALI RAZA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii. Namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa uwezo na pumzi yake kusimama hapa kuchangia bajeti hii muhimu sana katika nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nianze kwa kumshukuru Mheshimiwa Waziri na Naibu wake, Mheshimiwa Dkt. Ashatu Kijaji, pamoja na timu yake nzima kwa jinsi walivyoandaa hii bajeti ya fedha ambayo itatusukuma

mpaka 2019. Hongereni sana Mheshimiwa Waziri na timu nzima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile niwashukuru wenzetu wa *TRA*. Unajua tunapozungumzia masuala ya bajeti ya Serikali lazima tuwashukuru na wenzetu wa *TRA* namna wanavyohangaika kutafuta mapato ambayo yanatusaidia wananchi. Bila *TRA* kukusanya mapato leo hapa tusingeweza kuzungumzia bajeti hii. Kwa hiyo, nimshukuru sana Kamishna Charles Kichere na timu yake nzima ya *TRA* kwa jinsi wanavyofanya kazi nzuri ya kukusanya mapato. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naweza kusema sasa hivi kwa kiasi fulani *TRA* wamekuwa marafiki sana kwa wafanyabiashara na wameweza angalau kukaa kwenye meza kumaliza yale matatizo ambayo wafanyabiashara wamekuwa wanahangaika nayo. Kwa hiyo, lazima tuwape sifa *TRA* tofauti na miaka ya nyuma hawakujenga mahusiano mazuri na wafanyabiashara lakini sasa hivi wamekuwa wasikivu na wenye nidhamu ila baadhi yao bado siyo waaminifu lakini kwa asilimia kubwa wanafanya kazi nzuri. Nawapongeza sana *TRA*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Rais, Dkt. John Pombe Magufuli kwa sababu bila nguvu zake tusingefika hapa tulipo. Watu ambao wanataka tusimsifu Rais, hivi jamani kwenye Bunge hili tumsifu Uhuru Kenyata au tumsifu Museveni? Sisi tuko hapa kumsifu Rais John Pombe Magufuli, hatuko hapa kuwasifia Marais wa nchi nyingine, huo ndiyo ukweli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kiongozi yeyote anapofanya mazuri usitegemee wapinzani kukusifu sana hiyo ni kawaida. Nchi zote duniani hakuna chama kinachoongoza wananchi halafu wapinzani wakakisifu, si India, Ulaya hata huko Marekani. Kwa hiyo, nimwambie tu Mheshimiwa Rais asivunjike nguvu, aendelee na katika miaka yake miwili na nusu tumeona mambo makubwa aliyofanya Rais Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli kwa kushirikiana na Waziri Mkuu na Mawaziri. Mawaziri wa Awamu hii ya Tano

wamekuwa ni Mawaziri ambao wanafanya kazi usiku na mchana, kwa hiyo, niipongeze Serikali nzima ya Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nizungumzie bajeti hii. Kwanza niipongeze Wizara kwa kuondoa VAT katika masuala haya ya taulo kwa sababu kweli yatawasaidia akina mama na wanafunzi kwa kiasi kikubwa sana, nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuzungumzia kuongezea ushuru baadhi ya bidhaa kwa nia ya kuvilinda viwanda vya ndani. Kwa kweli, tulikuwa tunawafanyia biashara kubwa wenzetu wa nchi jirani, wao wanatuletea hapa sisi tunafanya manunuzi tu, tunawachumia wao, ajira zinakwenda nchi za jirani, nchini kwetu viwanda vinaumia na wafanyakazi wakati mwingine wanapunguzwa. Katika kuongeza Ushuru wa Bidhaa katika bidhaa mbalimbali hatua hiyo itavilinda viwanda vyetu vya ndani. Namshukuru sana Mheshimiwa Waziri na timu yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nikija katika masuala ya nguo zetu za mitumba, naomba Wizara hii iangalie kwa jicho la huruma hizi nguo za mitumba kwa sababu huwa zinatumiwa na wananchi wa hali ya chini kabisa Tanzania hii. Nguo za mitumba zinauzwa rahisi, kila mmoja wetu anajua zinakwenda mpaka vijijini na mikoani. Sasa hivi *container* moja la mitumba linatozwa shilingi milioni 40. Naomba tu Wizara, kama kuna uwezekano wa kupunguza angalau kidogo tukawapa nguvu hawa wananchi wa chini ambao hawawezi wakanunua shati la Sh.40,000 au Sh.50,000 wajipatie mashati hayo kwa bei rahisi na hii itatusaidia kujenga uhusiano mzuri na watu wa chini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile niombe Waziri aangalie sana sekta ya kilimo kwa sababu ni sekta moja muhimu sana katika nchi yetu ya Tanzania na asilimia 70 ya Watanzania wanategemea kilimo. Kwa hiyo, namwomba sana wakulima wawezeshwe, wapatiwe mikopo, wapewe

*initiative* ambayo itawasaidia kuwekeza katika kilimo. Kilimo kikiwa kizuri Tanzania tutapata *foreign exchange*. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, nchini India wanategemea sana *agriculture*, wana-*export* kwa hali ya juu. Serikali ya India inapata pesa nyingi sana katika kwa ku-*export* bidhaa za *agriculture*. Hata wenzetu wa Thailand kwa kiasi kikubwa cha fedha wanategemea *export* ya *agriculture*. Kwa hiyo, siyo vibaya nasi tukaipa umuhimu sana sekta hii ya kilimo ambayo kwa kiasi fulani itatusaidia kupata *foreign exchange* kwa sababu, njia kubwa ya kupata *foreign exchange* ni kuuza mazao yetu nje. Sisi Tanzania Mungu ametupa ardhi kubwa sana ambayo mimi naweza kusema asilimia kama 40 hazijatumika, bado tunayo ardhi ya kuwekeza katika kilimo. Tukikipa umuhimu kilimo basi Serikali yetu itapata *foreign exchange*. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna kasoro kidogo imejitokeza, wafanyabiashara wengi Dar-es-Salaam hawana mashine za *EFD*, wanatumia *receipt book*. Serikali inakosa mapato, *TRA* inakosa mapato na naona hawawatendei haki wafanyabiashara wengine wanaotumia mashine za *EFD*. Kwa hiyo, naomba *TRA* kupitia Wizara yako ihakikishe katika kipindi cha miezi miwili kila mfanyabiashara anatumia mashine ya *EFD*.

(Hapa kengele ililia kuashiria  
kwisha kwa muda wa mzungumzaji)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa, muda wako umekwisha.

**MHE. IBRAHIM HASSANALI RAZA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono asilimia 110. Ahsante sana. (Makofi)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Tunaendelea na Mheshimiwa Mendrad Kigola, atafuatiwa na Mheshimiwa Mahmoud Mгимwa na Mheshimiwa Murad Saddiq ajiandae.

**MHE. MENDRAD L. KIGOLA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nashukuru sana kwa kunipa nafasi hii na mimi niweze kutoa mchango wangu kwenye mapendekezo ya Serikali. Nianze na kuipongeza Serikali kwa kuleta mapendekezo ambayo yanalenga sisi Wabunge tutoe mapendekezo yetu ili bajeti itoke vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna maeneo mengine Serikali imefanya vizuri sana, kwa mfano, ku-*promote* viwanda vya ndani na ili uweze ku-*promote* viwanda vya ndani lazima uhibitie bidhaa zinazotoka nje. Kwa hiyo, kupunguza kodi kwenye baadhi ya bidhaa ambazo tunaweza tukazalisha sisi wenyewe ni mpango mzuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimeona hata kwenye mafuta ambayo tunaweza tukazalisha, tunalima alizeti na tuna viwanda vya alizeti, ili ku-*promote* hivi viwanda vifanye kazi vizuri wamepandisha kodi kwenye mafuta yanayotoka nje, hiyo ni sawa, lakini lazima tuhakikishe tunapata soko la uhakika la ndani ili wazalishaji wafanye vizuri. Kwa hiyo, hilo na mimi nakubaliana nalo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, halafu la pili ni bajeti. Bajeti ya mwaka huu 2018/2019 tumeenda na shilingi trilioni 32.5 mwaka jana tulikuwa na shilingi trilioni 31.6. Kuongezeka kwa bajeti ni kitu kizuri sana kwa sababu inalingana na mahitaji ambayo tunayo. Hatuwezi kusema mahitaji ya mwaka jana ni sawa na mahitaji ya mwaka huu. Kila mwaka mahitaji yanaongezeka na bajeti inaongezeka, huo ni mtizamo nzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, mikakati ya Serikali kukusanya mapato siyo mibaya isipokuwa kwa sababu tumesema tunataka ku-*promote* vitu ambavyo tuna uwezo wa kufanya wenyewe ni jambo zuri sana. Kwenye ukusanyaji kwa mfano kuna *Electronic Stamping Tax System*, kama alivyoongea Mheshimiwa Zungu ni *system* nzuri sana kwa ajili ya kuongeza mapato ndani ya nchi yetu. Hapo naunga

mkono kwa mtazamo wa kudhibiti mianya ya ukwepaji kodi ni suala zuri sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kuna *issue* ambayo Wabunge wengi tunajuliza, hivi hatuna wataalam pale *TRA*, vijana wetu ambao wanasoma vyuo vikuu nje wakashindwa kusoma hii *system*, tukaidhibiti wenyewe, tukaanzisha ndani ya nchi na tukaitumia kukusanya, kwa hiyo, tumeshindwa kabisa? Kwa sababu unapofanya *investment* ukiona anaweza aka-*recover within one year*, atapata faida kubwa sana. Kwa mfano, yeye atawekeza kwa thamani ya shilingi bilioni 48 lakini katika hesabu za haraka haraka wamefanya *analysis* kwa mwaka mmoja anaweza akapata shilingi bilioni 66, tofauti yake ni shilingi bilioni 18 ambayo yote inaenda nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikawa ninajuliza kama kuna zaidi ya shilingi bilioni 18 ndani ya mwaka mmoja, *recovery ya costs* ikafanyika mwaka mmoja, kwa nini tusingesomesha vijana tukachukua hata shilingi bilioni 5 wakaenda kusoma nje wakarudi wakafanya kazi *TRA* wakakusanya kodi? Hili ni suala la kujuliza sana. Hivi kuna umuhimu gani kuchukua makampuni ya nje waje wakusanye fedha yetu halafu wapeleke pale, sisi tukawa tumeshindwa. Mwaka wa pili kuna- *possibility* ya shilingi bilioni 66 zikaenda nje. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nakumbuka siku moja tulifanya semina hapa, vijana wetu *MaxMalipo* vijana wetu wasomi wa hapa hapa Tanzania siku ile Wabunge tuliwapigia makofi sana pale ukumbuni wali-*present issue* za kukusanya kodi na wakasema kwamba wako *worldwide* sasa hivi. Hawa vijana wa *MaxMalipo* wameshindwa kufanya utafiti wa kukusanya kodi? Labda tuwaite, tuwaulize itakuwaje wameshindwa kufanya makusanyo ya humu ndani na wakienda kwenye nchi nyingine wanafanya vizuri na kusifiwa, lazima tuangalie sana. Halafu ule mkataba tumeweka mrefu sana ni mpaka miaka mitano. Tungeweka labda hata miaka

mmoja au miwili ili tuangalie matazamia lakini miaka mitano, nadhani hii lazima iangaliwe vizuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ya Bajeti tumependekeza vizuri sana, tumesema *system* siyo mbaya ni nzuri nia ni kudhibiti na tunataka tudhibiti hata uzalishaji wa maji. Tunajua maji ni muhimu, tulikuwa tunafikiria kufanya *exemption* kwenye *product* za maji ili watu waweze kupata maji, watumie maji safi na salama. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa naongea na Ndugu yangu hapa Mheshimiwa Charles Kitwanga, yeye alishafanya kazi Benki Kuu na utalamu wa masuala ya *electronics*, nikamuuliza hivi wewe kama Mbunge mtaalam umeshindwaje ku-*advise* tuangalie hii *system*, kweli nime-*challenge* hapa. Amefanya kazi *BoT* karibu miaka kumi na *system* ya *tax collection* anajua. Ameshindwa kunijibu vizuri lakini naendelea kumuuliza lazima Wabunge wataalam watusaidie katika *collection* ya *tax* katika nchi hii na tunataka *tax revenue* iwe juu. Ndiyo maana kuna Wabunge wanachaguliwa wataalam. Kwa hiyo, nimeona hili suala ni la msingi sana nilielezee hapa ili siku nyingine tusianze kulalamika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine nataka niipongeze Serikali kwenye mgao wa fedha hasa ile ya vijana na wanawake. *Point* ambayo nimeipenda pale, ile asilimia 5 kwa vijana na asilimia 5 kwa akina mama Serikali imesema hakuna *interest*, cha msingi ni usimamizi mzuri, hilo ni jambo zuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ambalo ni *challenge* hasa Wizara ya Fedha, ule Mfuko Mkuu fedha yote mtakusanya kutoka Halmashauri, kutoka Serikali za Mitaa, na sehemu zote mtakusanya pale, halafu Halmashauri ikitaka kutumia itaomba kufuatana na mahitaji. *Challenge* ambayo ipo pale urudishwaji wa fedha unachukua muda mrefu sana. Lazima tuwe makini, Wizara ya Fedha lazima iwe *active*

katika kurudisha fedha Halmashauri. Tunaweza tukawa tuna *system* nzuri ya kuweka kwenye akaunti moja lakini Halmashauri inaweza ikatuma maombi ya kupewa fedha ili watumie mkachelewesha. Hili lazima tutoe angalizo kwa Serikali, kwamba kama Halmashauri zimeeomba fedha *on time* basi wapewe fedha *on time*. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Halmashauri yangu ya Wilaya ya Mufindi kuna fedha ya maji na Waziri wa Maji aliahidi kwamba mwezi Mei angeweza kuipeleka ile fedha. Wameomba kuanzia Machi tunaenda Julai ile fedha hawajapewa mpaka leo. Ni mradi wa maji mmoja tu. Sasa najiuliza kama mradi mmoja Mkurugenzi wa Halmashauri akishirikiana na *Engineer* ameandika *request*, vigezo vyote viko pale, tena ni shilingi milioni 270 mpaka leo Juni mradi wa maji kule umesimama Kata ya Mtwango wananchi hawana maji. Kupeleka shilingi milioni 200 ni kazi ya siku moja tu, mimi nikikaa kwenye komputa *just a minute* nimeshapeleka *transfer* ya hela zile, lakini mpaka leo hazijapelekwa. Je, tukisema wapeleke shilingi trilioni kadhaa kwenye Halmashauri itachukua muda gani? Hii ni bajeti ya mwaka mmoja mmoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano, sasa hivi Wizara ya Fedha ina shilingi trilioni 12 ambazo nyingi ni miradi zinapitia pale. Naomba Serikali, *system* ni nzuri ndiyo maana naiunga mkono, lakini utendaji kazi lazima tuongeze juhudi, lazima tuende na muda. Bahati mbaya sana sisi huwa hatujali muda.

*(Hapa kengele illia kuashiria  
kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa, kengele mbili zimeshagonga.

**MHE. MENDRAD L. KIGOLA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana.



**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Tunaendelea na Mheshimiwa Mahmoud Mgimwa atafuatiwa na Mheshimiwa Murad Saddiq na Mheshimiwa Lucy Magereli ajiandae.

**MHE. MAHMOUD H. MGIMWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichukue fursa hii kwa kumpongeza ndugu yangu Mheshimiwa Dkt. Mpango pamoja na dada yangu Mheshimiwa Dkt. Ashatu. Kwa namna ya kipekee, nimpongeze sana Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli kwa kazi nzuri na ya kizalendo anayoifanya katika nchi yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nimwambie Ndugu yangu Mheshimiwa Silinde namheshimu na najua wakati mwingine anachangia vizuri, lakini kuna watu katika nchi zingine wanampongeza Mheshimiwa Dkt. Magufuli anafanya vizuri. Profesa Patrick Lumumba mpaka amebandika jina na kumuita *Magufulification* kutokana na *performance* yake. Kuna watu wanataka kujifunza *the way* Mheshimiwa Dkt. Magufuli anavyofanya kazi nzuri katika nchi ya Tanzania. Kwa hiyo, mnyonge mnyongeni lakini kuna maeneo tunafanya vizuri. Katika nchi za Afrika Mashariki na Kati hata wenzetu wa Kenya wanatamani Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli awe Rais wao. Ameweza kusimamia matumizi ya pesa kwa nidhamu na kuna baadhi ya mambo makubwa ambayo tumeweza kuyafanya kwa hela yetu hiyo ya ndani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hii ni rasimu ya bajeti na siyo bajeti. Sisi Wabunge ni wajibu wetu kuikosoa na kuielekeza Serikali kwenye maeneo ambayo tunaona kuna upungufu. Kwa hiyo, tukikataa kabisa kwamba hakuna jambo la maana lililofanywa kwenye hii rasimu ya bajeti tutakuwa tunakosea. Yapo mambo mazuri Mheshimiwa Dkt. Mpango amekuja nayo nasi lazima tuyaunge mkono.

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi ni viongozi wa wananchi, tumetoka kwenye Majimbo yetu, pamoja na uzuri wa rasimu hii ya bajeti lakini kuna maeneo Mheshimiwa Dkt. Mpango alitakwa ayaangalie kwa ukaribu sana kwa sababu yanawagusa watu *direct*. Kwa mfano, eneo la kilimo linaajiri Watanzania wasiopungua asilimia 66.6 na yeye anajua, lakini ukiangalia bajeti iliyokwenda kwenye eneo hili hairidhishi kabisa. Tunaomba aliangalie maana tulitakiwa tuweke bajeti ya kutosha kwa sababu kwenye eneo hili kuna ajira, kuna usalama wa chakula, kuna malighafi ya viwanda ambapo tunataka twende kwenye uchumi wa viwanda. Sasa tusipowekeza vizuri kwenye eneo la kilimo tunategemea nini, tutaendaje kwenye uchumi wa viwanda? Kwa hiyo, namwomba sana Mheshimiwa Dkt. Mpango tuliangalie mara mbili eneo hili la kilimo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia wenzetu ambao tumesoma bajeti pamoja nchi za Afrika Mashariki na Kati, asilimia 10 ya bajeti nzima ndiyo wametenga kwenye bajeti ya kilimo, lakini bajeti yetu haifiki hata asilimia 3. Sasa tujiangalietutafika huko. Shilingi bilioni 170 *against* shilingi trilioni 32 wapi na wapi? Tutakwenda kwenye uchumi wa viwanda kweli? Kwa hiyo, Mheshimiwa Dkt. Mpango naomba sana eneo hilo tuliangalie. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ni Benki ya Maendeleo ya Kilimo ambayo anaiongoza mwenyewe. Wale watu wa Benki ya Maendeleo ya Kilimo hawapeleki hela kwa wakulima. Walianza na mtaji wa shilingi bilioni 60, ukakua ukafika shilingi bilioni 67, wakakopa mpaka wakafika shilingi bilioni 287, lakini tujjulize kwenye shilingi bilioni 287 ni kiasi gani wamewakopesha wakulima? Utakuta hela zile wanazokopa na wenyewe wanaenda kuweka dhamana kwenye mabanki mengine, ndiyo madhumuni ya kufungwa hiyo benki? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, Mheshimiwa Dkt. Mpango kwenye jambo hili nataka awaambie tumeanzisha Benki ya Maendeleo ya Kilimo kwa ajili ya kuwasaidia

wakulima siyo kwa ajili kufanya biashara. Wafanye yale ambayo tumekubaliana katika uanzishaji wa Benki hii ya Kilimo, kwenye jambo hili hatuko sawa. Mahitaji ya Watanzania kwenye eneo hili ni shilingi bilioni 800 lakini hata shilingi bilioni 287 zingekuwa zinakwenda *direct* kwa wakulima sasa hivi wakulima wangukuwa wamebadilika kwenye eneo hili. Kwa hiyo, naomba eneo hili tuliangalie sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine ambalo amelizungumzia ni suala la Bodi ya Mazao Mchanganyiko, amesema wanataka kuunganisha Bodi. Mheshimiwa Dkt. Mpango, hawa wananchi ndiyo wanatengeneza hela zao pale, mnataka mfanye nini pale, *interest* yenu ni ipi? Kama kuna watu wana ubadhirifu wa hela si wapelekwe Mahakamani. Wamelalamika kwenye maeneo ya korosho lakini hakuna hata mtu mmoja mpaka leo amepolekwa mahakamani.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, sikubaliani na hoja ya kutaka kuunganisha Bodi, kwenye eneo hili siwezi kukubaliana hata kidogo. Mkitaka kwenda vizuri kwenye eneo hili angalieni Bodi za Udhubiti (*Regulatory Board*) zina tozo mbalimbali ambazo hazina tija na tozo hizo zinawagandamiza sana wakulima na kuwaongezea gharama. Kwa hiyo, naomba tuangalie sana kwenye maeneo hayo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, watu wana shida ya maji na Wabunge wote tulikuwa tunasema hapa tunataka maji na mpaka tukasema tuko tayari kuwashawishi watu wetu kuongeza tozo la shilingi hamsini, lakini hakuna *respondyoyote* tuliyopata. Mwaka jana *collection* ya ndani iliyokuwa inatakiwa iende kwenye maji ilikuwa shilingi bilioni 250 lakini mpaka tunakuja kwenye bajeti ni shilingi bilioni 26 tu ambayo ni asilima 11 ya *collection* ya ndani ambayo ilikwenda kwenye maji. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye bajeti ambayo ilikuwa inatokana na Mfuko wa Maji ya shilingi bilioni 158 hela zote karibu zimekwenda kwenye miradi ya maji. Kwa hiyo, tukiongeza kwenye eneo hili tutafika mbali. Sasa Waziri hajakubaliana na shilingi hamsini angesema basi niwafikirie hawa Wabunge hata niwape shilingi thelathini au shilingi ishirini, akituacha hivi anatuacha solemba. Kazi ya Wabunge ni kuishauri na kuisimamia Serikali, lakini inawezekana ikawa kila siku tunashauri hakuna hata siku moja mmewahi kuchukua mawazo ya Wabunge mkaamua kuyafanyia kazi. Kwa hiyo, tunaomba eneo hili mliangalie. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine Mheshimiwa Dkt. Mpango amezungumza vizuri sana kuhusu kusamehe kodi kwenye chakula cha mifugo, yuko sahihi. Kama unasamehe kodi kwenye chakula cha mifugo halafu unatoza kodi kwenye mashudu umesamehe wapi sasa hapo? Unasamehe kushoto kulia unachukua hela ya wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, sikubaliani na hiyo hoja, hujasamehe hapo. Umetuvisha blanketi hapo, kwamba nimesamehe kodi kwenye chakula cha mifugo halafu unasema mashudu yatozwe VAT, haiwezekani. Kama tumeamua kusamehe kodi, iwe ni kwenye maeneo yote ili kusudi tupate tija kwenye eneo la kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine ambalo napenda kuchangia ni suala la viwanda vya maziwa na nyama. Mheshimiwa Waziri yuko sahihi, ameamua kuvilinda viwanda vya ndani kwa kuongeza kodi ya mazao ya mifugo kwa maana ya mazao ya nyama na maziwa yanayotoka nje ya nchi, lakini tunavisaidiaje viwanda vya ndani hapa. Namwomba ili kusudi twende kwenye ushindani halali, maana sasa hivi maziwa yetu ukilinganisha na maziwa ya Kenya na yanayotoka Uganda maziwa ya Tanzania gharama zaidi.

*(Hapa kengele ililia kuashiria  
kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mahmoud, kengele ya pili imegonga, malizia hiyo sentensi.

**MHE. MAHMOUD H. MGIMWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru, naunga mkono hoja. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Tunaendelea na Mheshimiwa Murad Saddiq atafuatiwa na Lucy Magereli na Mheshimiwa Rose Kamili ajiandae.

**MHE. SULEIMAN A. SADDIQ:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nikushukuru sana asubuhi ya leo na mimi kunipatia nafasi niweze kuchangia mawili, matatu katika bajeti hii ya Tanzania kwa mwaka 2018/2019. Naomba niseme naunga mkono hoja asilimia mia kwa mia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nianze kwa kusema, sasa hivi tuna kaulimbiu ya Tanzania ya Viwanda. Katika kauli mbiu hii naomba nimpongeze sana Mheshimiwa Rais anaisimamia kauli yake hii kwa vitendo. Sisi kama Kamati ya Viwanda na Biashara tulipata changamoto mbalimbali za wadau katika maeneo mbalimbali. Katika bajeti ya mwaka huu, naomba nimpongeze sana Waziri wa Fedha changamoto nyingi zimefanyiwa kazi na Serikali, zimefanyiwa kazi na *TRA* kwa maana hiyo Rais wetu anatekeleza kwa vitendo kauli yake ya Tanzania ya Viwanda. Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na *TRA* wote nawapongeza sana kwamba sasa tunakwenda vizuri sana katika eneo hili la Tanzania ya Viwanda. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naanza na suala hili la *electronic stamp*. Naunga mkono hoja, sina matatizo kwani mapato yataongezeka, uhakiki wa uzalishaji utafanyika lakini wasiwasi wangu ni eneo moja la gharama. Kampuni ambayo mnaingia nayo ubia *TRA* na Serikali kuna viwango wameeleza, kuna dola 6, 10 na 13. Unapozungumzia dola 6 unazungumzia *soft drinks*, unapozungumzia dola 10 unazungumzia *alcohol*, unapozungumzia dola 13 unazungumzia *spirit*, sigara na vitu vingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi yetu haina *coins* ya Sh.10, 20 au 30, tuna *coins* ya Sh.50 na 100 ambazo nazo ni chache sana. Mimi ni mdau nina *Super Market*, tuna shida kubwa sana ya *coins* ya Sh.100 na 200. Leo tunaposema dola 6, huyu bwana atanunua *stamp* Sh.1,000 atazalisha chupa 1,000, ina maana kila chupa moja imepanda Sh.13. Soda leo inauzwa Sh.500 kwa kutumia utaratibu wa *electronic stamp*, anatakiwa auze Sh.513, tunapata wapi *coins* Sh.13? Maana yake ni kwamba wafanyabiashara watauzwa Sh.550, ile *stamp* sasa itatoka Sh.13 ya ukweli itakwenda kwenye Sh.50. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye bia wanasema dola 10 sawasawa na Sh.23. Hatuna *coins* ya Sh.23, atatoka kwenye Sh.23 ataenda kwenye Sh.50 kwa maana *stamp* sasa pale ni Sh.50. Naomba *TRA* na Serikali mlifanyie kazi hili, gharama ziko juu. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi naomba kidogo niulize swali, je, wakati mna-*bargain* na hii kampuni, mliwaeleza ukweli wa uzalishaji wa *volume* za chupa Tanzania? Leo tunazalisha chupa zaidi ya bilioni 10 za soda, juisi, bia na vinywaji mbalimbali, viwanda vimekuwa vingi. Unapofanya biashara na mtu unatakiwa ufanye *bargain, volume* ya bilioni 10 chupa si *volume* ndogo. Kama ni dola 6 lazima wapunguze wafanye dola 2 au 3, *volume* ni kubwa sana ya hizi chupa.

Mheshimiwa Naibu Spika, je, *TRA* walikwenda na *volume* halisi? Walifanya uhakiki kwenye viwanda? Mbona wenye viwanda wanasema hawajafanya uhakiki huo au uhakiki wanatumia uwakilishi wa *return* zao kwenye *TRA*? Kama wanatumia uwakilishi wa *return* za *TRA* bado liko tatizo. Kwa sababu kuna viwanda vinazalisha lakini hawapeleki *return* za ukweli *TRA*, wanadanganya na Kamati tuliwashauri wafanyabiashara wawe wakweli. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, mimi kwenye upande wa *ETS (Electronic Tax Stamp)* sina tatizo. Tatizo langu

hizo gharama ambazo zipo mwisho zitamwangukia mlaji, Tanzania hatuna *coins* hesabu zake tutazifanyaje? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, upande wa mashine za *EFD* tumeanza kupata matatizo. Mwezi mmoja nyuma *server* iliharibika, wafanyabiashara siku nne, tano tulishindwa kupelekea *returns reports* zetu matokeo yake mapato kidogo yalipungua. Hata leo napozungumza mimi hapa bado ile *server* haijakaa sawa, *EFD* bado inasumbua. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri wa Fedha amefanya juhudi kubwa, mimi na Mheshimiwa Ndassa tulimwona na tulimpa na ushahidi na tunawasifu sana na Naibu Waziri walifanya kazi kubwa lakini bado *server* ya *EFD* haijatengemaa, je, imehujumiwa? Leo Mheshimiwa Waziri ameondoa kodi ya *EFD*, je, *server* iko sawasawa? Kama kwenye *EFD* mashine ndogo hizi tunachemka, je, kwenye *electronic stamp* tutakuwa na hali gani? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi ushauri wangu tuangalie upande wa gharama. Naunga mkono, itaongeza mapato, itafanya uhakiki, hatutaibiwa lakini tunali-*handle* vipi? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niende kwenye eneo la pili la *industrial sugar*. Sisi Kamati yetu ya Viwanda tulipata malalamiko mengi kuhusu *refund* ya *VAT* na ile ya 15%. Wafanyabiashara ambao ni *Big Five*: CocaCola Kwanza Pepsi, Azam, Nyanza *Bottlers* na *Bonite* wanaidai Serikali zaidi ya shilingi bilioni 35. Fedha hizi ni mitaji yao ya ndani, hawajapata ile *return* yao ya 15%. Kamati imewashauri waendeleo kuvumilia, Serikali inalifanyia kazi suala lao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri wangu katika eneo hilo, nia ya Serikali ya kudhibiti watu ambao si waaminifu ni njema, ndiyo maana tunawatoza 15% . Sasa tubadilike, badala ya kutoza 15% tuweke *penalt*, faini ambazo zitasababisha Serikali kupata mapato ya moja kwa moja. Hizi fedha si zetu ni zao, tunatakiwa tufanye *refund*. Tuweke

*audit team* maalum, kila miezi mitatu iende kwenye viwanda hivi ihakiki *Industry sugar* imetumika kiasi gani, *industry sugar* ambayo haikutumika viwandani, wapigwe faini na *penalt* na ikiwekana wakirudia makosa wafutiwe leseni. Kwa utaratibu huu wa kuchukua *refund* zao tunawanyima mitaji yao. Leo mitaji mingi imelala Serikalini na wanalalamika sana. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, niingie eneo la kilimo (*agri-business*), nazungumzia kilimo cha biashara. Tanzania tuna eneo kubwa na ardhi nzuri sana, maji ni mengi lakini bado Serikali haijawapanga wananchi na wakulima wake waingie kwenye *agri-business*. Leo nenda Dubai wana kila aina ya matunda duniani lakini wale *supplier* wanafanya *packaging* nzuri, wanaweka matunda yao katika hali ya usafi wanafanya *export*. Matunda ya Dubai yanatoka Malaysia, Indonesia, India na Vietnam. Embe linatoka maeneo ambayo maembe ya Tanzania ni mazuri zaidi. Twende kwenye *agri-business* tuwahamasishe watu wetu ili tusonge mbele zaidi. Katika maeneo ambayo yana ardhi nzuri, rutuba nzuri, mfano Mikoa wa Mbeya na Morogoro, tuna maeneo mazuri ya Mpunga, kwa nini Serikali isihamasishe watu wawekeze kwenye maeneo hayo?

(Hapa kengele ililia kuashiria  
kwisha kwa muda wa mzungumzaji)

**MHE. SULEIMAN A. SADDIQ:** Mheshimiwa Naibu Spika, najua ni kengele ya kwanza.

**WABUNGE FULANI:** Ya pili.

**MHE. SULEIMAN A. SADDIQ:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimalizie kwa kusema naunga mkono hoja, yangu mengine yote nitayaandika kwa maandishi. Ahsante sana. (Makofi)



**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Tunaendelea na Mheshimiwa Lucy Magereli, atafuatiwa na Mheshimiwa Conchesta Rwamlaza, Mheshimiwa Fakharia Shomar Khamis ajiandae.

**MHE. LUCY S. MAGERELI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru nami kupata fursa kuchangia Bajeti Kuu ya Serikali mwaka 2018/2019. Nianze tu kwa maelezo ya awali ambayo ningetaka niyaweke katika utaratibu ambao tumeutumia wakati wote kama Wabunge wa Kambi ya Upinzani, kama Kamati za Bunge tunapokuwa tunatekeleza majukumu yetu ya kuishauri Serikali, kama wadau wa maendeleo ya nchi hii tunapotaka kutoa ushauri wetu kwa Serikali na pia kwa wananchi wetu ambao ndio picha halisi ya kazi ambayo inafanywa na Serikali ya Chama cha Mapinduzi na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Biblia, Kitabu cha Yeremia 33:3, neno linasema hivi:-

*“Niite nami nitakuitikia na nitakuonesha mambo makuu, magumu usiyoyajua.” (Makofi)*

**WABUNGE FULANI:** Ameen.

**MHE. LUCY S. MAGERELI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na maelezo yangu ya awali kwamba kama Wabunge, kama Kamati, kama wadau wa maendeleo tumekuwa tukiishauri Serikali hii lakini bado imeendelea kutuletea mipango ambayo ni *copy and paste*, yenye mambo yale yale ambayo hayatekelezeki, basi nimefikiri labda *we need God's intervation*. Labda tusali sasa, kwa sababu kwa maneno tu kwa kusema kwa kuandika, kwa kuhubiri tumesema sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nilitamani nikuletee memo kwenye Kiti chako nikuombe labda leo Bunge hili tulibadilishe liwe nyumba ya lbada halafu niongoze maombi, halafu na Wabunge wanijibu kwa kusema twakuomba utusikie. Kwa

sababu sijaomba, basi naomba tu muwe wasikivu, mnisikilize niombe.

Mwenyezi Mungu nakuomba uwakumbushe Serikali ya CCM kwamba wananchi wanataka huduma za maji, afya, elimu bora na sio ndege ambazo hawatozipanda mpaka wanakufa. *(Makofi)*

Mwenyezi Mungu nakuomba uwakumbushe Serikali ya CCM waache kutuletea mipango ya maendeleo hewa. *(Makofi)*

Mwenyezi Mungu ninakuomba uwakubushe Serikali ya CCM kwamba wananchi wa Simanjiro walihitaji maji kwa sababu sasa hivi wanakunywa maji katika bwawa moja na ng'ombe, hawakutaka ukuta Mungu wakumbushe hilo.

Mwenyezi Mungu naomba uwasaidie kuwakumbusha Serikali ya CCM...

## T A A R I F A

**MHE. MARTHA J. UMBULLA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kumpa taarifa Mheshimiwa Mbunge.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Magereli pamoja na kwamba unasali naona kuna Mbunge anataka kukupa taarifa hapo. Kwa hiyo, unajua Mungu ni msikivu sana kwa hiyo usitie shaka. Mheshimiwa Martha Umbulla.

**MHE. MARTHA J. UMBULLA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kumpa taarifa mzungumzaji aliyezungumza hivi punde kwamba wananchi wa Simanjiro hususan Mererani waliojengewa ukuta Mheshimiwa Rais huyohuyo amewaletea mradi mkubwa wa shilingi milioni 780 na umeanza kazi na sasa hivi wananchi wale karibia wanaachana na tatizo la maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilitaka kumpa taarifa hiyo. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Magereli, kabla sijakuuliza kama unaikubali taarifa hiyo, naona wanakwaya wanatoka kwenda kujiandaa kabisa kwa ajili ya maombi. Kwa hiyo, naamini yule Nabii aliyekuwepo hapo *basement* leo, atatupata Wabunge wote hapa tuungane jamani na Mheshimiwa Magereli twende kwenye maombi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Magereli, unaipokea taarifa ya Mheshimiwa Martha Umbulla?

**MHE. LUCY S. MAGERELI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nimemsikia Mheshimiwa Umbulla lakini mambo haya huwa ni maneno yanayosemwa tu, ni tarakimu zinazotajwa tu. Hata bajeti zimekuwa zikitajwa kwa tarakimu hivyo hivyo mwisho wa siku asilimia moja, mbili, kumi na moja, tunangoja kuona hilo la Simanjiro litachukua muda gani.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niendelee na maombi yangu. (*Kicheko*)

Mwenyezi Mungu nakuomba uwaambie Serikali ya CCM ya kwamba uchumi wanaouhubiri unakua kwa kasi wao peke yao ndiyo wanaouona, wananchi wetu hawauoni na sisi Wabunge pia hatuuoni. (*Makofi*)

## T A A R I F A

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Magereli, naomba usubiri, kuna *Chief Whip* amesimama hapa.

**MHE. CHARLES M. KITWANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kitwanga, *Chief Whip* amesimama.

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Sina nia ya kukataa kwamba Mwenyezi Mungu hatumheshimu, lakini ni vema akakuelekeza wewe kwa sababu kwa mujibu wa taratibu zetu humu si sawa kutumia nafasi ya Mwenyezi Mungu katika sura kama hiyo.

*(Hapa baadhi ya Waheshimiwa Wabunge waliongea bila mpangilio)*

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, namwomba mzungumzaji a-address Kiti, ndiyo utaratibu.

**MHE. CHARLES M. KITWANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kitwanga, kikanuni kwa kuwa Waziri ameshazungumza inabidi nimpe nafasi kwanza Mheshimiwa Magereli.

Mheshimiwa Magereli ulikuwa unapewa ushauri, kwamba kwa kuwa inabidi uzungumze na mimi sasa itabidi mimi ndiye nikusaidie kupeleka labda hayo maombi. Kikanuni inabidi uni-address mimi, nadhani hilo limekaa vizuri. Mheshimiwa Magereli. *(Kicheko)*

**MHE. LUCY S. MAGERELI:** Mheshimiwa Naibu Spika, wakati naanza mchango wangu niliomba idhini ya Kiti, kwa hiyo, naamini na wewe unamwamini Mwenyezi Mungu na hili wala halikupi shida, naomba niendeleo na mchango wangu.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Magereli, maombi tulishaomba asubuhi, ndiyo utaratibu wa Bunge, kwa hiyo, wewe endelea na mchango wako huo lakini address Kiti kama kanuni zinavyosema, hapo ilikuwa unakumbushwa tu. Kwa hiyo, wewe endelea na mchango wako lakini address Kiti.

**MHE. LUCY S. MAGERELI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa maelekezo yako. Naomba basi niwakumbushe mimi kwa sababu tayari Mungu ameshaona dhamira niliyonayo moyoni kwangu, basi atayajibu maombi hayo kwa ileile dhamira yangu kwamba ...

## T A A R I F A

**MHE. CHARLES M. KITWANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Magereli, kuna taarifa ya Mheshimiwa Kitwanga.

**MHE. CHARLES M. KITWANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimpe taarifa mzungumzaji kwamba, Watanzania wanahitaji ndege za *ATC* si kwa sababu ya wao kuzipanda. Ndege hizi zitakapokuwa zikiruka zikileta watalii, watalii wataleta pesa, pesa hizo zitakuwa nyingi na tutakapozipata zitatumika katika maji, elimu na afya. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Lucy Magereli, unaipokea taarifa hiyo kutoka kwa Mheshimiwa Kitwanga?

**MHE. LUCY S. MAGERELI:** Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru Mheshimiwa Kitwanga kwa taarifa yake, lakini mngewapa fursa Watanzania wakachagua nini wanataka, kati ya ndege au nini ambacho kitaleta madhara kwenye maisha yao, wangekuambieni wanataka *X-Rays*, *CT-Scan*, *MRI* kwa ajili ya afya zao kwa sababu mpaka sasa hivyo ni vitu ambavyo vinaonekana ni vya kupatikana Ulaya na si Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sasa nimalizie kwanza kwenye ile hoja yangu ya sala, kwamba namshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kuwa amejidhihirisha yupo na anatenda miujiza katika maisha ya Mheshimiwa Tundu Antiphas Mughwai Lissu. Yule ambaye mlimtesa, mkampiga

risasi 18, mkakataa kupeleleza nani alifanya hivyo, mkashindwa kumtibu, navyozungumza ...

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Magereli, unafahamu maana ya 'm' kwenye hicho usemacho? Ukisema 'mli', ni akina nani na wewe upo ama mimi? Kwa sababu unani-*address* mimi, ukisema mlitesa, maana yake mimi ni sehemu ya watesaji. Sasa tusiende huko Mheshimiwa, naomba jielekeze kwenye mchango uliokuwa umejipanga kuuchangia, tusiende kwenye haya maneno mengine ambayo yanaleta ukakasi ambao hauna maana yoyote kwa sasa. Mheshimiwa Magereli.

**MHE. LUCY S. MAGERELI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimshukuru Waziri wa Maji, kwa kazi nzuri aliyofanya, baada ya malalamiko ya wananchi na wakazi...

#### T A A R I F A

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hii itakuwa taarifa ya mwisho kwa asubuhi hii. Mheshimiwa Musukuma.

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. Nilitaka tu kutoa taarifa kwamba, mzungumzaji anayezungumza amesema Mbunge mwenzetu alipigwa risasi 18 lakini taarifa za mwanzo zilizotolewa na Msemaji wa Kambi Rasmi ya Upinzani kwamba amepigwa risasi 38. Sasa inaonekana wenzetu wanajua mpigaji ni nani kwa nini wasilithibitishie Bunge ili hii hoja ikajiondoa kabisa Wabunge tukaacha kujadili suala la Lissu?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Lucy Magereli, unaipokea taarifa hiyo?

**MHE. LUCY S. MAGERELI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niendeele na mchango wangu. Naomba

nimshukuru Mheshimiwa Waziri wa Maji kwa kazi nzuri aliyoifanya baada ya malalamiko ya sisi wadau na wakazi wa Kigamboni kuhusu mradi wa visima 20 vya maji vya Kimbiji na Mpera ambavyo hata juzi wakati nauliza swali kwa niaba ya Mheshimiwa Mwita Waitara nilieleza kwamba vile visima havijakamilika, kwa hiyo, Serikali inatudanganya kutuambia kwamba visima vimeshakamilika kinachofanyika ni kutafuta fedha kwa ajili ya usambazaji. Kwa taarifa rasmi zilizotolewa na Serikali juzi nimeona amevunja Bodi ya *DUWASA* na kuwawajibisha waliohusika wote kwa sababu ya ubadhirifu uliofanywa katika vile visima 20 na kwamba mpaka leo havijakamilika. Kwa hilo, naomba nimpongeze Mheshimiwa Waziri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna jambo lingine ambalo na mimi nataka nilizungumzie kwa kina ambalo ni unyanyasaji na matendo yasiyo sawa kwa wafanyabiashara, watu wa sekta binafsi na wawekezaji. Ukitaka kuwekeza Tanzania, unaandamwa na ada, tozo, kodi, ushuru, leseni, na vibali visivyopungua 30. Tunasema tunakwenda kwenye Tanzania ya Viwanda, tunafikaje huko? Sisi tunaikimbia *PPP*, hatutaki kufanya miradi ya ushirikiano, wawekezaji wanaotaka kuwekeza nchini kwetu tunawaandama kwa milolongo ya kodi, ada na tozo zisizomithilika, tunafikaje Tanzania ya Viwanda? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ukitaka kuwekeza katika kiwanda au katika sekta ya kilimo kwa ujumla, unatakiwa kulipia kibali cha *BRELA, TBS, TPRI, TOSC, NEMC, Fire, Bima, OSHA, Zimamoto, TIN/VRN*, Leseni ya Biashara, Vibali vya Kusafirisha Mazao, Ushuru wa Kusafirisha Mazao, Usajili wa Mbegu, Mabango, Bodi ya Usajili na Mizani na Vipimo. Ukiwa mwekezaji ukafika nchini ukapewa orodha ya kwamba haya ndiyo matakwa unayotakiwa kukamilisha ndiyo hatimaye usajiliwe na kufanya biashara Tanzania, naamini hata kama ungekuwa ni wewe ungekimbia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie swali lingine la mipango inayoendelea ya kutaka kuuwa Serikali za Mitaa.

Mipango yote tuliyonayo sasa hivi kiukweli na ukitazama hali halisi ilivyo tunamaanisha tunataka kurudi kwenye *Centralization* na si *Decentralization* ambayo ndiyo mfumo ambao tumekuwa tunautumia wakati wote. (Makofi)

Mheshimiwa Naisu Spika, tumechukua vyanzo vya mapato vyote vya Serikali za Mitaa. Majukumu ambayo yalikuwa yakitekelezwa na Serikali za Mitaa mengi sasa naona yapigiwa upatu kwamba yarudishwe Serikali Kuu. Majukumu kama ya ujenzi wa barabara za vijijini tukaanzisha mamlaka inaitwa *TARURA*. Leo Serikali za Mitaa zinakwenda kukutana na aina ngumu kabisa ya mateso kwa sababu hata fedha za utekelezaji wa shughuli zake zitatakiwa kuombwa kutoka Serikali Kuu. Mmeshiona kwa miaka miwili hii iliyopita unaomba fedha inachukua muda mrefu sana hata kupatiwa hizo fedha kwa ajili ya matumizi mengineyo ya Serikali za Mitaa. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, fahamuni kwamba katika Serikali za Mitaa ndiko kwenye umma mkubwa wa Watanzania na ndiko wanakopata huduma kwa maeneo ya karibu. Sasa tunapofikiri kwamba lazima tupange mlolongo mrefu kusubiri fedha kutoka Serikali Kuu, nadhani hili ni kosa kubwa tunalolifanya na Mheshimiwa Waziri aangalie namna ya kulirekebisha. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna suala ambalo nimeliona kwenye bajeti kwamba kuna mpango wa kulinda viwanda vya ndani kwa kuongeza *import duty*. Mimi nadhani ambacho tunapaswa kufanya si kuongeza *import duty* kwa bidhaa zinazotoka nje ni kuangalia mazingira yetu yanavyoweza kuwa rafiki ili tuboreshe kilimo chetu lakini tuzalishe kwa wingi tutosheleze soko letu na tuweze kuwahudumia Watanzania bila kufikiri kuwakandamiza watu wengine ambao wanatakiwa kutuhudumiwa ambapo kwa wakati huo hatujaweza kuzalisha hizo bidhaa toshelevu kiasi tunachotaka. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye kitabu cha Kamati na kabla sijasoma maoni hayo niliyoya-*quote* kishemu



kidogo, niipongeze Kamati ya Bajeti wamefanya kazi nzuri, wamechambua vizuri na wamekuwa *honest*, wamekuja kwenye Bunge na wamesema ukweli kuhusu wanachokiona kuhusu mwenendo wa bajeti ya nchi hii. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika ukurasa wa 30, Kamati wanasema kwamba, Kamati inajiuliza kuwa upungufu huu mkubwa wa mikopo na misaada kutoka nje unatokana na nini? Naomba nisaidie kuijibu Kamati kwamba upungufu wa misaada na mikopo kutoka nje inaletwa na ukanywagaji wa Katiba katika maeneo ya utawala wa sheria, utawala bora, uhuru wa kupata habari, uhuru wa kujieleza, uchaguzi wa Zanzibar na mauaji ya raia ambayo mpaka sasa hayachunguzwi na hatupati majibu yake. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika...

*(Hapa kengele ililia kuashiria  
kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Kengele ya pili imeshagonga Mheshimiwa, ahsante sana.

Tunaendelea na Mheshimiwa Conchesta Rwamlaza, atafuatiwa na Mheshimiwa Fakharia Shomar Khamis kama muda utaruhusu Mheshimiwa Mansoor.

**MHE. CONCHESTA L. RWAMLAZA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili na mimi niweze kuchangia kidogo kuhusu hoja iliyo mbele yetu ya bajeti ya Serikali mwaka 2018/2019.

Mheshimiwa Naibu Spika, navyoelewa mimi ni kwamba hapa tunachojadili ni mipango yetu ya maendeleo tunaitafsiri kwa minajili ya pesa. Tunapanga bajeti, tunatoa pesa au sisi kama Bunge tunaidhinisha ili Serikali iweze kutekeleza ile mipango ambayo imeletwa hapa na imepitishwa na Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, kinachonisikitisha ni kwamba Bunge hapa linakaa linapanga bajeti lakini Serikali hii iliyoko madarakani kusema ukweli haina nidhamu ya kusimamia matumizi jinsi bajeti ilivyopitishwa. Tunapitisha bajeti Serikali inakwenda kutumia pesa bila hata kulishirikisha Bunge. Si makosa Serikali kuomba bajeti au *supplementary budget* pale ambapo kumelazimika kuwa na matumizi ya lazima na hayakuwepo kwenye bajeti lakini Serikali haileti inatumia inavyoona kitu ambacho nakiona ni dharau kwa Bunge hili. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, nije kwenye uhalisia wa bajeti. Nchi yoyote inapanga bajeti kulingana na uwezo na makusanyo yake. Ukiangalia mwaka jana, tulipitisha bajeti zaidi ya shilingi trilioni 31 lakini haikutekelezeka kwa sababu makusanyo hayakuweza kutosheleza. Mwaka huu pia tunakwenda kwenye bajeti ya shilingi trillion 32, je, tuna uhakika wa kukusanya ili bajeti iweze kutekelezeka? Nachoshauri Serikali wala isione aibu, pale ambapo wanaona makusanyo hayatoshelezi na hayatapatikana leteni bajeti ambayo inalingana na uwezo wa nchi yetu ili tusifanye kwa kuonesha wananchi kwamba Serikali inaweza kukusanya mapato makubwa na hatuwezi kufanya jinsi wananchi wanavyotegemea. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, niongelee kuhusu Halmashauri. Wengi sana wamesema kuhusu *D by D*, lakini mara nyingi nikisimama huwa nairejesha Serikali hii katika kitu kilichotendeka mwaka 1972 – 1982, kile kilichokuwa kinaitwa madaraka mikoani, walikuwa wanasema *decentralization*, sijui kama ilikuwa *D by D*. Zoezi hili lilishindwa kwa sababu naona Serikali hii inapenda kuongoza nchi hii kwa *trial and error*. Tunajaribu tunashindwa halafu sijui tuna-*retreat* halafu tunaenda kuanza upya. Kwa hiyo, nchi inakaa katika kupanga na kupangua tu, ni kama tunafanya *experiment* kwamba tujaribu hili. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali sasa inarudi kwenye *centralization* kwa sababu inachukua pesa yote inaweka katika mfuko mmoja. Dhana ya kuanzisha halmashauri hizi

ni ipi? Kama zilianzishwa kwa ajili ya kutoa huduma kwa wananchi na kwa kuzingatia kwamba nchi hii ni kubwa, huwezi kuiendesha ukisimama Dar es Salaam peke yake, haiwezekani. Kama tulijaribu tukashindwa ni kwa nini sasa Serikali inataka kuturudisha kule. Hizi halmashauri kama Serikali iliyoko madarakani haizitaki leteni sheria hapa tubadilishe, tubaki na madaraka kule makao makuu ya Serikali halafu pesa zote ziwe zinatoka huko zinakuja kule chini, kitu ambacho hakitawezekana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vyanzo vyote vya halmashauri, kama walivyosema wengine na wewe unavijua vimekwenda Serikali Kuu. Kitu ambacho kimenisikitisha ni hata ardhi, maana halmashauri nyingi zinategemea ardhi le ya wilaya lakini hata ile asilimia 30 ambayo ilikuwa inabaki au inapaswa irudishwe kule katika halmashauri kusaidia kwa sababu inatokana na ushuru au tozo mbalimbali ambazo zinatokana ardhi na yenyewe mmebeba mmepeleka Wizarani sijui Hazina na pesa hizi hazirudishwi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hebu tutazame ile *Local Government Development Grant* mpaka sasa hivi hakujatolewa hata senti tano. Kibaya zaidi hata kipindi hiki Serikali haijajaweka bajeti ya pesa hizo kurudi katika halmashauri. Kama pesa hizo hazirudi miradi yote ambayo ilikuwa imepangwa kufanywa na halmashauri madarasa, zahanati, imekwama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kama Serikali imeshindwa kurudisha hicho kidogo tu, je, ikiwa na mfuko mkubwa maana yake ni nini? Labda Serikali inachotaka kutuonesha ni kwamba imeweza kukusanya, siyo hivyo, la hashu, haijakusanya ni kwamba wamepora vyanzo vya halmashauri na halmashauri ziko mahututi na hatutegemei kwamba kweli wananchi wa Tanzania wataweza kupata huduma wanazostahili kama barabara.

Mheshimiwa Naibu Spika, mnaona barabara wanazotengeneza *TARURA* hata hapa Dodoma nendeni huku tunakokaa mitaani, wanatengeneza barabara ambazo

hata ma-*engineer* hawafiki. Mmechanukua ma-*engineer* wote wa halmashauri wameenda *TARURA*, halmashauri zimebaki hivi hivi zina wayawaya, ni kwamba hata barabara zinazotengenezwa hazipo. *TARURA* haiwezi kutengeneza barabara nzuri kwa sababu haipati pesa, watafanya *grading* tu lakini hawawezi kutengeneza barabara ambazo zitaweza kupitika ili wananchi waweze kusafirisha mazao yao. Hata huduma nyingine za afya, elimu hazitaweza kutekelezeka kama halmashauri hazipati pesa na Serikali Kuu inazikalia haipateki pesa katika halmashauri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nije kwenye kilimo. Ni jambo jema kwamba Serikali imeleta bajeti ambayo kipaumbele chake ni kilimo. Ila mimi ninajuliza kipaumbele hiki mmeweka katika makaratasi, je, utekelezaji wake ukoje?

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi ambao tuna umri kidogo unawazidi walio wengi hapa, hebu turudi nyuma tuangalie ile Awamu ya Kwanza ya Hayati Mwalimu Nyerere aliwezaje kufanikiwa kutengeneza kilimo kikasaidia nchi yetu. Si vibaya na wala si dhambi kuangalia kule nyuma huyu bwana alifanyaje kwani makaratasi hayapo, mafaili hayapo, mipango haipo? Naiomba Serikali irudi nyuma ione ni kitu gani ambacho Awamu ile ilifanya (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza walikuwa na *extension officers*, sasa hivi kilimo kinasemwa lakini hakuna elimu inayotolewa kwa wakulima. Hata yale mashamba darasa mnayoyasema hayapo na kama yapo yametelekezwa. Sisi tunakaa vijijini huko, mimi nikienda nakaa kijiji sijawahi kumwona *extension officer* wa kata na hata hao waliopo hawana huduma. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi niko kwenye kamati ya *LAAC* kuna siku moja tumemwambia *CAG* hebu nenda kafanye *performance auditing* ya hawa ma-*extension officers*, kwa kweli wanapata mishahara ya bure, atuoneshe wanalipwa nini na wanafanya nini. Kama hawastahili kuwepo basi waondoke wakulima wajitegemee wenyewe

wanavyoona yaani bora liende kila mkulima anafanya anavyoona. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hivi nchi yetu ina vijiji zaidi ya 19,000, je, wako ma-*extension officer* kiasi gani ambao wanaweza kusaidia kuongoza wakulima? Mimi nakumbuka baba yangu alikuwa analima kahama na kwenye kilimo cha kahawa walikuwa wanakuja *extension officers* wiki mara mbili na pikipiki sasa hivi hawana hata usafiri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nije kwenye kahawa. Niongezee kwa mchango wa Benardetha Mushashu jana ...

*(Hapa kengele ililia kuashiria  
kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Muda wako umeisha Mheshimiwa, ahsante sana. *(Makofi)*

Tunaendelea na Mheshimiwa Fakharia Shomar Khamis.

**MHE. FAKHARIA SHOMAR KHAMIS:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kupata nafasi hii na mimi kuchangia hoja ya Bajeti Kuu ya Serikali ya mwaka 2018/2019.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza lazima nifurahie kwamba sasa hivi Tanzania inaelekea katika viwanda, ina maana Tanzania ya Viwanda. Bajeti aliyoleta Mheshimiwa Waziri imepangika, ina vionjo vya kutendea kazi na inatekelezeka. Hongera Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Naibu na watendaji wote wa Serikali katika Wizara hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kujielekeza katika viwanda lazima tuwaangalie wakulima. Bila ya kuwa na wakulima hodari wakaweza kutupatia malighafi viwanda vitakosa malighafi na amesema kwamba viwanda vya ndani vitapata malighafi hapa hapa Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa wakulima, kama kweli watajielekeza kwenye kulima ina maana sasa ni mwaka wao nao wa kufarijika katika maisha. Kwa sababu wataweza kuongeza mashamba, watakuwa na ushindani katika bidhaa zao watakazokuwa wanalima, watakuwa na masoko kwamba watapeleka mazao yao katika viwanda vyetu. Naomba wakulima waangaliwe ili kupata malighafi ili viwanda vyetu viweze kujjendesha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ukija kwa upande wa pili, tukumbuke kwamba Wizara ya Fedha wanatumia *cash budget* kwa maana makusanyo mnayoyapata ndiyo mnayoyatumia. Sasa inabidi lazima wajitahidi kupata kodi ili kupata pesa za kutosha, bila ya kukusanya haitawezekana kutumia. Baadhi ya watendaji wetu wanaweza wakazembea katika kukusanya huruma isiwepo, mtu anazembea kwenye kazi unamuondoa kwenye nafasi yake kwa sababu akizembea yeye ameifanya Serikali yote mapato. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tuchukulie mfano, siku za hivi karibuni zile mashine zetu za kukusanya mapato *efd* zimeharibika, Wabunge wanapiga kelele, jawabu tunalolipata halitoshi kwa sababu mpaka leo ukweli hasa hatujaupata. Sasa tuangalie, tatizo lilikuwa kwa wenye mashine au uzembe wa wafanyakazi au kuna kitu gani kilichojitokeza mpaka leo hakuna suluhisho? Kuna Mbunge mmoja pia hapa kalizungumza hili kwa sababu sasa hivi watu wanatumia risiti na kama tunatumia risiti tayari tunapigwa. Mheshimiwa Waziri akija na hilo lazima alizungumzie ili tuweze kufarijika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, malalamiko mengi yanatokea hapa kuhusu malipo ya kodi mara mbili katika bandari zetu kwa vitu vinavyotoka Zanzibar. Suala hili limezungumzwa, nakumbuka Naibu Waziri wa Fedha alilitolea ufafanuzi kwamba wanakaa sasa hivi wanalizungumza na wakati wowote watafikia muafaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini mimi nina ushauri, kwa sababu jambo lolote linataka elimu, Wizara ya Muungano

iko inashughulikia Bara na Visiwani, ipeni majukumu pia Wizara hii kutoa elimu. Taasisi za Zanzibar na na Bara zinazoshughulika na mambo ya fedha wapewe elimu ili waelewe kwa nini huu mvutano unatokea, kwa sababu sheria mnajua ziko vipi na mwelekeo uko vipi ili huu mvutano uzidi kupungua. Nendeni kwenye *media* mtoe maelezo kuna nini na baadaye mkubali watu wapige simu nao watoe taarifa au malalamiko yao, myapokee na myajibu. Haya ni mambo madogo tu yanazungumzika. Jambo hili linachukua muda mrefu ilhali si refu. Tunalifanya liwe refu ili tuweke mvutano hapa usio na maana ilhali jambo hili linazungumzika na ni rahisi kumalizika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nakuja na suala lingine ambalo liko katika ukurasa wa 46(v), kuhusu kusamehe Kodi ya Ongezeko la Thamani kwenye taulo za kike ili isaidie vijana wetu wa kike na akina mama katika matatizo yao ya kawaida. Nakubali Mheshimiwa Waziri alivyosema kwamba wamepunguza kodi, ni sawa lakini kupunguza huko kusiwe kwa mwaka huu na mwakani upunguze tena ili iwe wanapunguza kidogo kidogo mpaka ifikie sawasawa kama mtu anakwenda kununua karanga haoni shida tena bei yake itakuwa rahisi tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, viwanda vya ndani vinazalisha, itakuwa kila wakiteremsha bei na bei ya dukani itakuwa inashuka na itakuwa rahisi kila mmoja kununua hata mtoto wa chini atanunua. Inaweza ikafika mpaka Sh.500; inategemea jinsi Wizara itakavyokuwa inashusha na malighafi hiyo itakavyokuwa inauzwa madukani ili vijana na akina mama wetu wamudu kununua bidhaa hiyo. Baadaye itafikia mpaka kupata bure, maana unaenda kununua kitu unaambiwa Sh.200 au Sh.500, si bure hiyo? Naomba Mheshimiwa hili aliangalie kila akija anapunguza bei mpaka tufikie katika malengo tuliyoyakusudia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, niongelee kuhusu halmashauri, ukurasa wa 54. Marekebisho ya Sheria ya Fedha Serikali za Mitaa, Sura Namba 290 kwa kuongeza kifungu cha

37A. Nakubaliana na maelezo ya Mheshimiwa Waziri, ni sahihi kwa sababu hii asilimia 10 inayokwenda kwa vijana na wanawake ilikuwa haina sheria lakini mtakapotungia sheria itakuwa ni lazima itendeke. Kwa hiyo, nawaomba TAMISEMI watengeneze kanuni haraka ili ziweze kutengenezewa sheria ije Bungeni ili tuwe na uhakika kwamba 10% ya vijana na wanawake ipo kisheria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, shida tunayoipa mkaona halmashauri hawatoi ni kwa sababu wanaona hawana panapombana ni maelezo tu ya maandishi. Isitoshe halmashauri zinajipangia miradi ambayo haina *priority* nyingi... *(Makofi)*

*(Hapa kengele illia kuashiria  
kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Fakharia, muda wako umekwisha.

**MHE. FAKHARIA SHOMAR KHAMIS:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, mengine nitachangia kwa maandishi. Naunga mkono hoja na Mheshimiwa hapa kazi tu, endelea na majukumu yako kama yalivyo. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Fakharia. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tumefika mwisho wa kipindi chetu cha asubuhi. Nilete tangazo moja kwenu kabla sijataja majina ya Waheshimiwa Wabunge tutakaoanza nao mchana, kuna miwani ilishaulika kwenye kiti cha Mheshimiwa Martha Mlata, ameileta hapa mbele imeandikwa *Carol* kwa maana ya wale watengenezaji wa hii miwani. Kwa hiyo, kama kuna mtu amepoteza miwani yake haioni atawaona Makatibu watamkadhi miwani hii iliyosahaulika hapo.

Waheshimiwa Wabunge tutakaoanza nao tutakaporejea ni Mheshimiwa Mansoor Shanif, Mheshimiwa Daniel Nsanzugwanko, Mheshimiwa Leah Komanya,



Mheshimiwa Magdalena Sakaya, Mheshimiwa Masoud Abdallah Salim, Mheshimiwa Cecilia Paresso, Mheshimiwa Susan Kiwanga na wengine tutaendelea kuwataja kadri tutakavyokuwa tukiendelea na michango yetu.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo, nasitisha shughuli za Bunge mpaka saa 11.00 jioni leo.

*(Saa 7.00 Mchana Bunge Lilisitishwa hadi Saa 11.00 Jioni)*

*(Saa 11.00 Jioni Bunge lllirudia)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tukae.

### **MWONGOZO WA SPIKA**

**MHE. PETER J. SERUKAMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Mwongozo wa Spika.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Peter Serukamba.

**MHE. PETER J. SERUKAMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba mwongozo kwa kutumia Kanuni ya 47(3) ambayo inasema:-

*“Hoja itatolewa na Mbunge kwa kusimama mahali pake kuomba idhini ya Spika kutoa hoja ya kuahirisha Shughuli za Bunge kwa madhumuni ya kujadili jambo halisi la dharura na muhimu kwa umma”.*

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka kukuomba unikubalie nitoe hoja tuahirishe shughuli za Serikali ili tuweze kujadili jambo la dharura lililotokea Bungeni leo.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Peter Serukamba amesimama akisema anaomba mwongozo na ametaja Kanuni ya 47. Sasa mwongozo unaombwa kwa mujibu wa Kanuni ya 68(7) lakini yeye anasema anayo hoja ambayo anataka kuileta chini ya Kanuni ya 47. Nitampa fursa aeleze maelezo yake ili niweze

kuona kama hiyo hoja ni ya dharura ama hapana. Mheshimiwa Peter Serukamba.

**MHE. PETER J. SERUKAMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kushukuru kwa kunipa nafasi hii niweze kutoa hoja ili Bunge lako liweze kujadili hoja hii kama itawapendeza, kwangu mimi naona ni hoja ya dharura.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo hapa Bungeni wamekuja maafisa wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi, wakaenda kwenye kantini ya Bunge, jikoni, wakaanza kupima samaki ambao wameshaandaliwa. Cha ajabu zaidi hawa maafisa wamekuja Bungeni hawakumwambia Spika, hawakumwambia Katibu wa Bunge, hawakuiambia Serikali, hawakukwambia wewe Naibu Spika, maana yake ni nini? Maana yake ni kwamba Bunge hili sasa hatuko salama na kantini ile wanaokula ni Waheshimiwa Wabunge. Hivi huyu anayekuja tunajua amekuja kwa sababu gani? Pia mtu yeyote anayekuja nyumbani kwako si anapiga hodi, anakuja na jambo mahsus. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, hili nataka niwaombe Wabunge wenzangu tulijadili ili tuone hawa maafisa uvuvi, maafisa samaki nguvu hii ya kutaka kuja kulishusha hadhi Bunge lako Tukufu wameipata wapi? Maana leo wamekuja kwa ajili ya samaki kesho watakuja kwa jambo lingine. Naomba Wabunge wenzangu tuwe na wivu na Ubunge wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja sasa ili tuweze kuahirisha Bunge tuweze kujadili jambo hili. Naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

*(Hapa baadhi ya Waheshimiwa Wabunge  
Walisimama Kuunga Mkono Hoja)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, naomba mkae kidogo kwa ajili ya utaratibu ili kanuni zetu tusizipungukie.

Waheshimiwa Wabunge, Kanuni ya 47(4), nitawasomea, inasema:-

*“Iwapo Spika ataridhika kwamba jambo hilo ni la dharura, halisi na lina maslahi kwa umma, basi ataruhusu hoja hiyo itolewe kwa muda usiozidi dakika tano na mjadala juu ya hoja hiyo utaendelea kwa muda ambao Spika ataona unafaa kwa kuzingatia mazingira ya suala linalojadiliwa”*

Sasa Mheshimiwa Peter Serukamba ametoa maelezo yake na yeye akafika mahali pa kutaka kuitoa hoja hiyo ili Waheshimiwa Wabunge muiunge mkono. Kwa maelezo aliyotoa na kwa masharti tuliyonayo kwenye Kanuni ya 47 jambo hili alilolieza Mheshimiwa Peter Serukamba halina utaratibu mahsusi ambao linaweza kushughulikiwa, kwa hivyo tutalijadili hapa Bungeni. Sasa nitakaa ili nimruhusu atoe hiyo hoja yake muiunge mkono kama itaungwa mkono, kama haitaungwa mkono basi tutaendelea na ratiba iliyo mbele yetu.

Mheshimiwa Peter Serukamba kwa sababu ulishatoa maelezo mwanzo huna haja ya kurudia hayo maelezo, utoe hoja ili tuendelee. *(Makofi)*

**MHE. PETER J. SERUKAMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Sasa Waheshimiwa Wabunge wenzangu, naomba kutoa hoja ili tuweze kuahirisha Shughuli za Bunge tuweze kujadili jambo hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja.

**MHE. DANIEL N. NSANZUGWANKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hoja ya Mheshimiwa Peter Serukamba imeungwa mkono. Mimi kwa kuzingatia ratiba iliyo mbele yetu, nitatoa muda usiozidi nusu

saa ili tulijadili jambo hili halafu nitatoa maelekezo kulingana na michango yenu Waheshimiwa Wabunge.

Waheshimiwa Wabunge, wanaotaka kuchangia hoja ya Mheshimiwa Peter Serukamba sasa wasimame ili niorodheshe majina yao. Nitachukua Wabunge 10 na dakika zitakuwa tatu tatu ili muda wetu tuweze kwenda nao vizuri. Mheshimiwa Mtolea, Mheshimiwa Paresso, Mheshimiwa Selasini, Mheshimiwa Dunstan Kitandula, Mheshimiwa Mwamoto, Mheshimiwa Rashid Shangazi, Mheshimiwa Almas Maige, Mheshimiwa Kadutu, Mheshimiwa Kuchauka na Mheshimiwa Sware Semesi. Tunaanza na Mheshimiwa Abdallah Mtolea.

**MHE. ABDALLAH A. MTOLEA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi nichangie hoja hii maalum na mahsus kwa jambo hili maalum kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mara kadhaa tumekuwa tukilalamika namna ambavyo watendaji wa Serikali wanavyowanyanyasa wananchi. Achilia mbali leo kuingia katika Ofisi za Bunge kwenye kantini ya Bunge na kuanza kunusa vyungu na kuangalia kama kuna samaki wadogo tumekuwa tukiona askari wa wanyamapori pia wakipita mitaani kwenye nyumba za watu wakikuta jembe lina mpini mpya wanakwambia wewe umeenda kukata mti, wakikuta chungu chako zimebaki nyama mbili, tatu wanasema hii nyama inanukia nyama ya porini ulienda msituni na watu wamekuwa wakikamatwa kwa namna hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa Mungu si Athumani leo tumeletewa ndani kabisa tuone manyanyaso yalivyo, kwamba hata wasingewakuta hao samaki wangekuta miiba bado wangesema hii miiba kwa ukubwa huu huyu samaki alivuliwa kabla ya muda wake. Hivi, watendaji wa Serikali wameishiwa mbinu kabisa za kuwakamata watu ambao wanavua samaki mpaka tunakuja kunusa vyungu, tunakuja kukaguana kwenye majiko? Hili haliwezekani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pili lazima tujue kama leo mtu anaweza kuja na kuingia mpaka kwenye kantini ambayo Waheshimiwa Wabunge wanakula, usalama wa Wabunge uko wapi? Kwa hiyo, tunakula vyakula ambavyo mtu mwingine anaweza akaingia, huyu mtu kabla hajaenda kwenye kuwakagua hawa samaki, yeye kakaguliwa wapi kama hana sumu, hana kitu chochote ambacho kinaweza kuwazuru Wabunge? Jambo hili halikubaliki na ni lazima hawa watu washughulikiwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Paresso.

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia katika hoja iliyowasilishwa na Mheshimiwa Serukamba na mimi naunga mkono hoja hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama alivyosema Mheshimiwa Mtolea labda inawezekana leo yalikuwa tu ni makusudi ya Mwenyezi Mungu hili likatokea ndani ya Bunge. Kwa sababu changamoto hizi na manyanyaso haya wamekuwa wakipata wananchi katika mambo mbalimbali ukiacha hili lililoko mbele yetu leo la Wizara ya Mifugo na Uvuvi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaokula kantini pale, tunaotumia wale samaki ni mlaji wa mwisho wa bidhaa yoyote. Sasa unajuliza hawa watumishi kama kweli ni waadilifu na wanajua utaratibu, inakuwaje unamfuata mtumiaji wa mwisho? Samaki tayari ameshakaangwa, ameshaandaliwa unachukua rula unampima, kwa nini hukudhibiti tangu kule mwanzo ambako samaki huyu anavuliwa? Kwa hiyo, huu ni ukiukwaji mkubwa wa sheria na taratibu na ni kuingilia kwa kiwango kikubwa uhuru wa mtumiaji wa mwisho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ofisi yako sasa lazima iangalie usalama wa Wabunge. Kama leo watu walidiriki wakaingia mpaka kantini bila taarifa, utaratibu au kibali, akaenda anachukua rula anapima samaki, kesho kutwa itakuwa nini? Ni lazima jambo hili sasa lituamshie, lituhakikishie usalama wa Wabunge lakini haya manyanyaso ambayo wanapata wananchi katika maeneo mbalimbali yaweze kuchukuliwa hatua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri wangu, watumishi wa ambao wamefanya kitendo hiki ni lazima wachukuliwe hatua za kisheria, kwa nini wamefanya jambo hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Joseph Selasini.

**MHE. JOSEPH R. SELASINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, niseme moja kwa moja kwamba naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Serukamba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeacha wenyewe heshima ya mhimili huu ikamomonyoka na sasa tusipoangalia itaporomoka itakwisha kabisa. Walianza polisi, wanakuja kuwakamata Wabunge hapa bila taarifa kwa Spika, bila taarifa kwa Uongozi wa Bunge. Tulilalamika Spika akatoa utaratibu kwamba asingependa Mbunge wake yeyote achukuliwe tukiwa kwenye *session* bila yeye kuarifiwa. Wamekuwa wakiachwa wakiendelea, sasa taasisi zingine zimeona ni uchochoro. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna suala la afya, mashine zetu zina uwezo wa kupima vyuma na silaha hazina uwezo wa kupima sumu ndani ya mifuko ya watu. Hatujui wale samaki wamewashika katika mazingira gani ya kiafya. Siyo hivyo tu, yaani samaki wameshapikwa, wapo kwa mlaji wa mwisho ndiyo wanapimwa, hapa tulipofikia ni pa kushangaza.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Mheshimiwa Serukamba atakapokuwa anafanya majumuisho ya hoja yake, Bunge hili liazimie watu hawa waitwe kwenye Kamati ya Maadili, wahojiwe, ijulikane kwanza waliingiaje humu, walieleza wanakuja kufanya nini humu, walieleza mwenyeji wao ni nani ili tujue huo mlolongo na utaratibu waliotumia mpaka wakafika hapo walipofika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Dunstan Kitandula.

**MHE. DUSTAN L. KITANDULA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa fursa hii. Nianze kusema maneno haya. Kama kweli kuna mtu ameweza kuingia kwenye Bunge lako Tukufu bila kupata ruhusa, Bunge lichukue hatua stahiki haraka. Hatuwezi kuuacha mhimili huu muhimu ukachezewa hovy hovy namna hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa miaka kadhaa nimekuwa nikipiga kelele kuhusu sekta ya ufugaji wa samaki, jinsi ambavyo tumeshindwa kama Taifa kuwekeza kwenye sekta hii. Leo tunashuhudia nguvu kubwa inatumika kwenye kudhibiti unaoitwa uvuvi haramu. Ningetegemea nguvu hiyo kubwa kiasi hicho tuiweke kwenye kuhakikisha wananchi wa Ukanda wa Pwani ambao wanaangamia kwa umaskini wananufaika na rasilimali yao iliyopo ambayo haitumiki kwa kuwekeza kwenye ufugaji wa samaki. Badala ya nguvu hiyo kuipeleka kule tunaipeleka kwenye vitu *trivial*, hii haikubaliki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nilitegemea nguvu hiyo leo tungekuwa tunaielekeza kwenye kuangalia *incentive package* ambayo ingewezesha ufugaji wa samaki ukaibuka katika nchi hii. Tungehakikisha vyakula vya kufugia samaki vinazalishwa kwa wingi nchini, mashine za kuweka *oxygen* kwenye ufugaji wa samaki zingeingia kwa bei ambayo ni rahisi ya kuwawezesha wafugaji lakini nguvu hizi tunazona zinapelekwa kwenye vitu *trivial*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hili halikubaliki na naomba Wabunge wenzangu tuoneshe hasira yetu kwa kuhakikisha wote waliohusika kuja kufanya mchezo huu katika Bunge letu wanachukuliwa hatua.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Venance Mwamoto.

**MHE. VENANCE M. MWAMOTO:** Mheshimiwa Naibu Spika, niunge mkono hoja ya Mheshimiwa Serukamba. Niseme tu kwamba utaratibu wa wageni kuingia ndani ya Bunge letu unafahamika na utaratibu ambao huwa unatumika mtu anapokosa nidhamu kwa Wabunge au kwa chombo hiki cha Bunge unafahamika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, bahati nzuri waliofanya kosa wanafahamika aidha kwa makusudi au kwa kutaka kuchafua Serikali yetu. Sasa ni vyema wakachukuliwa hatua na wakitwa kwenye Kamati yetu ya Maadili ya Bunge na kushughulikiwa kama wahalifu wengine. Walichokifanya wangeweza hata kuleta kitu kibaya kikawadhuru Wabunge ndani ya Bunge. Kwa hiyo, jambo hili ni *serious* washughulikiwe. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante.

**MHE. JOHN W. HECHE:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Heche, Mbunge uliyetaka kumpa taarifa ameshamaliza kuzungumza. Mheshimiwa Rashid Shangazi.

**MHE. RASHID A. SHANGAZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa nafasi hii. Naomba niunge mkono hoja ya Mheshimiwa Serukamba lakini nataka nitofautiane kidogo na Waheshimiwa Wabunge wenzangu.



Mheshimiwa Naibu Spika, hawa watu sidhani kama wamekuja tu wenyewe hapa ndani ya viwanja vya Bunge. Kwa mujibu wa *clip* ile ambayo inazunguka inaonyesha kabisa kwamba Waziri mwenye dhamana ndiye aliyewapigia simu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nadhani kwamba Mawaziri wetu kuna viburi vingine sijui wanavitoea wapi. Kwa sababu Waziri huyu angekuwa na ujasiri huu ambao ameufanya leo angeenda kuanzia kwenye mipaka na kule bandarini, ambako nyavu zinaingia na kuna maafisa wote wanaokagua halafu unaenda kuchoma za wavuvi kule kwenye maziwa. Nyavu hizo zinapita bandarini, nyavu hizo zinapita mpaka wa Sirari kama zimeingilia Mombasa hatujawahi kuona hata siku moja anawajibishwa Afisa Uvuvi kwa kuruhusu nyavu ambazo ziko chini ya kiwango na kuchukuliwa hatua. Mara zote tumeona kwamba wanaonyanyasika ni wavuvi wadogo na raia wa kawaida. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hili ni jambo ambalo tunapaswa kulichukulia kwa umakini mzito na kwa namna yoyote ile tusingependa...

## T A A R I F A

**MHE. MARWA R. CHACHA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Taarifa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Shangazi, kaa kidogo. Waheshimiwa Wabunge, nitaruhusu taarifa hii moja tu kwa sababu nilikuwa nimetoa nusu saa na bado kuna wachangiji wanahitaji kuchangia. Mheshimiwa Ryoba Chacha.

**MHE. MARWA R. CHACHA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kumpa taarifa msemaji kwamba hili jambo limetendeka hapa lakini huko mtaani ni *very worse*. Kama tunachukua hatua isiishie hapa Bungeni, tutaonekana vibaya kwa wale watu wetu wanaooneka kule, ana samaki wawili

anakamatwa. Mimi naomba jambo hili lisiishie hapa, liende mpaka chini.

Mheshimiwa Naibu Spika, yule mwenye *clip* amesema katumwa na Waziri, huyu Waziri ana shida.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Rashid Shangazi, unaipokea taarifa hiyo?

**MHE. RASHID A. SHANGAZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naipokea kwa sababu ndilo jambo ambalo limetufikisha hapa tulipo na kwa msisitizo zaidi niseme tu kwamba tunasikitika kwamba sisi kama vijana tunapopewa dhamana hizi tunatakiwa tuoneshe ubunifu na si kufanya mambo haya ambayo yanaweza kufanywa hata na mgambo ambaye ameishia darasa la saba. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nilitarajia kwamba kwa kupewa nafasi hizi vijana tungeonesha ubunifu, tungetafuta namna ya kuongeza uzalishaji wa samaki maeneo mbalimbali, tungezalisha vitalu vya samaki maeneo ambayo hayana hata mito na maziwa. Kwa kuendelea kukumbatia maziwa tu haya inaonekana kabisa kwamba nchi hii isingekuwa na maziwa na bahari basi tusingekuwa na Mawaziri ambao wana dhamana hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Kuchauka.

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ili nami nichangie.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi kwa tendo hili ni ili Waheshimiwa Wabunge wajue uwepo wa Mwenyezi Mungu. Mwenyezi Mungu sisi ametupa uwezo wa kulinda haki za watu lakini kwa vile tumeshindwa kuzilinda leo Mwenyezi Mungu amelileta hapa ili mlione mfanye maamuzi. Kwa sababu jambo hili Waheshimiwa Wabunge wengi hapa walishawahi kuomba miongozo kwa mateso wanayoyapata

wananchi wetu huko majimboni na aidha wanyamapori na watu wengine kama askari polisi na lilionekana kama ngonjera, lakini leo Mwenyezi Mungu amelileta hapa ndani ili ninyi mlione, limo kwenye mhimili wenu ili mpate uchungu na ndiyo maana mmeibuka na hoja hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nataka niwaambie Waheshimiwa Wabunge kwamba Mwenyezi Mungu ana makusudi yake kulileta jambo hili hapa. Kwa sababu siku za nyuma mpaka vitanda vimeshatolewa kwenye mabasi, mboga zimeondolewa kwenye majiko, leo hii Mwenyezi Mungu amelileta ndani ya Bunge hili Tukufu ili muone ni jinsi gani wananchi wetu wanavyonyanyasika na uongozi huu na hawa watu ambao wamepewa madaraka yasiyo na ukomo, wajue Mwenyezi Mungu naye ana ukomo, watakwama kwa amri za Mwenyezi Mungu. Kwa hiyo, haya maamuzi mnayoyachukua hapa leo mjue kwamba Mwenyezi Mungu yupo na wale wanaonyanyaswa muda wote na mjue kwamba jambo hili ni zito. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi inawezekana vipi mtu aingie Bungeni? Hivi Dodoma kuna hoteli ngapi? Kwa nini hawajaenda kwenye hizi hoteli nyingine, hawapiki samaki, wanapika Bungeni pekee? Naomba hawa watu waletwe kwenye Kamati yako ya Bunge ya Maadili kwa kuwa lengo lao lilikuwa ni kulidhalilisha Bunge. Kama kufuata samaki wangeweza kwenda hata kwenye hoteli kubwa huko, wangekwenda Morena lakini walikuwa na lengo la kulinyanyasa Bunge na Mwenyezi Mungu anataka kuwaonesha Wabunge ni jinsi gani wananchi wake wananyanyaswa ndiyo maana limekuja hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mchango wangu ni huo.

**MHE. MARWA R. CHACHA:** Huyu Waziri aondoke.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Almas Maige.

**MHE. ALMAS A. MAIGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, kawaida mimi sichangii michango inayotolewa kwa dharura namna hii lakini leo limefikia pabaya sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, zoezi la kupima samaki ndani ya kantini ya Bunge na wafanyakazi wa Serikali, ni wafanyakazi wa mhimili mwingine kuingilia mhimili mwingine makao makuu. Haiwezekani akatumwa mtu kutoka Bungeni kwenda kupima samaki lkulu na haiwezekani mtu akaenda kupima samaki mahakamani. Imekuwaje Serikali wakaja kupima samaki kwenye kantini ya Makao Makuu ya Bunge? Huku ni kuvuana nguo kupita kiasi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja hii ya ndugu yangu Mheshimiwa Serukamba kwa sababu imegusa sehemu mbaya ya usalama wa Wabunge, usalama wetu leo umeguswa katika hali mbaya. Mimi nafikiri kama ni kweli wametumwa na Waziri kama ambavyo watu wanasema basi Waziri huyu ana bidii lakini hana busara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile mimi nadhani Waziri huyu hayuko na Mheshimiwa Rais, Mheshimiwa Rais hataki mambo ya hivi. Mheshimiwa Rais hataki watu wanyanyaswe, hataki watu wakate miti ya bangi badala ya kupanda. Waziri wa Mheshimiwa Magufuli ninayemfahamu hawezi kuja kupima samaki kantini.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini vilevile imekuwaje usalama wamejaa mlangoni kote kule, wameingiaje? Wamedanganya nini mpaka ...

## KUHUSU UTARATIBU

**MHE. JOHN W. HECHE:** Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu utaratibu.

**MHE. ALMAS A. MAIGE:** Walikuwa wamevaa *badge* za wageni, walidanganya vipi...

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Almas Maige, kuhusu utaratibu, kanuni iliyovunjwa Mheshimiwa.

**MHE. JOHN W. HECHE:** Mheshimiwa Naibu Spika, Kanuni ya 64(1)(g), anatumia lugha ya kuudhi dhidi ya Mheshimiwa Waziri, kwamba Mheshimiwa Waziri ana bidii lakini hana busara.

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Lugha mbaya sana.

**MHE. JOHN W. HECHE:** Anapimaje kwamba Waziri Mpina hana busara? Afute kauli yake dhini Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Waziri, chapa kazi. *(Makofi/Kicheko)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Heche amesimama kwa mujibu wa Kanuni ya 64(1)(g), akisema kwamba Mheshimiwa Mbunge aliyekuwa anachangia ametumia lugha ya kuudhi na inayodhalilisha kwa kuzungumzia busara na bidii.

Waheshimiwa Wabunge, matumizi ya maneno hayo, hayo ni maneno ya Kiswahili, ya kawaida kabisa wala si matusi.

**WABUNGE FULANI:** Aaaa.

**NAIBU SPIKA:** Kwa hiyo, kwa mchango anaoutoa Mheshimiwa Almas Maige...

Waheshimiwa ninyi tena mkikaa wote hapo wawili, Mheshimiwa Heche na Mheshimiwa Mchunguji Msigwa yaani mnatusumbua sasa tunashindwa kuendelea na mambo ambayo yako mbele yetu hapa. Aidha, mmoja wetu atoke hapo au mtulizane tafadhali maana mkikaa hapo mnaongea kila wakati. *(Kicheko/Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Almas Maige yuko sawasawa. Mheshimiwa Maige malizia mchango wako.

**MHE. ALMAS A. MAIGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kulinyoosha hilo. Kwanza sikusema Mheshimiwa Waziri ana kosa, nimesema kama hawa watu wametumwa, maana hatujathibitisha kama walitumwa au

wamekuja wenyewe, basi aliyewatuma ana bidii ya kufanya kazi lakini busara hana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, mimi nadhani kama amewatuma huyu mtu hayuko kabisa na mawazo ya Mheshimiwa Rais wetu Mtukufu. Nafikiri watu hawa waliotumwa waeleze wameingiaje Bungeni, walipita mlango gani, walitumia mbinu gani za kuingia ambazo zimeshindwa kulinda usalama wa Waheshimiwa Wabunge?

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha, ahsante na naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Serukamba.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Dkt. Sware Semesi.

**MHE. DKT. IMMACULATE S. SEMESI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa nafasi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nami naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Serukamba. Ni sheria ipi hiyo waliyoitumia hao maafisa wa *fisheries* kuja kufanya *inspection*, kuja kusema kwamba wanaangalia *size* ya samaki au wanaangalia *quality* ya samaki? Namba moja, kama unaangalia *size* ya samaki kuna maeneo mahsusi ya kuangalia *size* za samaki na akiwa katika hali gani. Samaki wale waliokwenda kupimwa walishakuwa wamepikwa. Sasa sentimeta ya yule samaki unai-*judge* vipi? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, namba mbili, unajuaje yule samaki amevuliwa wapi? Kama una wasiwasi na hao samaki wanaokuwa *saved* hapa kwenye Bunge lako kwa nini usimhoji yule mwenye kile kitengo ni nani *supplier* wa wale samaki? Halafu *from there* unakwenda ku-*trace back source* zinatoka wapi? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza huku ni kuudharau mhimili. Wamefuata kanuni zipi na sheria zipi ku-*ambush* Bunge lako? Pili, wamekwenda ku-*risk* afya zetu kwa sababu hata hao wapimaji wamekwenda jikoni na kuepua samaki

waliopikwa bila hata kuvaa *gloves* na kuanza kumpima na sisi ku-*risk* afya zetu. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, bahati mbaya huyu mhusika wa mgahawa amepigwa faini ya shilingi laki tatu. Warudishiwe hela zao kwa sababu hawakufuata utaratibu ule unaotakiwa. Kwa sababu huyu *fish* na *fishery product inspector* alitakiwa aandike ripoti iende kwa *director* wake, wenyewe wamekaa hapa *hardly half an hour* wamepeleka kwenye *news media* kwamba Bunge ni hivi na hivi, huu ni udhalilishaji. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, wiki kadhaa zilizopita tulilia hapa kuhusu Operesheni Sangara kwamba wananchi wananyanyasika na *operation* ile, sasa imetukuta sisi hapa. Mungu si Athuman wamekuja hapa hapa kutudhalilisha kwenye Bunge letu, kile kilio cha wananchi kimeletwa katika Bunge lako. Ahsante. (Makofi)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mchangiaji wa mwisho ni Mheshimiwa John Peter Kadutu.

**MHE. JOHN P. KADUTU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa fursa hii. Mungu ni mwema, watu wote wenye viburi huwa wanaonekana mapema. (Makofi/Kicheko)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa bahati nzuri jambo hili limefanyika na mimi nikiwepo pale. Nilikuwa na Mheshimiwa Mbogo, tukaulizana, kamera zinaingia jikoni na watu wanaingia jikoni. Kwa kifupi ni kwamba jambo hili limeandaliwa, Mheshimiwa Waziri hawezi kukwepa lawama, jambo hili limeandaliwa. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi sipendi kabisa watu wenye kiburi, pepo kiburi ni mbaya kuliko kila kitu. Mheshimiwa Waziri tumeongea hapa mjadala wa Wizara yako, ukaomba kwamba tuwe na utulivu, hivi ni utulivu huu? Unakuja ku-*test* mitambo hapa Bungeni? Haifai. (Makofi/Vigelegele/Kicheko)

Mheshimiwa Naibu Spika, wadogo zangu Mheshimiwa Mpina na mtani wangu Mheshimiwa Ulega, hapa mmetukosea, muombe radhi hapa Bungeni na hili lipeleke kwenye Maadili. Wapo watu tuliwajadili hivi hivi tukawapeleka kwenye Maadili na viburi vyao vikateremka. Hivi ninyi Wabunge wenzetu mnakuja kutu-*test* sisi? Haifai, tuache. Mwaka 2020 unakuja, hivi tukikutana mtaani? Mimi siwaombe mabaya lakini viburi hivi. Tumewaona wengi wenye viburi, yaani ukishatoka hapa ni matatizo, kiburi chote kitakwisha. Kwa nini mtufanyie hivi? Hivi tunakula samaki halafu watu wanatupiga picha na kamera, kiko wapi? Huko mtaani wanasema ahaa, sasa ninyi huwa mnajifanya kututetea mbona mmeshindwa kujitetea? Hili jambo si zuri, hebu tuwe na busara, busara si lazima uwe na umri mkubwa, ukiwa mdogo na busara watu watakuheshimu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Waheshimiwa hawa hawawezi kukwepa jambo hili limepangwa. Ni kama mnapanga mashambulizi kwenda kukomboa mateka pale Entebe, ni jambo limepangwa, hawawezi kukwepa. Twende kwenye Maadili na tuone hatua nyingine zinachukuliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, halafu jambo hili kwa nini limetokea na walenzi wa Bunge wako wapi? Kwa sababu kila anayeingia hapa ana sababu maalum. Sisi tunavyokaguliwa hapa, mtu anavyoingia si lazima aseme nakwenda ku-*search*, nakwenda kutafuta hiki, kwa nini waruhusiwe waingie mpaka kwenye kantini ya Wabunge mpaka tunapigwa picha sisi Wabunge tunakula samaki ambao wamezuiwa?

Mheshimiwa Naibu Spika, tutaendelea kuwaombea ili viburi viondoke. Ahsante. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa mtoa hoja, Mheshimiwa Peter Serukamba, hitimisha hoja yako.

**MHE. PETER J. SERUKAMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Waheshimiwa Wabunge, Bunge letu leo liko majaribuni. Kama kuna jambo Waheshimiwa Wabunge tutajua kwamba



tunauheshimu mhimili huu ni kwenye hili jambo. Maana kama mtu anaweza akaja, amepanga na TV, lakini hayo yote amepanga asimwambie Spika, Katibu wa Bunge, Naibu Spika, maana yake yeye yuko juu ya Bunge hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimeshukuru sana Mheshimiwa Waziri Mkuu yupo, tunakuomba ufanye maamuzi kwa kiongozi huyu wa Wizara hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi niombe Waziri huyu na wale maafisa wake waende kwenye Kamati ya Maadili ya Bunge ili atuambie alikuwa anatekeleza sheria ipi na Bunge hili lifanye maamuzi. Leo Waheshimiwa Wabunge msipofanya maamuzi kwenye jambo hili niwaambieni hatutaheshimiwa tena na Serikali hapa mbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, maana kuna ile hata heshima tu kwamba hawa ni wenzangu. Samaki amekuja kupimwa mtu hajavaa *gloves*; na unajua kilichotokea? Wamemaliza kupima, wamechukua Sh.300,000 wamewaruhusu samaki waendeleo kuuzwa. Mnataka tudharauliwe kiasi gani? *(Makofi)*

**MHE. SUSAN L. KIWANGA:** Risiti ya mashine wametoa?  
*(Kicheko)*

**MHE. PETER J. SERUKAMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naomba Bunge lako Tukufu, nakuomba wewe kwa sababu tuna Kamati yetu ya Maadili, jambo hili liendeke kwenye Kamati ya Maadili na itatuambia tufanye nini kama Bunge lakini tunalo jukumu. Amesema hapa Mheshimiwa Almas Maige, nataka kujjuliza, hivi kweli afisa wa samaki anaweza kwenda nyumbani kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu kupima samaki anaokula? Tuambiane ukweli hapa. Anaweza akaenda Ikulu kupima samaki anaokula Mheshimiwa Rais? Hawezi hata kidogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi ninaliachia Bunge busara yake. Nakushukuru. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, imeletwa hoja na Mheshimiwa Peter Serukamba kupitia Kanuni ya 47 kama Hoja ya Dharura. Waheshimiwa Wabunge, wameunga mkono hoja hiyo na baadhi yetu wamepata fursa ya kujadili. Kwa mjadala ulivyokuwa na mtoa hoja ameshahitimisha, jambo hili ni zito kwa nafasi yake na kati mazingira hayo yametajwa mambo mengi ambayo si kusudi langu kuyarudia; mambo ya afya na usalama wa Waheshimiwa Wabunge na namna watu hawa walivyolingia hapa Bungeni.

Waheshimiwa Wabunge, kwa sababu taarifa hii, ukiacha Mheshimiwa Kadutu ambaye anasema alikuwepo lakini naye si kwamba alikwenda mpaka jikoni labda na hizo kamera pengine naye akajua wamepima na rula, lakini kwa sababu Mheshimiwa Waziri Mkuu yuko hapa ndani sasa, naiagiza Serikali ilete taarifa ya jambo hilo kesho hapa Bungeni. Baada ya kuleta taarifa hiyo, sasa tutapata picha kama jambo hili liamuliwe hapa ndani ama liende kwenye Kamati ili wale watu wapate fursa ya kusikilizwa, kulingana na taarifa ambayo itakuwa imeletwa kesho. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kwa hivyo, kesho Serikali ilete taarifa Bungeni kuhusu mazingira ya jambo hili, namna lilivyotokea ili Bunge liweze kufanya maamuzi juu ya jambo hili. Wakati huo Waheshimiwa Wabunge tutapata sasa fursa ya kuazimia kama Bunge ama kupeleka jambo hili kwenye Kamati ili Kamati ije kutushauri namna ya kwenda nalo. Kwa hiyo, kwa leo tutahitimisha jambo hili hivi kwa leo, lakini tutasikia kesho baada ya hiyo taarifa na kuchukua hatua zinazotakiwa.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kuyasema hayo, tutaendelea na ratiba yetu, Katibu.

**NDG. PAMELA PALLANGYO - KATIBU MEZANI:**

**HOJA ZA SERIKALI**

**Hali ya Uchumi wa Taifa kwa mwaka 2017 na Mpango wa  
Maendeleo wa Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019**

**Na**

**Mapendekezo ya Serikali kuhusu Makadirio  
ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa  
Fedha 2018/2019**

*(Majadiliano yanaendelea)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Tutaendelea na michango ya Waheshimiwa Wabunge na tutaanza na Mheshimiwa Masoor Shanif atafuatiwa na Mheshimiwa Daniel Nsanzugwanko, Mheshimiwa Leah Komanya ajiandae.

**MHE. MANSOOR S. HIRAN:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia hoja ambayo iko mbele yetu. Kwanza kabisa, naomba nichukue nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa afya njema ili niweze kusimama mbele yako.

Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue nafasi hii pia kuwashukuru wananchi wa Kwimba kwa kunipa ushirikiano mzuri ili niweze kutimiza wajibu wangu wa kuwatumikia.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichukue nafasi hii pia kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri wa Fedha, Katibu Mkuu na watendaji wote wa Wizara ya Fedha kwa bajeti nzuri sana ambayo wamependekeza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sababu ya kusema bajeti hii ni nzuri ni kwa sababu mimi kwa mara ya kwanza kwenye historia ya bajeti yetu nimekutana na bajeti ambayo haijapandisha kodi kwenye mafuta ya dizeli na petroli. Ni busara nzuri sana ambayo Mheshimiwa Waziri ametumia kuhakikisha kwamba mafuta hayapandi bei. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimesema hivyo kwa sababu unapotaka kupata uchumi wa viwanda unatakiwa uhakikishe nishati ya mafuta ni bei nafuu. Nampongeza kwa hilo na kama tukienda hivi Mheshimiwa Waziri nina uhakika uchumi wa viwanda ataweza kuufikia vizuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nichukue nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri kwenye historia ya nchi yetu kwa mara ya kwanza mwaka huu tumekutana na riba za benki kushushwa. Riba za kukopa zimeshuka, hiyo ni mara ya kwanza imetokea kwenye historia. Pia ameweza kupambana na *inflation* ambayo iko tarakimu moja, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri kwa kazi nzuri ambayo anafanya yeye na Wizara yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nijielekeze kwenye mchango wa bajeti iliyowasilishwa. Naomba nijielekeze kwenye hotuba ukurasa wa 46, *paragraph* ya kwanza. Naipongeza Wizara kwa kuleta mapendekezo ya kupunguza *Corporate Tax* kwenye viwanda vipya vya dawa za binadamu na ngozi. Nachoomba kwa Mheshimiwa Waziri asibague, viwanda vyote vinavyotengeneza dawa za binadamu na ngozi ambavyo vipo na ambavyo zitakuja vyote azipe *incentive* ya *corporate tax* asilimia 20. Atakapowabagua, wale wenye viwanda sasa hivi watahinda kushindana na viwanda vipya ambavyo vitafika. Kwa hiyo, ni vizuri kuwe na *Corporate Tax* ambayo inafanana kwa wote. Pia nashauri Waziri asiishie kwenye dawa za binadamu, naomba pia viwanda vya dawa za mifugo na kilimo vihusishwe kwenye hili punguzo la *Corporate Tax*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu nyingine nayopenda kuelekeza mchango wangu ni kwenye ukurasa wa 51, *paragraph* 12 ambayo inazungumzia Ushuru wa Bidhaa kwenye sigara zisizo na kichungi. Naomba ni-*declare interest* kuwa mimi ni mdau. Nimesoma hotuba vizuri, amesema kwamba sigara ambazo zinatengenezwa kwa tumbaku inayozalishwa hapa Tanzania kwa asilimia 75 na zaidi ambazo hazitumii kichungi atazichaji *Excise Duty* ya Sh.12,447 na zile nyingine ambazo zinatumia kichungi atazichaji Sh.29,425.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi sikuelewa sababu ya kuweka tofauti hiyo kwa sababu kwanza kabisa mtu anayevuta sigara ambayo haina kichungi anapata madhara makubwa zaidi kuliko yule anayevuta sigara ambayo ina kichungi. Kwa hiyo, mimi nashauri ingekuwa *opposite*; kwamba zile za Sh.12,000 angeziwekea Sh.29,000 ili watu wavute sigara ambayo ina kichungi kwa sababu ile ambayo haina kichungi maana yake anaivuta tumbaku moja kwa moja. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, leo ukienda sokoni sigara ambayo ina kichungi au haina kichungi zote zinazwa kwa Sh.100 mpaka Sh.150 kwa sigara moja. Ukichukua hizi sigara ambazo hazina kichungi zinazotozwa Sh.12,447, sigara hiyo inatakiwa iuzwe kwa Sh.60 mpaka Sh.65 kwenye soko, lakini sasa hivi inazwa kwa Sh.100 kwa sababu sisi hatuna *coins* za Sh.20 na Sh.30. Kwa hiyo, alichotaka Waziri ni kupunguza bei ya sigara ili mwananchi wa kawaida apate faida ya kupata sigara ya bei nafuu, hiyo faida haipo, anayefaidika ni mwenye kiwanda, mwananchi analipa ileile Sh.100. Kwa hiyo, kuna karibu Sh.40 ambayo inapotea kama kodi kwa sababu ya kutokuchaji hiyo bei. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri Waziri aende kuangalia suala hili kwa undani zaidi. Asilimia 70 ya Watanzania wanavuta sigara bila kichungi. Ni vizuri ku-

*discourage* suala hilo na ku-*encourage* watu waende kwenye ile yenye kichungi ili angalau madhara yapungue.

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu nyingine ambayo napenda kupeleka mchango wangu ni ukurasa wa 52, *paragraph* 48 inayohusiana na stempu za kodi za kielektroniki. Mimi napongeza Wizara kwa maamuzi haya mazuri sana, naunga mkono maamuzi haya mia kwa mia. Shida yangu ni moja tu, ni gharama ya hiyo huduma.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo gharama ya kununua stempu moja ya kuweka kwenye boksi la sigara unanunua kwa Sh.13. Naomba nirudie ili Mheshimiwa Waziri anisikie vizuri, leo gharama ya kununua stempu ya sigara kwenye boksi unalipa Sh.13, huyu *SCIPA* ambaye mmemteua kuwa ndiye atakayetoa huduma hii ataitoa kwa Sh.29.75, mara tatu ya bei ya sasa hivi ambayo tunalipa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa mimi sielewi hiyo hesabu imefikaje mpaka mmekubaliana na hii Sh.29.75 wakati sasa hivi tunalipa Sh.13. Ningetegemea tungepata hiyo huduma kwa bei nafuu zaidi kwa sababu ni *electronic tax stamps* si tena karatasi, maana yake gharama zingepungua zaidi kuliko kupanda, ningetegemea ingekuwa Sh.10 au Sh.5. Kwa hiyo, ningependa hili suala mliangalie kwa undani zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia kwa hesabu ya haraka haraka, mwekezaji anawekeza shilingi bilioni 44, ana mkataba wa miaka mitano, kwenye taarifa ya Kamati ya Bajeti imesema kwamba kwa mwaka atakuwa anafanya biashara ya bilioni 66. Kwa hiyo, kwa miaka mitano mtu amewekeza bilioni 44 anachukua bilioni 330 kwa nchi yetu, kweli hesabu ya wapi ndugu zangu? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri pia Ofisi ya *Attorney General* iangalie mkataba huu kwa sababu taarifa nilizonazo ni kwamba huu mkataba alishapata huyu bwana

mwaka 2016 lakini ulikuwa na matatizo ndiyo maana ulikuwa umechelewa kutoka sasa hivi ndiyo umetoka. Kwa hiyo, naomba Serikali iangalie upya hili suala kwani ni zito.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho kabla sijamaliza nichukue nafasi hii pia kumpongeza *Commissioner General* wa *TRA* kwa kazi nzuri wanayofanya yeye na timu yake maana bila makusanyo tusingeongea mambo ya bajeti hapa. Kwa hiyo, naomba nichukue nafasi hii pia kuwapongeza *TRA* na Wizara ya Fedha kwa kazi nzuri ambazo wanafanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja, ahsante sana. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana, Mheshimiwa Daniel Nsanzugwanko atafuatiwa na Mheshimiwa Leah Komanya, Mheshimiwa Masoud Abdallah Salim ajiandae.

**MHE. DANIEL N. NSANZUGWANKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kwa namna ya pekee niunge mkono hoja hii na mapendekezo ya Waziri wa Fedha. Hata hivyo, naomba niwape hongera nyingi sana Waziri wa Fedha na timu yake kwa kazi nzuri wanayoifanya na hasa sera hizi za kodi za kuja na mkakati wa kulinda viwanda vya ndani na kuchochea uwekezaji katika Taifa letu, hilo ni jambo jema, hongereni sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini naomba pia kuwapa hongera sana wenzetu wa *TRA* kwa kubadilisha mtazamo (*attitudes*), wameanza kuwa *tax friendly* kwa walipa kodi. Ni kitu chema sana na Ndugu Kichere na wenzake hongereni kwa kazi nzuri, songeni mbele.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze na hili la mfumo mpya wa stempu za kodi za kielektroniki. Kwanza ni jambo jema, kama alivyosema ndugu yangu yule wa Kwimba na Mheshimiwa Waziri nadhani cha msingi hapa hebu rudini

kwenye meza tena muangalie hizo *economics* zake, haya yanayozungumzwa yana ukweli kiasi gani?

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia ni vyema Watanzania tusiogope mambo mapya. Mzee Dkt. Kikwete aliwahi kutueleza hapa kwamba ili ule lazima uliwe. Kwa hiyo, utaratibu huo wa stempu za kieletroniki uendelee lakini nimwombe tu Waziri wa Fedha na wenzake, warudi kwenye meza ya mazungumzo (*drawing board*) waangalie *economics* zake hizo. Hicho kinachosemwa kwamba watatupiga sana ni kitu cha kweli ili wajiridhishe na jambo hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nina ushauri katika suala hili la mifumo ya kutoza kodi. Wakati kampuni hiyo inafanya kazi hizi mngeifungamanisha na kampuni ya Kitanzania, hii Kampuni ya *Maxicom Africa*, hawa ni Watanzania, ni Waafrika wanaofanya kazi nzuri. Wamekubalika Uganda, Zambia, Rwanda na Kenya kwa washindani wetu wakubwa wa kibiashara. Kwa hiyo, ingekuwa jambo jema kwa miaka hii mitano muwafungamanishe na hii *local company* ili baadaye kazi hii iweze kufanywa na kampuni ya Watanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, nitakuwa na machache tu. Jambo ambalo napenda niliseme ni nidhamu ya kibajeti. Pamoja na mambo mazuri haya ambayo yamekuja kwenye bajeti hii ambayo ameyaainisha na mengine akayazungumza hata kwenye hali ya uchumi, nizungumzie nidhamu ya utekelezaji wa bajeti, hili ni jambo kubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukurasa wa 29 Mheshimiwa Waziri mwenyewe amebainisha kwamba kipaumbele kitakuwa ni ukamilishaji wa miradi inayoendelea. Sasa nimwombe sana miradi mipya isimame kwanza tukamilishe



miradi ya kielelezo ambayo imekwama ili tuwe na *consistency*.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini siyo hilo tu, kwenye hotuba pia ameanisha juu ya Waraka wa Hazina Na. 01 wa mwaka 2018/2019 ambapo anawaagiza Maafisa Masuuli wote watenge fedha za kutosha kwenye miradi inayoendelea. Narudia tena, miradi inayoendelea kabla ya kuanza mingine mipya. Sasa ipo miradi tunajua ya kielelezo, miradi ya kipaumbele tangu bajeti ya mwaka jana, hiyo miradi haijakamilika. Moja ya miradi hiyo muhimu ni miradi hii ya barabara ya kuunganisha mkoa na mkoa mwingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika nchi yetu mikoa ambayo haijaunganishwa kati ya mkoa mmoja na mwingine ni pamoja na Mkoa wa Kigoma. Mkoa wa Kigoma haujaunganishwa na Tabora, Katavi, Mwanza wala Shinyanga. Niombe sana kupitia Waraka Na. 01 aliouainisha Waziri kwenye hotuba yake katika ukurasa wa 29 basi miradi hii ambayo ina wakandarasi tayari kwenye maeneo mbalimbali ipewe kipaumbele na fedha ili ikamilike. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimkumbushe Mheshimiwa Waziri barabara muhimu sana katika nchi hii inayoitwa ya Kigoma – Kidahwe – Nyakanazi, hiyo ni barabara ya kielelezo imekaa miaka 20, bajeti zinakuja zinatoka barabara hii haijakamilika. Nimwombe Mheshimiwa Waziri naye aache *legacys* sasa kwamba barabara hii muhimu na kubwa katika nchi yetu inayotoka Kigoma - Nyakanazi haijakamilika. Nashauri Waziri akae na *TANROADS* na Katibu Mkuu wa Hazina, barabara hii ipewe fedha kwa sababu ni muhimu sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo napenda nilizungumze ni umeme. Umeme ni muhimu sana kwa maendeleo ya viwanda na hata hizi juhudi zinazofanywa za kujenga *Stiegler's Gorge* maana yake

umeme huu utaingizwa kwenye Gridi ya Taifa. Mimi nataka nimkumbushe Waziri kuna mikoa iko *off grid* na inahitaji kuendelea kiviwanda na moja ya mikoa hiyo ni pamoja na Mikoa wa Kigoma na Katavi. Napenda sana Mheshimiwa Waziri atakapokuja atueleze ule mkakati ambao Waziri wa Fedha mwenyewe alikwenda Korea kusaini pesa kwa ajili ya kitu kinachoitwa *North West Grid*, umeishia wapi? Kwa mradi ule Mikoa ya Geita, Kigoma, Katavi na Rukwa ingeunganishwa kwa Gridi ya Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, zaidi ya hayo, sisi ambao tuko *off grid* kuna Mradi mkubwa wa Kielelezo wa *Malagarasi Hydro Power* ambao una uwezo wa kuzalisha megawati 45. Naomba nimueleze Mheshimiwa Waziri wa Fedha, mradi huu ni muhimu sana na hii mikoa ambayo sisi tuko *off grid* lazima tupate *treatment* sawasawa kama mikoa ambayo ipo kwenye Gridi ya Taifa. Haiingii akilini mikoa ambayo ipo kwenye Gridi ya Taifa inanufaika na umeme mwingi wa kiviwanda lakini kuna mikoa ipo *off grid*. Bahati nzuri sana sisi Mkoa wa Kigoma tuna umeme wetu huu wa Malagarasi wa megawati 45.4, nina uhakika umeme huu utasaidia sana pia kuchochea maendeleo ya viwanda katika Mkoa wa Kigoma na maeneo ya jirani.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, naomba nizungumzie uimarishaji wa ushirikiano na washirika wa maendeleo. Liko jambo ambalo ningependa Mheshimiwa Waziri atueleze, washirika wa maendeleo, Jumuiya ya Nchi za Ulaya, *USAID* na *World Bank* wana malalamiko makubwa na wamekuja kwenye Kamati zetu kutueleza kwamba Serikali mpaka tarehe 12 Juni kulikuwa na fedha shilingi bilioni 700 ambazo ni sawa na *USD* milioni 300, Serikali imeshindwa kusaini *MoU*. Mheshimiwa Waziri wa Fedha, ni kitu gani hiki? Naomba aje atueleze tatizo liko wapi? Mfumo wa majadiliano ni wa kimkakati, kisera na kisiasa, zungumzeni na watu hawa tupate fedha hizi.

*(Hapa kengele ililia kuashiria  
kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Nsanzugwanko, muda wako umekwisha.

**MHE. DANIEL N. NSANZUGWANKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru, naunga mkono hoja lakini Waziri aje atueleze juu ya jambo hili muhimu sana, ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Leah Komanya atafuatiwa na Mheshimiwa Masoud Abdallah Salim na Mheshimiwa Magdalena Sakaya ajiandae.

**MHE. LEAH J. KOMANYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipatia nafasi na mimi niweze kutoa maoni yangu katika mpango wa bajeti.

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, napenda kuipongeza Wizara ya Fedha kwa namna ilivyotuletea mpango na kwa jinsi ilivyojikita zaidi kufuta tozo au kodi zilizokuwa kero kwa wananchi, naipongeza sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla ya kuanza mchango wangu, naipongeza Serikali kwa namna ilivyoanza kulifufua zao la pamba kiasi kwamba sasa kumeanza kuwepo matumaini kwa wakulima wa pamba katika Mkoa wa Simiyu na Kanda ya Ziwa kwa ujumla. Naipongeza Serikali kwa kufuta mchango uliokuwa ukitozwa, Sh.30 kwa kila kilo kwa ajili ya kuendeleza zao la pamba. Mchango huu haukuwa na tija kwa sababu Mfuko huu ambao unajulikana kama *CDTF* haukuwa na tija yoyote, haukuweza kumsaidia mkulima na badala yake uliendelea kuleta pembejeo hafifu na uzalishaji uliendelea kupungua. Kwa mfano, takwimu za msimu 2015/2016, zilikuwa tani 149,000 na kupungua zaidi katika msimu wa 2016/2017 ambapo zilivunwa tani 121,000. Kwa hiyo, hakukua na tija yoyote kuwepo kwa mfuko huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naamini kazi zilizokuwa zinafanywa na Mfuko huu zitafanywa na Bodi ya Pamba kwa kushirikiana na Maafisa Kilimo walioko katika halmashauri zetu. Kwa sababu muda wote ule kulikuwa na mgongano wa maslahi, mkulima alikuwa anamfahamu tu Bodi ya Pamba pamoja na Mfuko ule kwa sababu ndo uliokuwa unapelekea pembejeo ya mbegu na dawa kiasi kwamba Afisa Kilimo hakupewa nguvu yoyote au hakuthaminika kwa mkulima kuweza kulisimamia zao hilo kikamilifu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nina shauri sasa Serikali kupitia halmashauri iwawezeshe Maafisa Kilimo kikamilifu kwa sababu kila Kata kuna Afisa Kilimo. Iwawezeshe usafiri na iwawezeshe kwa namna yoyote ili waweze kulisimamia lile zao badala ya Bodi ya Pamba ambayo ina mtu mmoja tu katika Wilaya ndiyo aliyekuwa anasimamia zao hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niendeleo kuipongeza Serikali kwa kufufua ushirika na kwa msimu huu imeanza kununua pamba kupitia vyama vya ushirika. Nafahamu mwanzo ni mgumu, sisi Wabunge tuko nyuma yenu, tunamshukuru sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa jitihada zote anazozifanya kulisimamia hili zao. Mheshimiwa Waziri Mkuu mimi niko nyuma yako nitaendelea kukupa ushirikiano ambao ninaweza kukupa ili kuweza kufikia malengo ambayo Serikali inatoa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naamini sasa zao hili linaenda kuwa mikononi mwa Serikali, Serikali itakuwa na uwezo wa kuweza kulitolea maamuzi yoyote tofauti na ilivyokuwa mwanzo. Naamini sasa vile vyama vinaibuka na kutoza hela kwenye ushuru huo sasa vinaenda kujifuta vyenyewe kupitia ushirika. Halmashauri za Wilaya zinaenda kupata takwimu sahihi kwa ajili ya kutoza ushuru wa pamba. Nachoshauri vile vitabu vinavyotumika Wakurugenzi waone kwamba ni nyaraka muhimu kwa sababu zinaenda kutumika kukokotoa kupata takwimu sahihi badala ya ule mgongano uliokuwepo baina ya Halmashauri na Bodi ya Pamba.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini tatizo lililopo hatuna Maafisa Ushirika wa kutosha. Halmashauri zetu zina Afisa Ushirika mmoja mmoja wengine wanaenda kustaafu mwezi wa sita. Kwa kipindi hiki cha mpito Maafisa Ushirika ni wa umuhimu kwa ajili ya kufufua ushirika, kwa sababu mara tu baada ya msimu ukaguzi unatakiwa ufanyike mara moja ili vyama vya ushirika vijijendeshe kwa faida. Bila Maafisa Ushirika tunaenda kurudi nyuma, mapato yanayotokana na ushirika kwa vyama vya ushirika hayatajulikana badala yake tutaendelea kutengeneza hasara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi hiki ni muhimu sasa kuwezesha kuwepo kwa COASCO kwa ajili ya ukaguzi ili baadaye tusirudi kule tulikotoka. Kwa mfano, Wilaya ya Meatu ina AMCOS 80, ina vituo vya kununulia pamba 200, lakini Afisa Ushirika aliyepo ni mmoja. Je, ni nani anaenda kukagua mapato na matumizi ya vyama vya ushirika? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niendeleo kuipongeza Serikali kwa kufuta Kodi ya Ongezeko la Thamani katika taulo zinazotumiwa na akina mama na wasichana wakati wa hedhi,. Kufuta tozo hiyo inaenda kumpunguzia mwanamke mzigo kwa kiasi fulani. Naishauri Serikali bado ina nafasi kubwa ya kumsaidia mwanamke kupunguziwa bei ya taulo hizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano, nikiangalia pedi nyingi zinatoka nje, sisi Tanzania tunatumika kama wasambazaji, pamba inayozalishwa asilimia 30 tu ndio inayotumika nchini asilimia 70 inaenda nje. Hii inamaanisha kwamba hatuna viwanda vya kutosha vinavyoweza pia kutengeneza pedi. Hata pedi tunazotengeneza nchini pamba inayotumika inaenda nje kwanza ndipo inarudi Tanzania kwa ajili ya kutengeneza. Kwa hiyo, Serikali inalo jukumu kubwa la kuhakikisha sasa tunakuwa na viwanda vya kutosha ili sasa asilimia kubwa ya pamba iweze kutumika nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mpango wa Serikali katika ukurasa wa 85 umesema kwamba unaongeza uzalishaji wa mbegu bora za pamba aina ya UKM09 tani 40,000. Pia, inaenda kutenga maeneo kwa ajili ya uzalishaji wa mbegu hiyo; kutoa elimu kwa ajili ya wakulima; na kutoa vitendea kazi na kuhamasisha wakulima. Ukiangalia mikoa iliyotajwa Simiyu haijatajwa kama inaenda kuwezesha na hapo hapo Serikali imepanga shilingi bilioni 6.1 kwa ajili ya kutekeleza zoezi hilo. Ukiangalia Mkoa wa Simiyu pia asilimia 60 ya pamba inayozalishwa nchini inatoka Mkoa wa Simiyu. Kwa hiyo, naiomba Serikali Mkoa wa Simiyu na wenyewe uwemo katika kuwezesha kwa namna Serikali ilivyojipanga kuwezesha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mkoa wa Simiyu unacho kituo...

*(Hapa kengele illia kuashiria  
kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Muda wako umekwisha Mheshimiwa.

**MHE. LEAH J. KOMANYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Masoud Abdalla Salim, atafuatiwa na Mheshimiwa Magdalena Sakaya, Mheshimiwa Cecilia Paresso ajiandae.

**MHE. MASOUD ABDALLAH SALIM:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushuru, kama Serikali inataka kuambiwa ukweli ili ijirekebishe bajeti ya 2018/2019 ni bajeti ya kuwadanganya Watanzania, ya kufikirika, ya kusadikika na isiyo tekelezeka. Ni bajeti ambayo kwa kweli imewahadaa Watanzania na hasa wakulima. Ikiwa leo wakulima wametengewa asilimia 0.4 ya fedha za maendeleo ndani ya fedha za bajeti ya maendeleo ya shilingi trilioni 12 ukiachia shilingi trilioni 2.1 fedha za nje, hivi Tanzania ya viwanda kuelekea uchumi wa kati ni kweli inawezekana? Mnawadharau wakulima tangu bajeti iliyopita mwaka 2017/2018 walitengewa shilingi bilioni

150.2 mkapeleka shilingi bilioni 16.5 hadi mwezi Machi sawa na asilimia 11, Tanzania ya viwanda iko wapi? Mmewatelekeza wavuvi, leo wavuvi bajeti ya maendeleo kwa mwaka huu mmetenga 0.06 ndani ya shilingi trilioni hizo ambazo nimezitaja. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli Serikali kama inataka kuambiwa ukweli ni kwamba wavuvi wametelekezwa, wakulima wametelekezwa na mifugo imetelekezwa. Sasa nauliza mkakati wenu wa Serikali wa kuboresha uvuvi uko wapi, hauonekani. Wananchi wa Mtwara, Lindi, Dar es Salaam mpaka Tanga mkakati wa kuboresha maisha yao uko wapi? Kwenye maziwa nako vilevile, Mikoa ambayo iko katika Ziwa Viktoria, Ziwa Tanganyika na maziwa mengine, yote hakuna mkakati, bajeti yao ni 0.06 ya fedha za maendeleo, ina maana Serikali haina mkakati. Mkakati mkubwa unaojulikana ni kuchoma nyavu moto na kupeleka wapimaji wa samaki kantini, tutafika kweli? (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nashangaa kweli kweli, ukiangalia Vote 99, *Ministry of Livestock Development and Fisheries Livestock, Subvote 1001, item 22010 Travel-In-Country*, hii ndiyo Waziri mwenyewe, wametoka kwenye Sh.108,960,000 hadi shilingi milioni 300 safari za ndani kumbe ni za kuchoma nyavu moto na kupima kantini samaki wa Bunge. Hili halikubaliki lazima tubadilike tuendane na wakati ulivyo kwamba wavuvi mmewaacha kuendelea kuwa maskini, nchi nyingine duniani wanaandaa mazingira mazuri kuwawezesha wavuvi wadogo wadogo kutafuta vyombo mbalimbali baadaye wanakwenda kuvua bahari kuu na Serikali inapata mapato, lakini nyie mkiambiwa mnasema sisi siyo wazalendo, hatuwezi kufika. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, nigusie jambo lingine, nimesema bajeti hii ni kiini macho, ni kizungumkutu kwa sababu kwenye ukurasa 78 hakuna uhalisia wa ukweli wa matumizi ya lazima yanayoendana na mapato. Deni la Taifa ni shilingi trilioni 10 kwa hivyo kwa kila mwezi zinatakiwa zipatikane shilingi bilioni 833, ukienda kwenye mishahara

shilingi trilioni 7.4 kwa kila mwezi lazima zipataki shilingi bilioni 617, matumizi mengineyo ni shilingi bilioni 3, kila mwezi ipatikane shilingi bilioni 254, shilingi trilioni 1.7 mtaipata wapi na hamna makusanyo? Tukisema vyanzo chukueni vyanzo hamtaki, hamueleweki. Amesema Mheshimiwa mmoja pale Mheshimiwa Mgimwa, kwamba Waziri usiwe mgumu ukubali ushauri wa Waheshimiwa Wabunge. Ikiwa makusanyo ya mwisho ni shilingi trilioni 1.2 mpaka 3, leo mnataka ipatikane shilingi trilioni 1.7 ya lazima, hamna kitu. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, tena basi angalia ukurasa wa 74 wa kitabu chao kuna shilingi trilioni 12 hizi ni fedha za maendeleo ukiachia shilingi trilioni 2.1 ya fedha za nje. Bado haijakuja hapo, nazo zikusanywe shughuli iende. Ukiangalia kitabu cha Mheshimiwa Mpango na mwenzake Naibu Waziri picha ya juu hapa wanasema, uzinduzi wa mfumo wa ukusanyaji wa mapato kwa njia ya kielekitroniki, uzinduzi lakini hawawezi kumuonesha Rais, tena Rais yupo hapa Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli, muonesheni Rais vyanzo vipya vya mapato mbona hamumuoneshi? Kuna picha hapa, nawashangaa kweli kweli, andaeni mazingira, njia mpya ya mapato iko wapi, uzinduzi wa vyanzo vipya vya mapato iko wapi? Ni vilevile vya siku zote hivyo ni kuwaumiza wananchi, hamsomeki hamueleweke shauri yenu. (Makofi/Kicheko)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo linanikera Serikali hii hakuna ongezeko la mshahara, bajeti hii haijagusa kabisa wafanyakazi, hakuna nyongeza yao. Hata lile takwa la kisheria la nyongeza ya kila mwezi nalo haliko, *annual increment* hakuna. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo baya zaidi ni kwamba ukiangalia ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali mbali na kwamba mishahara haikupandishwa, hakuna ile *annual increment* ile ya mfanyakazi ambayo ni ya kisheria haipo lakini hata pale wanapostaafu hawa wafanyakazi wanapunjwa, wanadhulumiwa na kunyonywa nakupa ushahidi. Ripoti ya Mdhibiti ninayo hapa, ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa mwaka



wa fedha unaoishia 30 Juni, 2017, ukurasa wa 71 sikiliza uovu na ubaya walionao hawa jamaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ukurasa wa 71, majalada yanayokaguliwa wastaafu 406 asilimia 11 ya majalada, majalada hayo 176 yamepunjwa yakiwa pungufu kwa Sh.516,078,816. Hiyo ndiyo ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi wa Hesabu za Serikali, mishahara haipandishi, hakuna ongezeko la mwaka la kisheria na wale wanaostaafu nao wanapunjwa mnataka nini kwa Mungu, mkaseme nini? Nawashangaa jamani mwogopeni Mwenyezi Mungu, nyie tumewapa kazi ya kusimamia kwamba hata wastaafu nao kumbe maslahi yao wanayopata mafao yao siyo, mwaka mabaya kweli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niwaambie Waheshimiwa wenzangu hapa kwamba jukumu mlilopewa ni kubwa sana na kama jukumu mlilopewa ni kubwa sana muandae mazingira kwamba mtende haki. Siyo hiyo tu, huu wizi na ubadhirifu katika nidhamu ya matumizi ya fedha umekuwa mkubwa sana na inaelekea kwamba Mawaziri wameshindwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia kitabu hiki hapa kuna wizi na ubadhirifu unaonekana. La kwanza, naomba nianze na kwenye ukurasa wa 291 wa ripoti na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali. Katika ukurasa huu inaonekana kwamba hata Hazina yenyewe chombo ambacho wanakisimamia, Idara ya Hazina Fungu 21 kuna ubadhirifu mkubwa wa fedha umeonekana na wao ndiyo wasimamizi. Ukurasa wa 291 Naibu Waziri fungua uangalie lakini ukusara wa 290 pia mmepata hati isiyo na shaka, ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kumbe ukiona kilemba kimeloa uchafu sijui shuka inakuwaje? Mtihani, tumewapa dhamana lakini hakuna kitu. Maisha yamekuwa magumu, mzunguko wa pesa hakuna. Mwaka 2017 baya zaidi, hii hapa hotuba ya Mheshimiwa Dkt. Mpango alituambia kwamba lengo lake ni kuwatoa wale wanaokula mlo mmoja kutoka

asilimia 9.7 mpaka asilimia 5, nendeni Majimbo Wabunge wote hapa tuandae vikundi twende Mikoa yote Tanzania Bara tukachunguze wanaokula mlo mmoja wameongezeka au wamepungua?

**WABUNGE FULANI:** Hawajapungua.

**MHE. MASOUD ABDALLAH SALIM:** Hali mbaya kupita kiasi. Sasa yale maelezo ambayo mnatupa siye tunayasoma na tunayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri akubali kwamba bado hali ya maisha ya Tanzania ni mbaya sana na Watanzania wana matumaini makubwa sana lakini hakuna kinachoeleweka, mpaka sasa hakuna kinachokwenda. Ushauri wangu kwa Mheshimiwa Waziri, akae na wataalam wa kweli ambao wataweza kusadia hii Wizara angalau maisha ya Watanzania yabadilike lakini kwa hali tunayokwenda nayo Watanzania tumepigika. Bajeti hii ni mbaya, mbovu, ya kusadikika, funika kombe. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria  
kwishwa kwa muda wa mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Masoud, hata ile asilimia karibia 70 ya mwaka jana haujaiona kabisa, ni *zero*?

Tunaendelea na Mheshimiwa Magdalena Sakaya atafuatiwa na Mheshimiwa Cecilia Paresso, Mheshimiwa Susan Kiwanga ajiandae.

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nami nakushukuru sana kunipa nafasi niweze kuchangia kidogo kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri, hotuba ya Serikali ambayo iko mbele yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye vitabu vyote vya Mheshimiwa Waziri; kitabu cha hotuba hata kitabu cha hali ya uchumi wa Taifa, uchumi wa Tanzania umekua kwa asilimia 7.1 tofauti na mwaka 2017 ambapo ulikua kwa asilimia 7

mwaka 2016. Ukijaribu kuangalia hivi vitabu vinavyosema na ukienda kwenye *actual ground* kule chini kwenye maisha ya watu ni tofauti sana. Uchumi tunaosema kwamba umekua kwenye vitabu kule chini bado hauendani. Nami nakubaliana kabisa na hotuba ya Kamati kwamba tumeshindwa kuoanisha uchumi na hali ya wananchi kule chini, tumeshindwa kuoanisha kukua kwa uchumi kwa kufungamanisha na hali ya maisha ya Watanzania kule waliko chini. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi tunavyoongea kilo ya dagaa Sh.10,000 tena wa Mwanza. Hivi tunavyoongea jana sato Sh.10,000 kilo moja hata hapa kantini tunakula haijalishi ni mdogo au mkubwa. Ukiondoa mazao ya nafaka, mazao mengine yote gharama ni juu. Kwa hiyo, kwa mwananchi wa kawaida ukimwambia uchumi umekua hakuelewi. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini tukienda pia kwenye vifaa vya ujenzi, *cement* wiki iliyopita ilikuwa Sh.14,500 leo asubuhi ni Sh.15,500. Sasa uchumi umekua umekuaje? Miezi miwili iliyopita nondo milimita 16 ilikuwa Sh.19,500 mpaka Sh.20,000 leo nenda duka la dawa vifaa vya ujenzi ni Sh.38,000 imepanda *almost* mara mbili. Nashindwa kuelewa, mimi siyo mchumi ni mtu wa maliasili na mazingira, Waziri atuambie uchumi ukikua unaupima wapi? Unaupima juu au kule kwa wananchi walioko kule chini? (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, naishauri Serikali lazima tuhakikishe kukua kwa uchumi kunaendana na hali kule chini. Hivi tunavyoongea watu wanazidi kuuza mashamba na viwanja vyao, mabenki yanatangaza kila siku kapiga minada nyumba za watu, watu wameacha kukaa kwenye nyumba zao walizokuwa wamejenga wameziuza wameenda kupanga nyumba, sasa hii kusema uchumi umepanda umepandaje? Kiukweli kusema uchumi umepanda wakati hatuoni huko chini tunaishi na wananchi bado kuna walakini mkubwa sana. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ni uzalishaji wa mazao. Ukienda kwenye Kitabu cha Hali ya Uchumi kwenye *page* 134, kuna baadhi ya mazao ambayo siku za nyuma ndiyo yalisaidia uchumi wa Taifa hili kukua ikiwemo kahawa, pareto, katani, tumbaku, mkonge, pamba, korosho na chai. Leo ukisoma kitabu kinasema mazao haya yamepungua tena kwa asilimia kubwa na sababu zilizotolewa hapa ni kwamba, kwanza mvua za kutosha zimekosekana lakini pili, wakulima wameshindwa kununua pembejeo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tunazungumzia habari ya uchumi wa viwanda, bado tunategemea mvua ambazo hazina uhakika. Hatuwezi kuzungumzia uchumi wa viwanda wakati mazao ambayo yalikuwa yanainua uchumi wa Taifa hili, ukisikia Kagera wameendelea ujue ilikuwa ni ndizi na kahawa; Kilimanjaro wameendelea ni kahawa, kule Mbeya cocoa, Tanga viwanda vilikuwa zaidi ya mia ni katani ilisaidia sasa leo yale mazao hayapo, yamekuwa ni mapori, tunazungumzia habari ya uchumi wa viwanda, vinatoka wapi hivyo viwanda? Kwa hiyo, tukitaka kwenda kwenye uchumi wa viwanda lazima tujizatiti kwenye kilimo cha umwagiliaji. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tulikubaliana miaka mitano iliyopita kwamba tutahakikisha tuna angalau hekta 1,000 za umwagiliaji. Kwenye hotuba ya Waziri wa sekta nilisoma mpaka sasa hivi ni hekta 460,000 hata nusu kwa miaka mitano hatujafika, hatuwezi kwenda na leo tena mabadiliko ya tabianchi, *global warming* na mambo mengine mengi. Kwa hiyo, hatuwezi kwenda kwenye uchumi huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini sababu ya pili tumeambiwa ni wakulima kushindwa kutumia pambejeo. Zao kama kahawa leo ukisema mkulima anunue pembejeo hawezi, ni *very expensive*. Kwa hiyo, kwenye mzao kama haya lazima Serikali itoe ruzuku kuwaachia wakulima ni vigumu. Wengine wanang'oa wanapanda maharage, migomba kwa sababu hawawezi kuendelea kumudu kununua pambejeo. Kwa hiyo, naomba tuangalie historia ya nyuma, Mwalimu

Nyerere alifanya kazi kubwa sana, mazao ambayo ndiyo yalikuwa kielelezo cha Taifa letu tusiyaache. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini hata kwa mazao ambayo yapo sasa hivi, kwa mfano, suala la tumbaku Mkoa wa Tabora tunalima lakini bado wakulima wake wameendelea kuwa maskini. Bei za mazao yetu bado ni tatizo. Hivi navyoongea masoko ya jana na juzi bei imeshuka kutoka Sh.4,000 mpaka Sh.4,500 kwa kila sasa wanauza kilo nzima ya tumbaku kwa Sh.181, hayo ni masoko ya jana. Sasa mkulima kama huyu ambaye amenunua pembejeo kwa Sh.90,000 mfuko mmoja wa kilo 50 mpaka Sh.140,000 kwa wale waliokosa ruzuku lakini bei ya Serikali Sh.90,000, mkulima huyu akauze tumbaku Sh.181 wakati amekwenda kukopa benki, anadaiwa kwenye taasisi za fedha, ananyanyukaje huyu? Kwa hiyo, hata kwa mazao ambayo yanasaidia bado Serikali hatujaweza kusimamia bei nzuri ya mazao yetu, hili ni tatizo kubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine, Mkoa wa Tabora umelima tumbaku lakini bado kiwanda kipo Morogoro. Tumepiga kelele sana hapa kwa nini Kiwanda cha Tumbaku hakijengwi Mkoa wa Tabora? Majibu tunaambiwa kwamba tunatafuta wawekezaji lakini juzi mwaka uliopita amekuja mwekezaji wa Kiwanda kingine cha Tumbaku amejenga Morogoro. Naomba Serikali na Waziri aje na majibu, tunataka Kiwanda cha Tumbaku kiende kikajengwe Mkoa wa Tabora na mtuambie namna gani mtafanya kiwanda kile kiweze kujengwa vinginevyo kiukweli vijana wale hawana ajira lakini tumbaku inalimwa kwao tena asilimia 60 ya tumbaku ya Tanzania inalimwa pale Mkoa wa Tabora. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ukienda kwenye kitabu pia cha Mheshimiwa Waziri ukurasa wa 92 utaona namna gani ambapo tunaingiza sana bidhaa ndani kuliko kupeleka nje kwa hiyo, tunauza kidogo, tunaingiza sana, hili ni tatizo. Kuna vitu vingine ambavyo hatuhitaji kuingiza kutoka nje, kwa mfano, *toothpick*, pamba za kwenye masikio, viberiti lakini

tuna-*import* kutoka nje, fedha tunayokusanya tunapeleka nje kutengeneza ajira kwa vijana wao, sisi tunabaki ni masoko ya bidhaa za wenzetu, hatuwezi kupiga hatua, hili ni tatizo kubwa sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mkoa wa Tabora tunalima mbao, tena *quality* mbao, mninga na mpogo safi unaupata Tabora. Serikali ilisema itahakikisha samani zote za Serikali zinatoka ndani ya nchi lakini leo tunapeleka magogo, mbao, Wachina wanakwenda kuchukua, tunakwenda kununua bidhaa za Kichina *very weak*, hazina ubora kwa gharama kubwa. Kwa nini Serikali inashindwa kusimamia vitu ambavyo tunaweza kutengeneza hapa ndani ya nchi? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi kweli kwa ule Msitu wa *Sao Hill* pale Iringa, kuna haja ya kwenda kununua kiberiti nje? Hata mtoto wa darasa la saba anatengeneza kiberiti, hata mtoto wa darasa la pili anatengeneza *toothpick*, tunayo pamba, vitu vingine ni sisi tunajitakia. Fedha ambayo tunaipeleka nje inakwenda kujenga kule nje kumbe tunaweza tukaitumia ndani ya nchi yetu ikazunguka humu humu, tuka-*invest* ndani ya nchi yetu. Kitendo cha Serikali kuruhusu hata vitu vidogo vidogo vikaingizwa ndani ya nchi ni kushindwa kusimamia nchi yetu lakini pia ni kushindwa kusimamia namna gani vijana wetu wapate ajira, tuna-*create* ajira kwa Wachina na kwa wengine huku vijana wetu wakiwa watanga tanga bila ya kuwa na ajira. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika...

*(Hapa kengele ililia kuashiria  
kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Muda wako umekwisha Mheshimiwa, ahsante.

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Cecilia Pareeso atafuatiwa na Mheshimiwa Susan Kiwanga, Mheshimiwa Mwita Mwikabe Waitara ajiandae.

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi niweze kuchangia katika hoja iliyoletwa mezani kuhusu Bajeti Kuu ya Serikali ya mwaka 2018/2019.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeeleza vipaumbele vitatu ikiwemo kilimo, viwanda, huduma za jamii kwa maana ya maji, elimu na afya. Mimi nitachangia katika suala la kilimo na elimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ya CCM toka tumepata uhuru wananchi hii imekuwa na kaulimbiu na mikakati mingi kuhusiana na sekta ya kilimo. Tulikuwa na kaulimbiu na mikakati mingi ikiwemo, Siasa ni Kilimo ya mwaka 1974, Azimio la Arusha la mwaka 1967, Azimio la Iringa mwaka 1974 lakini hata mwaka 2009 tulikuja na Kilimo Kwanza na Serikali ya Awamu ya Nne pia katika *Big Results Now*, sekta ya kilimo na yenyewe iliongezewa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hakuna ambaye anapinga umuhimu wa sekta ya kilimo kwa Watanzania. Nilipochangia Wizara ya Kilimo hapa nilieleza umuhimu wa sekta ya kilimo kwamba inaajiri nguvu kazi asilimia 65 ya Watanzania, inachangia asilimia 30 kwenye pato la Taifa, malighafi viwandani asilimia 65 inatoka sekta ya kilimo na asilimia 100 ya chakula hapa nchini inatoka kwenye sekta ya kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika malengo ya MKUKUTA ya miaka 10, ilijiwekea mkakati wa ukuaji wa sekta ya kilimo angalau kwa asilimia 6 mpaka asilimia 8. Ukuaji wa sekta ya kilimo kwa miaka mitano kuanzia mwaka 2011 mpaka 2015 umekua kwa asilimia 3.4 tu. Hata hivyo, toka Serikali ya Awamu ya Tano iingie madarakani, Serikali ya Hapa Kazi, Serikali ambayo inataka kutupeleka kwenye uchumi wa Kati, Serikali inayojiita ya viwanda, ukuaji wa sekta ya kilimo

pamoja na umuhimu wake wote umeshuka ukilinganisha na Serikali ya Awamu ya Nne ilivyokuwa madarakani. Ukuaji wa sekta ya kilimo umekua kwa asilimia 1.9 tu toka mwaka 2016 mpaka 2017. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, bajeti ambazo tumekuwa tukizipitisha hapa Bungeni kwenye sekta ya kilimo imekuwa haifiki kwenye Wizara, hazitolewi kwa wakati. Mwaka 2016/2017 tulipitisha Bungeni hapa shilingi bilioni 100 zilizotolewa ni shilingi bilioni 2 tu fedha za maendeleo ni sawasawa na asilimia 2.2. Mwaka 2017/2018 sekta ya kilimo ilitengewa shilingi bilioni 150 zilizotolewa ni shilingi bilioni 16.5 sawasawa na asilimia 11 na mwaka huu fedha zilizoombwa kwenye sekta ya kilimo kwa maana ya Wizara ya Kilimo zitakazotekeleza miradi ya maendeleo ni shilingi bilioni 98.1. Tunawashangaa sana kila siku Serikali iliyoko madarakani, pamoja na kaulimbiu zenu na mikakati yenu mnayosema kwenye vitabu lakini sekta ya kilimo ambayo tunaitegemea sisi Watanzania tulio wengi, mmeendelea kutoipa kipaumbele na kutoona umuhimu wa sekta ya kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ukifanya uwiano kati ya bajeti kuu ya Serikali na sekta ya kilimo, mwaka 2016/2017 uwiano kati ya bajeti kuu na sekta ya kilimo kama ambavyo mmesaini Maazimio mbalimbali ya Kimataifa ni asilimia 0.93, mwaka 2017/2018 ni asilimia 0.85, mwaka 2018/2019 ni asilimia 0.52 na mwaka huu imeshuka zaidi ukilinganisha na miaka mingine. Sasa tunajuliza mmesema mtaweka kipaumbele chenu cha kwanza ni sekta ya kilimo lakini sekta hiyo hiyo ya kilimo hamuipi fedha, mmewasahau Watanzania wakulima walio wengi, tutawaaminije? Mbona mmetudanganya miaka mingi sana? Mmekuwa wazuri kwenye maandishi, kwenye vitabu lakini kuja kwenye utekelezaji mmekuwa tofauti kabisa. Kwa kweli nirudie kusema, wakulima wa nchi hii adui yenu namba moja ni Serikai iliyopo madarakani kwa mikakati na sera mbovu ambazo hazitekelezeki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kutuambia kwamba kwenye bajeti hii kipaumbele ni kilimo lakini miaka



iliyopita, mavuno ya mwaka juzi, wakulima mbaazi tu imewasumbua mpaka leo, kupata masoko ya wakulima wetu mbaazi ni mtihani, korosho ni mtihani, pamba ni mtihani yaani hakuna ambako afadhali, tumbaku ni mtihani, mahindi imewasumbua mwaka mzima yanawahangaisha mnakataza vibali, mnageuka kwa nyuma mnaruhusu vibali. Kahawa imewasumbua, pamba, mkonge, mazao mchanganyiko hakuna mkulima wa nchi anayelima zao lolote ambaye ana uhakika wa soko. Sasa mnasema kipaumbele ni kilimo mnawahakikishiaje Watanzania wakulima kuwa na uhakika wa masoko? Nini mkakati kwenye bajeti hii kuhakikisha wakulima wana masoko ya kutosha? Tunaomba majibu Mheshimiwa Waziri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie kuhusu sekta ya elimu. Serikali ya Awamu ya Tano mmesema mnatoa elimu bure na Serikali ya Awamu ya Nne iliona kutoa elimu bure ni changamoto, ikaona namna bora ni kusaidiana na wazazi kuhakikisha wanakabiliana na upungufu mbalimbali kwenye sekta ya elimu ikiwemo miundombinu na changamoto nyingi katika shule zetu za msingi na sekondari hapa nchini. Ninyi mmekuja, mmefuta michango, mnasema elimu ni bure, Mheshimiwa Waziri kwenye mambo yako 10 uliyoyataja hapa ya kumsifia Rais Magufuli umeelezea suala la elimu bure, nataka nikwambie elimu bure imekuwa na changamoto kubwa, mnaua sekta ya elimu kuliko hata Serikali ya Awamu ya Nne ilivyokuwa madarakani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nitoe takwimu, upungufu wa walimu, shule za msingi, mwaka 2016 upungufu ulikuwa 191,772 mwaka 2017 upungufu umeongezeka umefika 179,291; shule za awali, upungufu wa walimu umekuwa 1,948; shule za sekondari masomo ya hisabati upungufu wa walimu ni 7,000, baiolojia 5,000, kemia 5,000, na fizikia 6,000. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, upungufu wa miundombinu; upungufu wa maktaba...

**T A A R I F A**

**NAIBU WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Umeongezeka...

**NAIBU WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa

**WABUNGE FULANI:** Mheshimiwa Kandege, si utajibu baadaye.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Paresso, kuna taarifa.

**NAIBU WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, naheshimu sana mchango wa Mheshimiwa lakini ni vizuri tukapeana taarifa; angekuwa anakwenda na takwimu walikuwa wanafunzi wangapi na ongezeko limekuwa kiasi gani ndiyo unafanya *comparison*. Ukitazama ongezeko la wanafunzi huwezi ukasema kwamba kuna pungufu, ni vizuri akaenda na hiyo taarifa ili asije akawapotosha wananchi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Cecilia Paresso, unaipokea taarifa hiyo?

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Mheshimiwa Naibu Spika, siipokei hiyo taarifa na kitu ambacho nafikiri Serikali mnakosea sana, mnapima mafanikio ya elimu bora na idadi ya uandikishwaji siyo *quality* na hiki kitu mmekuwa mnakisema siku nyingi. Pia idadi ya wanafunzi wanaondikishwa inawezekana ikaongezeka kwa sababu ya uzao, *birth rate* nayo inawezekana ikawa inaongezeka, *population* inaongezeka, sasa mnapimaje hayo? Mheshimiwa Naibu

Waziri utapata nafasi baadaye na wewe utasema ya kwako.  
(Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, upungufu wa maktaba; mwaka 2016 upungufu ulikuwa ni asilimia 88, mwaka 2017 upungufu umekuwa ni asilimia 91. Maana yake badala ya kwenda mbele kupunguza changamoto mbalimbali za kimiundombinu tunarudi nyuma hatua kadhaa haya matatizo yanazidi kuongezeka. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, maabara; upungufu wa maabara ya baiolojia ni asilimia 51, fizikia 54 na kemia 53. Upungufu wa madawati ni milioni 1,170,000 na upungufu wa walimu ni 186,000. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, tunajuliza, mnatuambia elimu bure, elimu hii siyo bure, mnakwenda kuua Taifa la kesho. Badala tuliandae Taifa la kesho, mnajua umuhimu wa elimu ni kuandaa rasilimali watu, kuliandaa Taifa, tuwe na wataalam na wajuzi wa kutosha, tuandae mazingira ya kufikia haya, tunatengeneza mazingira mabovu ya kuwa na elimu mbovu ya kuiangamiza nchi hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. (Makofi)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Susan Kiwanga atafuatiwa na Mheshimiwa Mwita Waitara, Mheshimiwa Mussa Ramadhan Sima ajiande.

**MHE. SUSAN L. KIWANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii adhimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze na kitabu hiki cha Waziri, ukurasa wa 11 anazungumzia wastani wa pato la Taifa la kila mtu, anasema kwamba wastani wa kila mtu kwa mwaka 2017 ni sawa na dola za Kimarekani 1,021 ukilinganishana na mwaka 2016 ni dola 958 kwa mwaka, kwa hiyo anasema umekua. Sasa swali langu, mlishawahi kupandisha mishahara? Hawa watumishi katika nchi hii wastani wao wa pato la Taifa umepanda au umesimama

pale pale? Kwa hiyo, hapa kipato chako kinatudanganya? Hawa watumishi ambao hamuwapandishi mishahara pamoja na sisi Wabunge mnasema wastani kwa dola ya Kimarekani 1,021 badala ya dola 958 huo ni uwongo wa mchana kweupe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, watumishi wanapata wapi hela nyingine, wanakula rushwa mpaka mnawapima wastani wao wa kipato kwa mwaka? Tusidanganyane. Yaani ninyi wataalam wa kuandika hivi vitabu, mnaandika peke yenu halafu mnatuletea hapa, mnawadanganya Watanzania, wastani haujakua, hivyo ni vitabu tu lakini hali halisi sifuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naenda sasa kwenye bajeti kuhusu kilimo maana mimi ni mtoto wa mkulima na naishi kwa kutegemea kilimo. Bajeti ya mwaka 2016/2017, Bunge hili tuliidhinisha bajeti ya kilimo shilingi bilioni 100.5 lakini hela zilizotolewa kwenye kilimo ni shilingi bilioni 2.252 halafu unasema pato limekua, limekua kwa nani? Labda kwako wewe lakini kwa Watanzania wa kawaida na wananchi wa Mlimba halijakua chochote, bado wanarudi nyuma badala ya kusonga mbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Kilimo mwaka 2017/2018, Bunge hili tuliidhinisha kwenye bajeti shilingi bilioni 150.25 na sifuri sifuri huko, lakini hadi kufikia Machi mwaka huu pesa zilizotoka za miradi ya maendeleo ni shilingi bilioni 16.5 sawasawa na asilimia 11 tu, leo unasema pato la Mtanzania limeongezeka, limeongezeka wapi wakati miradi ya kilimo ni shida?

Mheshimiwa Naibu Spika, kule kwetu na karibu Tanzania nzima hivi ninavyosema ni wakati wa mavuno, wananchi sasa wanavuma pumba kwa sababu mipunga panya waliingia, mahindi panya waliingia wakahangaika wakulima mpaka sasa wakati wa mavuno watu hawavuni tena, halafu tunaambiwa ikitokea njaa Mkuu wa Wilaya, sasa kama panya wamekula halafu kilimo hamjawapa hela za kutoa wale panya hivi unadhani watu hawataomba tena

msaada? Mjiandae Wizara ya Fedha kuweka fungu maalum kwa ajili ya kuwasaidia Watanzania ambao wamekosa kuvuna sasa hivi mazao yao yote yaliliwa na panya. Siyo kwamba wavivu wamelima lakini uwezo wa kuvuna tena haupo, hiyo ni hali mbaya, sijui watu wengine kama wamevuna lakini kwangu hali ni mbaya sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hali hii imeendelea katika miradi yote, tumepiga kelele hapa Bunge zima, Serikali ilitenga shilingi bilioni 251 kwenye Miradi ya Maendeleo Vijijini, *(Local Government Development Grants*, kwenye mwaka huu tunaomaliza, Wakurugenzi wote Tanzania nzima na Wenyevitwa wa Halmashauri wakapuliza magari mafuta wakaharibu bajeti zao wakaja Dodoma, wakaambiwa mnapewa hela, leteni miradi ya mikakati, mkishaweka tu mkirudi pesa zinaingia. Mpaka leo hakuna senti tano iliyoingia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mkurugenzi wetu na Mwenyekiti wa Halmashauri alirudi Kilombero tukakaa vikao wakatimia pesa kwa ajili ya kuidhinisha miradi ya kimkakati, wananchi wamejenga madarasa, maabara, zahanati, mmesema mtaleta hela na mvua zitaingia ile miradi itakwenda kubomoka, nguvu za wananchi zitakwenda bure, halafu leo mnasema bajeti iko sawasawa, sawasawa gani ninyi? Acheni mambo yenu bajeti hewa hizo. Kwani tunaposema bajeti hewa ni zipi? Si ndiyo hizo za kudanganyana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa leo mnatuambia tupitithe tena bajeti, haya hii bajeti tunayoipitisha mtaitekelezaje wakati hii bajeti ya mwaka huu tunaenda kuomaliza mwezi huu hakuna kitu, hewa. Mnaharibu karatasi tu hapa hamna lolote, bora mngesema tu kwamba, hatuna hela, eti ninyi mnasema mna hela pato la Taifa limekua kwa asilimia 7.1 limekuakua vipi, mmekusanya wapi? Nini mmekusanya mpaka leo? *Cash budget*, mmekusanyaje hiyo bajeti, mnaishia kulipa madeni lakini kibaya zaidi mnaenda kukopa kwa biashara, halafu mnalipa madeni, nyie vipi? Nyie

mnadhani hatujui siri zenu mnazofanya? Mnajikazakaza tu, mnatumbua watu kila kukicha hamtaki kusema ukweli Watanzania huku wanaumia, watu hawalipwi mishahara yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeona wenzetu wa Uganda walimu tu hawakupandishwa mishahara wametangaza mgomo, hapa Tanzania, yaani sijui tumelogwa na nani? Ni haki kabisa ya kila mfanyakazi kupandishwa mishahara lakini mpaka leo hata senti tano, mnavunja sheria, kwa nini mnavunja sheria? Kama ninyi kweli mnakusanya pesa na mna pesa kwa nini mnashindwa kupandisha mishahara ya watu kwa mujibu wa sheria? Leo mnajitamba hapa tuna pesa, pesa ziko wapi? Pesa hamna, mkiambiwa ooh, mnakopa kopa tu. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wapandisheni wafanyakazi mishahara yao kwa mujibu wa sheria zilizowekwa. Hii Serikali ya Awamu ya Tano ni hatari kuliko Serikali zote zilizopita, nawaambia. Halafu leo vitabu unasema uchumi umekua, umekua kwa nani, labda umekua kwa ninyi mnaoshikashika hela huko Benki Kuu. Hela siyo zenu ni zetu halafu mnakuja hapa mnatudanganyadangnya. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi hii tulipofikia hali ni hatari hata wewe unajua, Waziri anajua kila mmoja anajua, lakini kwa vile mnaillinda Serikali ndiyo mnasema haya hamtaki tu kusema hali mbaya. Kama hali nzuri lipeni mishahara kwa Watanzania wanaolitumikia Taifa hili, kutwa mnatumbuatumbua. Kama pato la Mtanzania limekua, wale wafanyakazi waliotumbuliwa mpaka leo hawajui hatma yao pato lao limekua au limeondoka? Watanzania gani wanaowazungumzia? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hata ukiwa na kiwanja wakati wa JK utauza shilingi milioni 5 sasa hivi mpaka milioni 1 hupati mnunuzi. Ninyi nini ninyi! Eti pato limekua limekulia wapi wakati watanzania wako hoi. *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Hapo sasa.

**MHE. SUSAN L. KIWANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye kitabu chake amezungumzia Tume ya Taifa ya Uchaguzi waliidhinishia hela kidogo wakafika mpaka asilimia 300, acheni ubabaishaji, kwa nini kutumia hela nyingi za uchaguzi? Kwa sababu kazi yenu Awamu ya Tano kununua Madiwani na Wabunge halafu mnaenda mnafanya uchaguzi matokeo yake Tume ya Taifa ya Uchaguzi imeenda kutumia mpaka asilimia 300, acheni hizo. *(Makofi)*

### KUHUSU UTARATIBU

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU):** Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu utaratibu.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Susan Kiwanga Mchumi kutoka Mlimba, naona *Chief Whip* amesimama hapa. *(Kicheko)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU):** Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu utaratibu, pamoja na kumsikiliza sana Mchumi kama ulivyosema kutoka Mlimba, Mheshimiwa Susan hapa anasema tulichobakia hapa ni kununua Madiwani badala ya kushughulikia masuala ya msingi ya maendeleo ya wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nafahamu kabisa kwamba, hata yeye anafahamu ni kwa kiasi gani Serikali hii ilivyoweza kuboresha huduma nyingi ikiwemo huduma za afya katika nchi yetu ya Tanzania. Hata hivyo, nafahamu utaratibu wa uchaguzi katika nchi yetu ya Tanzania unazingatia sheria na taratibu zilizokuwepo na zilizowekwa. Kama kuna mtu anaona kabisa amedhulumiwa na katika uchaguzi hajashinda uko utaratibu wa kisheria wa kudai madai halisia kwa mujibu wa sheria. Kama hajafanya hivyo, nataka kumthibitishia kwamba hakuna Diwani ambaye ameshinda eti kwa sababu labda mmoja alinunuliwa na mwingine hakununuliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa naomba kwa mujibu wa utaratibu Mheshimiwa Susan atuthibitishie kama ana uhakika wa Diwani aliyenunuliwa na kama hana uhakika afute kauli hizo ili aweze kuendelea na mchango wake.

*(Hapa baadhi ya Waheshimiwa  
Wabunge walikuwa wakiongea bila mpangilio)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa *Chief Whip* tusaidie kanuni uliyokuwa unaisoma.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU):** Mheshimiwa Naibu Spika, ni Kanuni ya 64(1)(a), Mbunge hatatoa ndani ya Bunge taarifa ambazo hazina ukweli.

*(Hapa baadhi ya Waheshimiwa  
Wabunge walikuwa wakiongea bila mpangilio)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Heche, yaani kila siku unapenda jina lako liingie kwenye Taarifa Rasmi za Bunge kwamba, unapenda sana kuongeaongea. Tafadhali, tuwe tunasikilizana, lazima utajwe kwa sababu unavurugu za kuzungumza bila kusikiliza wenzako, kila wakati ni habari yako wewe tu, tafadhali.

Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Jenista Mhagama amesimama kwa mujibu wa Kanuni ya 64 akimtaka Mheshimiwa Susan Kiwanga aliyekuwa akichangia kwa mujibu wa fasili ya (1)(a) ambayo inamtaka Mbunge asitoe taarifa Bungeni ambazo hazina ukweli, lakini pia fasili ya (2) ndiyo inayotaka Mbunge huyo atakiwe kufuta kauli yake.

Waheshimiwa Wabunge, hili ni jambo kuhusu utaratibu na Mheshimiwa anaomba jambo hili lithibitishwe ama lifutwe kwenye Taarifa Rasmi za Bunge. Mambo haya si ya leo yalishawahi kutolewa utaratibu siku za nyuma. Tuhuma za namna hii zimeshawahi kuzungumzwa hapa ndani mara nyingi na tuhuma hizi zilishatolewa utaratibu. Kwa hivyo,



tunapokuwa tukitoa michango yetu tujielekeze kwenye yale mambo ambayo yanaruhusiwa kwa maamuzi ya kiti yaliyopita lakini pia kwa Kanuni zetu. Ndio maana mara zote Waheshimiwa Wabunge Kiti kinaposimama huwa nawasihhi sana tusikilizane ili usirudie makosa yale yale kila wakati.

Waheshimiwa Wabunge, mnafahamu wote kwamba vyama vyote vinapokea wanachama kila wakati, watu wakitoka huku, wakielekea huku na wengine wakitoka huku kuelekea kule. Tusilete mambo humu ndani yanayotupotezea wakati wetu sisi wenyewe. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, kwenye hili la hayo aliyoyasema Mheshimiwa Susan Kiwanga kwa sababu ndiye aliyekuwa anachangia nitamtaka afute hiyo kauli kwa sababu uamuzi wa hili jambo ulishatolewa siku za nyuma hakuna uamuzi mpya kuhusu jambo hili na ulitolewa humu ndani, kwa hivyo tujielekeze huko. Mheshimiwa Susan Kiwanga, jambo hili lilishazungumzwa humu ndani, lilishatolewa maamuzi kwa hivyo ufute kauli yako ili tuweze kuendelea mbele. Mheshimiwa Susan Kiwanga.

**MHE. SUSAN L. KIWANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, sijui dakika zangu umenilindia maana mara nyingi hawa Makatibu wako huwa wanasema na za Mheshimiwa Jenista tumeingiza mle mle, tutakuja kuonana wabaya.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa wewe futa halafu tuendeleo na mengineyo, futa hiyo kauli yako.

**MHE. SUSAN L. KIWANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nafuta kauli kwa sababu Watanzania wengi wanajua hilo.

**MHE. DKT. GODWIN O. MOLLEL:** Taarifa Mheshimiwa Naibu Spika.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Susan Kiwanga, naomba uifute kauli yako kwa unavyofahamu kikanuni na wewe sio Mbunge mpya humu ndani, futa kwa kadri kanuni zinavyokutaka, usianze *message sent*, sijui kitu gani, sijui

Watanzania wamefanya nini, futa kadri kanuni zinavyokutaka, tafadhali Mheshimiwa Susan. Mheshimiwa Hawa Mwaifunga tafadhali.

**MHE. SUSAN L. KIWANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nafuta kauli ili maisha yaendelee. *(Makofi)*

**MHE. DKT. GODWIN O. MOLLEL:** Taarifa Mheshimiwa Naibu Spika.

*(Hapa baadhi ya Waheshimiwa Wabunge walikuwa wakiongea bila mpangilio)*

**MHE. SUSAN L. KIWANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, wamenitoa kwenye reli ndio hao akina Shika hao, unamwona. *(Kicheko)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Susan, hapa nilikuwa nakusifia Mchumi wa Mlimba kwani kuna tabu gani huko Mlimba, leo umekujaje humu ndani mwenzetu, malizia muda wako.

**MHE. SUSAN L. KIWANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimalizie muda wangu kama alivyosema ndugu yangu hapa Mheshimiwa Nsanzugwanko pamoja na mipango yenu basi muangalie na sera ya nchi hii kuunganisha mikoa. Mimi natokea Mkoa wa Morogoro, kuna Mkoa wa Njombe unaunganika kwenye barabara Jimbo la Mlimba lakini tangu nilivyoanza kusema mpaka leo, *okay*, wamefanya upembuzi kiasi mpaka Mlimba lakini kutoka Mlimba mpaka Madeke Njombe hakuna upembuzi, hakuna kinachoendelea. Kwenye vitabu vyao vya Serikali sioni hata mafungu yanayotengwa kujenga barabara angalau waanze kidogo ili Mkoa wa Morogoro na Mkoa wa Njombe kupitia Mlimba ile barabara iunganishwe. Ndio maana wakati mwingine tunachangia hapa tunaona uchumi haujakuwa kwa sababu wananchi wa maeneo yale bado wanateseka na sera hazitekelezwi. *(Makofi)*

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha  
kwa muda wa mzungumzaji)

**NAIBU SPIKA:** Naambiwa muda wako umekwisha Mheshimiwa.

**WABUNGE FULANI:** Aaaaa.

**MHE. SUSAN L. KIWANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Makatibu hawa ni tatizo.

**WABUNGE FULANI:** Hajamaliza muda wake.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mwita Waitara, atafuatiwa na Mheshimiwa Mussa Ramadhan Sima, Mheshimiwa Aida Khenani atachangia dakika tano, tutamaliza na Mheshimiwa Emmanuel Papian John.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Nimepiga kelele sana humu ndani, nachangia kwa nguvu mno lakini mambo ni yale yale mpaka koo limeharibika sasa, leo nitachangia taratibu sitapiga kelele sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye taarifa ya Mheshimiwa ndugu yangu Mheshimiwa Dkt. Mipango, ukurasa wa 81 alikuwa anamlinganisha Mheshimiwa Magufuli na watu maarufu waliofanya mambo makubwa duniani. Sasa na mimi nimeingia kwenye *Google* hapa nikajaribu kuangalia, amemtaja mtu anaitwa Park Chung Hee, huyu amezaliwa mwaka 1917 na amekufa mwaka 1979 lakini alikuwa *assassinated* maana yake aliuwawa. Alikuwa mwanajeshi tangu mwaka 1944 mpaka 1945 na alikuwa cheo cha Jenerali halafu alikuwa ni Dikteta. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini mtoto wake pia wa kwanza alikuja akawa mwanamke wa kwanza kuwa Rais wa Korea. Kwenye historia inaonyesha tarehe 10 Machi, 2017 aliondolewa madarakani kwa kupinduliwa kwa tuhuma za rushwa. Historia inaonesha pia tarehe 6 Aprili, 2018, huyu

mwana mama aliyekuwa Rais wa Korea (*South Korea*) amefungwa jela miaka 24 kwa tuhuma za rushwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nilipoangalia historia hii nikasema haya maneno inabidi Mheshimiwa Dkt. Mpango ayafute kwa sababu Mheshimiwa Rais wetu hafanani na mambo ya namna hii. Afute maneno haya sio sawasawa. Nadhani Mheshimiwa Dkt. Mpango atakuwa labda ame-*quote* vibaya lakini hii uindoe historia imekaa vibaya, nilikuwa nataka nianze hapo. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nitatumia kitabu cha Mheshimiwa Mpango, ukiacha hilo andishi moja tu ambalo nimeona lina shida, ameandika maneno mazuri kwa sababu amekiri vizuri na nitapitia maeneo machache aliyosema ukweli. Nampongeza sana Mheshimiwa Mpango kwa kusema ukweli.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Mpango yeye ni msomi mchumi, mimi ni mwalimu sielewi, ni mwanasayansi tu wa kawaida lakini 2016 uchumi ulikua kwa asilimia 7, mwaka 2017 ulikua kwa asilimia 7.1, mwaka 2018 ulikua kwa asilimia 7.2. Mimi naomba Mheshimiwa Dkt. Mpango atusaidie hivi ukimueleza mtu wa kawaida yaani miezi hii kwa mwaka huu kwamba uchumi umekua ataelewa yaani Mbunge wake sielewi, atusaidie Watanzania waelewe, yaani hii ina-*reflect* vipi maisha ya kawaida ya wananchi? Kwa kweli hii napata nayo shida sana, unaweza ukaeleza hapa na fomula umeandika, wananchi wa kawaida wanataka kuona kama unasema uchumi unakua, mzunguko wa fedha mtaani uwe mkubwa uonekane, bidhaa ipatikane, watu wapate mahitaji ya kawaida. Sasa hiyo lugha hapa mimi siioni kwa kweli unisaidie Mheshimiwa Dkt. Mpango kwa utalaam wako.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye Bajeti ya Serikali 2016/2017 zilitengwa shilingi trilioni 29.5 hazikufika asilimia 80 katika utekelezaji wake. Mwaka 2017/2018 tulipitisha bajeti ya shilingi trilioni 31.7 sasa hivi taarifa inaonyesha ni asilimia 69 labda imeongezeka kabla ripoti haijaandaliwa. Hii bajeti ya sasa hivi ni shilingi trilioni 32.5, naomba unisaidie ni kwa

nini tusiende na bajeti halisi? Tumeshatenga bajeti miaka kadhaa iliyopita tumeona fedha yetu ya ndani ni kiasi gani, tumeona misaada ikoje na mingine inakwama halafu tuseme hapa sisi uwezo wetu ni shilingi trilioni 20, tupange mipango ya shilingi trilioni 20. Hapa ndipo malalamiko yanapokuja kwamba tunawapa watu matumaini makubwa, bajeti kubwa, mambo mengi lakini hayafanyiki, inaonekana tunadanganya, nadhani hili pia lifanyiwe kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini lingine ni kwenye ukurasa wa 14, Mheshimiwa Mpango amesema kiwango kikubwa cha umaskini kimekuwepo kwa Watanzania, ni maneno kwenye kitabu hiki cha hotuba. Anasema ukosefu wa ajira, sasa naomba unisaidie kwa hapa Mheshimiwa Dkt. Mpango. Maduka mengi yamefungwa huo ndio ukweli, watu wamefungwa biashara zao. Kama biashara zinafungwa maana yake mzunguko wa fedha unapungua, wananchi wa kawaida wale ambao waliokuwa wamepata ajira hawana ajira tena, uchumi unakuwaje hapa? Kwa hiyo, katika hili pia mliangalie.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kuna usafi wa kila Jumamosi, nimeona tu mahesabu ya kawaida, Watanzania wanaambiwa wafunge biashara zao kila Jumamosi asubuhi wanafungua saa nne haijalishi kama kuna famasi, kuna wagonjwa lakini wale mama lishe ambao wanapika chapati, wanaopika supu, huo ndiyo muda wa kupata hiyo huduma na hao wamejiajiri, sasa tunafanyaje hapa. Kwa hiyo, naomba mtuambie hii ratibu ya kila Jumamosi kufanya usafi tumepata faida kiasi gani na hasara kiasi gani ili tuweze kuamua maamuzi mengine tofauti na haya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine bar za Tanzania zinafunguliwa saa kumi zinafungwa saa tano usiku. Kule kuna Ma-*barmaid* walikopata ajira zao lakini kuna biashara zinafanyika wanalipa kodi. Kwa mfano, Dar es Salaam kuna foleni kweli kweli kama wewe umetoka mjini unafika nyumbani saa tatu, yaani unafika mtaani kwetu Kivule, Gongo la Mboto ni saa tatu usiku kwa mazingira ya Dar es Salaam, mwendo kasi haijafika. Maana yake hawa watakaa

pale saa mawili wanazungumza *bar* inafugwa na ma-*defender* yanakamata watu kweli kweli, hawa watu wanalalamika. Kama kuna sheria ilikuwepo siku nyingi kwa nini isibadilishwe twende na wakati? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, wenzetu Kenya hapa hao Usalama wa Taifa, Polisi wanatakiwa kuhangaika na watu ambao vipato vyao havijulikani wamepataje. Kama kuna mtu anakunywa, anakula, anavaa vizuri, ana magari mazuri hatujui kazi yake, hiyo ndiyo kazi ya Usalama wa Taifa kuwatafuta watu ambao wana vipato ambavyo havieleweki. Kenya hapo Nairobi huduma ni saa 24, biashara inazunguka, kila mtu anafanya kazi yake, watu wawajibike. Kwa hiyo, tusitengeneze mazingira ya kutisha watu, wafundishwe ustaarabu na wajitegemee na wafanye maamuzi sahihi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ukurasa wa 15 amezungumza habari ya kilimo, mifugo na uvuvi na amesema mwenyewe hizi sekta tatu zinawaajiri Watanzania asilimia 66. Sasa nimuulize Mheshimiwa Dkt. Mpango kwenye bajeti hii malalamiko yote ambayo Wabunge wamesema kwenye kilimo watu wamelima mazao ya pamba, tumshukuru Mheshimiwa Waziri Mkuu amechukua hatua lakini hata mahindi mpaka unaenda kwenye msimu mwingine haya mazao bado yapo mtaani. Mifugo imepigwa, imeteswa hakuna malisho, hakuna sehemu ya kuchungia, ugomvi na wakulima, Operesheni Sangara, leo mmezungumza habari ya samaki, haya mambo Mheshimiwa Mpango mngeyachukua mkakae pamoja mkayafanyia kazi mkatengeneza Taifa ambalo tunataka kwenda mbele badala ya kurudi nyuma tusirudie mambo yaleyale ya kila siku.

Mheshimiwa Naibu Spika, iko hoja hapa Mheshimiwa Jenista ametoka nje, tulipokuwa tunajadili habari ya kuunganisha Mifuko ya Hifadhi ya Jamii tulilalamika hapa kwamba ile *formula* iingizwe kwenye sheria. Waheshimiwa Wabunge ile *formula* haijaingizwa, sasa hivi kuna ugomvi mkubwa kati TUCTA na Serikali na wameshusha, ilikuwa <sup>1/</sup><sub>540</sub>

sasa imeenda  $\frac{1}{580}$ . Mafao kwa mkupuo ilikuwa asilimia 50 kwa formula hii ambayo inalazimishwa wataalipwa asilimia 25,. Kwa mkupuo walikuwa wanalipwa asilimia 50 imeshuka zaidi ya nusu kwa yale mafao na kuna ugomvi mkubwa. Tullilalamika sheria iingizwe haijaingizwa wametunga kanuni. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, hii ina madhara kwa sababu hawa watumishi ambao, kwa mfano watu wa *LAPF*, *PSPF* wanaidai Serikali siyo chini ya shilingi bilioni 600 za madeni hayajalipwa na huu mzigo ni wa Serikali, hawa wastaafu wanachama wa vyama hivi ndiyo wataingia kwenye mzigo huu na hili ni janga la Taifa. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kama hauongezi mshahara Mheshimiwa Dkt. Mpango hawa wakienda kustaafu *calculation* ya mafao yao mwishoni inategemea *increment* ya kila mwezi. Ndiyo maana tunasema fuateni taratibu watu waongezwe pesa zao zitawasaidia siku za mbele katika maisha yao. Watu wanakufa haraka kwa sababu ya kukosa huduma nzuri. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nishauri jambo muhimu sana hapa, kwa mfano, kwenye Wizara ya Elimu ametaja data ndugu yangu Mheshimiwa Paresso sitaki kurudia yaani ukiangalia *figure* ya matundu ya vyoo, madarasa, nyumba za walimu, upungufu wa walimu, mimi nadhani Mheshimiwa Dkt. Mpango akija atuambie kwenye bajeti hii haya mambo yatatekelezwa kwa kiasi gani. Wabunge wamelalamika mmechukua kodi ya majengo, kodi ya mabango kwenye maeneo mbalimbali tumeathirika, haujarudisha asilimia Mheshimiwa Mpango, ungetuambia fedha hii imerudishwa kwa kiasi gani, haya mambo yangefanyika ingetusaidia. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nishauri jambo muhimu sana, kuna maneno mengi sana yanaendelea na kwa sababu mambo yanafanyika kwa haraka haraka sana kwa mazingira fulani hisia zinakuwa nyingi sana mtaani. Kwa mfano, mimi nimesoma ule Waraka wa Watumishi wa Mungu

wa Waislam na Wakristu, mambo ambayo yametajwa, wanashauri hivi, tuwe na utawala bora, tufuate sheria, hii nchi haiongozwi kwa llani za vyama na matumizi mabaya ya dola. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano, hivi haya mambo ya kutishiana, haya mambo ya kufuata utaratibu kuna kosa gani, Taifa hili humu ndani tumebaguana sana kivyama. Wabunge wa CCM, Wabunge wapinzani wakijadili wanadhani wengine wana haki zaidi kuliko wenzao kumbe Taifa ni la kwetu sisi wote. Tungeona tu kwamba hawa watu wanashauri, mimi nikitoa hoja ingepokelewa kwa nia njema kabisa kwa kujenga Taifa. Hii bajeti ni ya kwetu na ikipita siyo ya CCM ni bajeti ya Watanzania, iwe tumeunga mkono au hatujaunga, tusaidieni kupeleka Taifa mbele kwa kutuunganisha. *(Makofi)*

*(Hapa kengele illia kuashiria  
kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa muda wako umekwisha, ahsante sana.

Tunaendelea na Mheshimiwa Mussa Ramadhan Sima, atafuatiwa na Mheshimiwa Aida Khenani dakika tano, Mheshimiwa Emmanuel Papian John ajiandae.

**MHE. MUSSA R. SIMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue fursa hii kumshukuru sana Mwenyezi Mungu lakini pia niwapongeze Mheshimiwa Waziri na Naibu wake kwa bajeti hii ambayo mipango yake imekaa vizuri, yapo maeneo ambayo tunapaswa kuishauri Serikali vizuri sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, tuliweke jambo moja sawa, unajua mnyonge mnyongeni haki yake mpeni, Mheshimiwa Dkt. Mpango alisema vizuri sana, amesoma vitabu vya viongozi hawa amejifunza *best practice* na *worse practice* sasa afute nini? Mheshimiwa Dkt. Mpango nikupongeze sana. Nadhani mimi nilikuelewa vizuri wakati umezungumza na hiyo



itakuwa imetusaidia sana lazima ujifunze sehemu zote mbili.  
(Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imejikita katika uchumi wa viwanda utakaochochea ajira na ustawi endelevu kwa jamii. Likisemwa hivi kwenye bajeti maana yake lazima tuone *indicator* za kuelekea kwenye uchumi wa viwanda. Serikali imeeleza vizuri imepunguza *Corporate Tax* kwenye kilimo lakini kwenye bidhaa za ngozi, nataka nijielekeze kwenye bidhaa za ngozi. Tukizungumzia bidhaa za ngozi ni lazima tujue kama viwanda vyenyewe vya kutengeneza ngozi vipo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka hapa tujielekeze vizuri sana, tulikuwa na viwanda vya ngozi mimi sidhani kama vipo. Leo Mwanza hatuna kiwanda cha ngozi, ile Mwanza Tannery imebaki kuwa *go-down*. Ukienda Arusha kipo kiwanda kimoja kazi yake kubwa ni kutengeneza *wet blue*, inalainisha tu ile ngozi na kuisafirisha kwenda nje. Tuna Himo Tannery na tuna Kiwanda cha *Moshi Leather* ambacho kimefungwa. Morogoro tulikuwa na kiwanda pale na chenyewe kimefungwa kilikuwa kinafanya *temporary*.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nataka kujiuliza tumepunguza kodi kutoka asilimia 30 kwenda 20 kwenye bidhaa za ngozi wakati viwanda hamna. Nataka Serikali itusaidie hapa na nishauri vizuri, leo bidhaa ya ngozi hii tunayoizungumza ngozi yenyewe imeshuka thamani. Ngozi leo kilo moja inauzwa Sh.200 mpaka Sh.500 lakini hivyo viwanda viwili vinavyofanya *finishing* kwa maana ya Himo na Moshi Tannery, Himo tu kinaweza kununua ngozi tani 100 peke yake, Dar es Salaam peke yake inazalisha kwa siku ngozi tani 45 maana yake Dar es Salaam peke yake inaweza ikalisha hivi viwanda viwili basi, kwa hiyo, mikoa yote hii ikiwemo na Singida ngozi yetu imekosa thamani.

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa lazima tuishauri Serikali vizuri na iwe makini kwenye jambo hili. Tunapotaka kuonesha *indicator* kwenda kwenye viwanda kuna eneo la muhimu sana, tunataka mashine ziingie humu lakini kwenye *Customs*

*Duty* ni lazima tuondoe *Import Duty* na *VAT* asilimia 18. Itakuwa imetusaida mno kwenye eneo hili ili viwanda na mashine ziingie ili tuweze kuanzisha hivi viwanda tofauti na hapo hatuwezi kuwa na uchumi wa viwanda lakini bidhaa tunazo. Ngozi hii tunayoizungumza ukitaka kuitoa nje unalipa kodi asilimia 80 maana yake ngozi ambayo umeinunua kilo Sh.500 unalipa kodi Sh.1,200 utaenda kuiuza wapi lakini ngozi inateseka leo. Nataka niombe Serikali wakati tunajiandaa kuweka viwanda hivi iruhusu ngozi hii iuzwe ili Serikali ipate mapato na wananchi waweze ku- *survive*. Kwenye eneo hili nilikuwa nataka niombe Serikali iliweke vizuri sana taarifa hii haiko sawa. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini hata kwenye kilimo, nchi yetu leo kilimo ni uti wa mgongo kuondoa *Corporate Tax* kwa asilimia 10 peke yake haitoshi. Nashauri tuweke *zero* tu kabisa walau kwa miaka miwili itatusaidia sana ku-*promote* eneo hili la kilimo. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, ziko *Regulatory Authority* *TFDA*, *TBS*, *TPRI*, *NEMC*, Vipimo na wengine wengi. Tumezungumza sana kwenye bajeti iliyopita kwamba ifike mahali tu-*harmonize* hizi *Regulatory Authority* zote zinafanya kazi moja. Kila mmoja anakwenda kwa mfanyabiashara anatoza ada. Sasa tukaomba tufanye *One Shop Stop Center* nataka kusema leo hii nayo haiwezekani hawa wote wanafanya kazi ya Serikali, niombe Serikali ilipwe ada moja tu ya mfanyabiashara kulingana na kiwango; kama mfanyabiashara ana mtaji wake wa Sh.100,000 mpaka Sh.10,000,000 *whatever* alipe ada moja tu hawa kazi yao waende wakatoe *certificate*, basi. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, aende kwenye kiwanda kwa mfanyabiashara akague atoe taarifa Serikalini siyo na yeye aende akatoze faini na yeye anataka ada, hatuwezi kufika. Tunataka *indicator* hizi ziwekwe sawa. Kama tunataka uchumi wa viwanda hizi *Regulatory Authority* ni sehemu ya kumomonyoa hatuwezi kufika, ilipwe ada moja tu Serikalini. Mtu akilipa ada moja hawa kazi yao waende wakafanye *auditing* kuangalia kama hiyo bidhaa ni halali ama sio halali

watoe taarifa Serikalini. Wanalipwa mshahara na Serikali lakini hawana sababu ya wao kuanzisha vyanzo vya mapato. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, niipongeze Serikali kwenye eneo moja la *betting*, amezungumzia Sheria ya Michezo ya Kubahatisha (*sport betting*) imeongeza kodi kutoka asilimia 6 mpaka 10 lakini kwenye *slot mashine* Sh.35,000 mpaka Sh.100,000. Tukizungumzia *sport betting* maana yake tunazungumzia Watanzania sasa wameamka na mwamko huu ni wa eneo la soka, wapenzi na wanachama wa soka wameona sasa kuna haja ya kuingia kwenye eneo hili na Serikali inapata mapato.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa isiishie hapo, nataka nioneshe na eneo lingine kila mchezo wa soka unaochezwa Tanzania kwenye viwanja vyetu tunalipa VAT baada ya kutoa yale mapato yote *get collection* wanatoa asilimia 18 inayobaki ndiyo wanaita asilimia 100 wanaanza kugawana. Naiomba Serikali kwenye eneo hili tunataka kuboresha michezo Tanzania na tuboreshe mchezo huu wa soka ili tupate mapato zaidi maana yake hii asilimia 4 na hii shilingi sabini na kitu inayoongezeka tuwape Baraza la Michezo la Taifa ili liweze kujielekeza kuhakikisha kwamba tunapata viwanja na kuboresha mchezo huu wa soka. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, Tanzania hii leo hata ukipewa msaada wa vifaa vya michezo kutoka nje maana yake unalipa kodi. Sasa niombe Serikali vifaa vya michezo hivi hebu viingie bure hatuna sababu ya kulipa *Import Duty* wala VAT sababu tunaboresha michezo Tanzania. Nataka niombe sana Serikali eneo hili ili angalie vizuri sana. Hata ile asilimia 18 ya *get collection* ambayo inapatikana kwenye viwanja wapeni Baraza la Michezo waweze kuboresha michezo yetu. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna eneo lingine la wafanyakazi hapa, niipongeze Serikali kwa kuweka *single digit* kwenye *Income Tax* lakini *single digit* tunayoizungumza hapa inazungumzika kwenye eneo la kima cha chini, hao

wengine inaendelea kama kawaida. Serikali izungumze *single digit* kwenye *Income Tax* kwenye mshahara wote bila kujali kima cha mshahara cha mtu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimpongeze Mheshimiwa Waziri Mkuu alifafanua vizuri sana kuhusu mishahara ya wafanyakazi, sina sababu ya kurudia eneo hili kwa sababu ya muda lakini nataka niombe eneo moja muhimu sana. Tangu Serikali imeingia madarakani mwaka 2015 tulianza zoezi la uhakiki la wafanyakazi tukasimamisha madaraja ya watumishi wakiwemo walimu, madaraja haya yamesimama mpaka leo. Maana yake mtu aliyeanza kazi 2015 na 2012, 2018 tutawakusanya pamoja waweze kulipwa daraja moja, *this is unfair*, halitakubalika. Niombe kama alistahili kupanda daraja 2015 kama anaenda daraja D, mwaka 2018 alipaswa kuwa daraja E apewe daraja lake la sasa E na tusirudi huko kumpa daraja D, tutakuwa tumemuonea. Nataka niombe sana Serikali kwenye eneo hili itusaidie ihakikishe watumishi wetu wanapata haki yao. Hawa watumishi hawana kosa lolote, uhakiki ulikuwa ni wa kwetu wenyewe Serikali siyo wa watumishi, tutoe mwongozo huu. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie eneo lingine la *PPP (Public Private Partnership)*. Nataka niende haraka hapa nitolee mfano, leo eneo la UDART pale Dar es Salaam kwenye usafirishaji mwendokasi mradi ule unakufa lakini Serikali tuna asilimia 49, mtu anaye-*hold share* na sisi ana asilimia 51, mradi unakufa. Mradi unakufa kwa sababu gani na Serikali imekaa kimya?

Mheshimiwa Naibu Spika, miradi mingi tunaendelea nayo, juzi Mheshimiwa Rais amezindua *Agricultural Sector Development Program Phase II* lakini *Phase I* hatujaitathmini ikoje. Hapa tunazungumzia *PPP*, hata tunapokwenda kwenye *standard gauge* tunatarajia kwenda kwenye *PPP* tutakwendaje? Niombe Serikali ituletee taarifa kuhakikisha miradi hii ya *PPP* inatusaidia. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. (Makofi)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Tunaendelea na Mheshimiwa Aida Khenan dakika tano, tutamalizia na Mheshimiwa Emmanuel Papian John.

**MHE. AIDA J. KHENAN:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Kwa kuwa dakika tano ni chache sana kuna mambo nategemea Waziri atakuja kutoa ufafanuzi ili tuweze kuelewa. Unapozungumzia kukua kwa uchumi leo katika kilimo wakulima wa mahindi ambao mwaka jana waliweza kuuza mahindi yao gunia Sh.60,000 leo ni Sh.24,000. Kwa hiyo, unapozungumzia kukua kwa uchumi mtuambie umekua sehemu gani.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo katika Taifa hili nimekaa nimefanya tafakari kubwa ni nani ana amani, mfanyakazi hana utulivu kwa sababu alitegemea sheria itamlinda kuongezeka kwa mshahara wake leo mshahara hauongezwi, mkulima hana amani kwenye Taifa hili, hali ya kilimo ni mbaya, njoo kwa wavuvi, njoo kwa wafanyabiashara, nani ana utulivu kwenye Taifa hili. Mheshimiwa Waziri wa Fedha wewe ndiyo unaweza kumshauri Rais vizuri kama unaweza kusikiliza mawazo ya Wabunge tunayozungumza humu ndani.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo mfanyabiashara anajiona ni kama mkimbizi ndani ya Taifa lake. Ni kwa nini mmeshindwa kutengeneza mazingira rafiki kwa wafanyabiashara ni kutoza kodi zisizokuwa na sababu. Leo TRA wanajua hali ya uchumi ni mbaya lakini wakiamua kufunga wanafunga, huwezi kukamua maziwa ng'ombe usiyemlisha, unategemea wao wanapata wapi pesa. Taifa hili unategemea wakulima, wavuvi, wafanyakazi, leo watu hawa wote wako kwenye wakati mgumu Taifa tunaliendeshaje? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sera ya kulinda uchumi wa Taifa. Tuliopo humu ndani siyo kwamba wote tumesoma uchumi tuko kwenye *facult* tofauti tofauti lakini ni pale ambapo unaweza kuchukua mawazo yetu ukaoanisha na

taaluma yako kuweza kulipeleka Taifa mbele. Kama utachukua mawazo yako binafsi ndiyo haya tunarudi tena kuzungumza ndani ya Bunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vijana kama mimi wana wakati mgumu kwenye Taifa hili, ajira ni shida, wamejiingiza kwenye kilimo, kilimo hicho ndiyo imekuwa taabani hili Taifa tunalipeleka wapi? Waziri wa Fedha ukisema uchumi unakua wewe ndiyo unayempotosha Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania hali ni mbaya kuliko hiki unachokiandika, hii hali ni nzuri kwa nani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunapozungumza mazingira wezeshi kwa wafanyabiashara ni lazima tuangalie hawa wafanyabiashara wanapolipa kodi wanategemea wayaone matokeo ya kodi wanayoilipa. Leo hakuna matokeo yoyote ambayo yanaweza yakawaletea tija na wao kujisukuma kuweza kulipa kodi. Leo wanaona ukiwa mfanyabiashara ni bora ukae nyumbani. Hili suala ambalo tunazungumza kwamba mfanyabiashara ukimuelimisha akajua umuhimu wa kodi na akayaona matokeo hakuna ugomvi utakaotokea kwa sababu faida ya kulipa kodi anaiona. Leo mnatumia nguvu kuliko kutumia busara na maarifa inatuweka kwenye wakati mgumu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hili Taifa sio la Waziri wa Fedha ni Taifa la Watanzania, hiki unachokiandika unategemea kodi za Watanzania wakiwemo wakulima, wafanyakazi pamoja na wafanyabiashara. Ukijifungia mwenyewe ukaja na hizi takwimu unazozileta hapa zitaisha kwenye kitabu na haitakusaidia. Kwa sababu ulipoteuliwa na Rais aliamini ukija humu ndani utasikiliza mawazo ya Wabunge na sio mawazo yako. Haya mawazo tunayokwambia sisi kwamba unapozungumza hali ya uchumi umepima kwenye kipimo gani, ni kipimo gani ambacho umekitumia, wafanyakazi wanalia, wakulima wanalia, wafanyabiashara wanalia, wewe hizi takwimu unazipata wapi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ndani ya Bunge pia tuna wakati mgumu na ndiyo maana tunasema Mheshimiwa Waziri wa Fedha zungumza ukweli. Ni lazima mbadilishe *approach* na Taifa lolote makini linakuwa na vipaumbele na kipaumbele sio cha kwako ni kipaumbele ambacho kinawagusa Watanzania na maisha halisi ya watanzania. Leo ukienda kwenye uhalisia hiki ulichokiandika haujaonesha mkakati wowote...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Muda wako umekwisha Mheshimiwa, ahsante sana. Mheshimiwa Emmanuel Papian John atakuwa ndio mchangiaji wetu wa mwisho.

**WABUNGE FULANI:** Hayupo.

**NAIBU SPIKA:** Nadhani ametoka kidogo.

Waheshimiwa Wabunge, tumefika mwisho wa uchangiaji wetu kwa leo. Nitaleta matangazo niliyonayo hapa halafu nitatoa taarifa kuhusu mwongozo uliokuwa umeombwa na Mheshimiwa Charles Kitwanga asubuhi.

Waheshimiwa Wabunge wote wa Chama cha Mapinduzi wanatangaziwa na Mheshimiwa Jasson Rweikiza, Katibu wa Wabunge hao kwamba mara baada ya Bunge kuahirishwa jioni hii wanatakiwa kufika Morena Hotel. Naamini wanakaribishwa na wale wanaotaka kuhamia labda. *(Makofi/Kicheko)*

### **MAJIBU YA MWONGOZO**

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, niliombwa mwongozo leo asubuhi na Mheshimiwa Charles Kitwanga kuhusu tangazo nililokuwa nimelitoa kuhusu taarifa zinazotakiwa na Sekretarieti ya Tume ya Madili za uthibitisho wa mali na madeni ya Waheshimiwa Wabunge yaliyoko

ndani ya nchi na pia nje ya nchi. Wakati nikisoma tangazo lile nilitoa taarifa kwamba tarehe ya mwisho iliyotolewa kwa wale ambao walikuwa wamepata taarifa mapema za kutakiwa kuwasilisha uthibitisho huo itakuwa ni tarehe 25 Juni, 2018. Sasa nilisema baadaye tutatoa taarifa kuhusu wale ambao walikuwa hawajapewa taarifa kuhusu kutakiwa kupeleka uthibitisho huo na kwamba tarehe yao tungeitaja baadaye baada ya kufanya mawasiliano na wenzetu wa maadili.

Waheshimiwa Wabunge, sasa nimeletewa taarifa na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kuwa kama tulivyokuwa tumesema asubuhi kwa wale ambao mwezi Januari, 2018 walitakiwa kuwasilisha vielelezo na ambao hawajawasilisha mpaka sasa wafanye hivyo kabla ya tarehe 25 Juni, 2018. Kwa wale ambao hawakutakiwa kufanya hivyo ama hawakupewa taarifa hiyo Januari sasa watapeleka vielelezo vyao katika Ofisi zao za Kanda kabla ya tarehe 31 Agosti 218. Hawa wanaweza sasa kupeleka taarifa zao kwenye Ofisi za Kanda na ili tuende vizuri Ofisi za Kanda nitazirudia kuzisoma kwa haraka ili Waheshimiwa Wabunge mmpesheleke huko taarifa baada ya kurudi majimboni na kupata hivyo vielelezo.

Kwa upande wa Dar es Salaam, Ofisi ya Kanda ya Dar es Salaam itahudumia Dar es Salaam na Zanzibar. Upande wa Kanda ya Mashariki, Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Pwani Kibaha itahudumia Pwani, Morogoro na Tanga. Kanda ya Kaskazini Arusha A/CC itahudumia Arusha, Kilimanjaro na Manyara. Kanda ya Kati Dodoma Kilimani itahudumia Dodoma na Singida. Kanda ya Magharibi Tabora itahudumia Tabora, Kigoma na Simiyu. Kanda ya Ziwa (Mwanza) itahudumia Mwanza, Geita, Kagera, Shinyanga na Mara. Kanda ya Kusini (Mtwara), itahudumia Mtwara, Lindi, Ruvuma. Kanda ya Nyanda za Juu Kusini (Mbeya NBC House) itahudumia Mbeya, Iringa, Njombe, Katavi, Songwe na Rukwa. Naamini Kanda ya Ziwa itahudumia pia Wabunge wanaotoka Simiyu.



*NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kuyasema haya, naahirisha shughuli za Bunge mpaka siku ya kesho, tarehe 20 saa tatu asubuhi.

*(Saa 01.20 Usiku Bunge Liliahirishwa  
Hadi Siku ya Jumatano, Tarehe 20 Juni, 2018)*